**1 JUNI, 2022**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Thelathini na Tano – Tarehe 1 Juni, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**MHE. JULIANA D. MASABURI K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na

Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu!

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali tunaanza na ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 305

### Hitaji la Gari la Wagonjwa – Hospitali ya Wilaya Mkalama

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itapeleka gari la kubebea Wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mkalama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama ina gari moja la kubebea wagonjwa ambalo lipo katika Hospitali ya Wilaya ya Mkalama na linahudumia Vituo vingine vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 itanunua magari 195 ya kubebea wagonjwa ambayo yatapelekwa kwenye Halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Hospitali ya Wilaya ya Singida Vijijini, inakabiliwa na ukosefu wa gari la kubebea wagonjwa. Je, ni lini Serikali itapeleka gari katika hospitali hii ili kuokoa vifo vya kinamama wajawazito na watoto?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa kituo cha afya cha Sepuka, kiko pembezoni na hakina gari la kubebea wagonjwa. Je, ni lini Serikali itapeleka gari katika kituo hiki cha afya?

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwali kwamba ni kweli kwamba Hospitali ya Halmashauri ya Singida Vijijini inahitaji gari la wagonjwa na Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuwajali wananchi wote katika Halmashauri zetu kote nchini itapeleka magari ya wagonjwa ndani ya mwaka huu wa fedha au mapema mwaka ujao wa fedha ikiwemo Halmashauri ya hii ya Singida Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Kituo cha Afya cha Sepuka ambacho kiko pembezoni, tumefanya tathmini ya kuona vituo ambavyo viko pembezoni ambavyo vinahitaji magari ya wagonjwa vitapelekewa magari ya wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, amekuwa akifuatilia sana masuala ya maendeleo ya wananchi wa Mkoa wa Singida na Watanzania kwa ujumla nimhakikishie kwamba tutaendelea kumpa ushirikiano.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nataka nimuulize swali Naibu Waziri, kuna

Halmashauri zingine zina Majimbo zaidi ya mawili au matatu, sasa kama mtapeleka gari moja, hilo gari litaenda kwenye Jimbo gani? Kwa nini usiweke wazi, kwa nini isiwe kwa Majimbo badala ya kuwa Halmashauri? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Mwenisongole, Mbunge wa Jimbo la Mbozi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa kupeleka magari ya wagonjwa kwenye Halmashauri unazingatia vigezo, kigezo cha kwanza ni idadi ni ya watu katika Halmashauri, kigezo cha pili ni idadi ya wagonjwa kwa maana ya *burden of disease* katika Halmashauri husika. Utaratibu huu hauzingatii Majimbo kwa sababu Majimbo pia yanatofautiana na idadi ya wananchi ukilinganisha na Halmashauri. Kwa hiyo, tutakwenda kupeleka magari haya, kwa kigezo cha Halmashauri na idadi ya watu na *burden of disease.* Pale ambapo itahitajika kwa Majimbo mawili kupata gari tutafanya hivyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, sasa aulize swali lake.

Na. 306

**Serikali kusaidia juhudi za wananchi katika ujenzi wa Vituo vya Afya**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa Vituo vya Afya Kata za Mundindi, Lupingu, Lupanga, Ludende, Madilu, Ludewa, Lugarawa na Mawengi utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Jimbo la Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 imekwishapeleka Shilingi Milioni 500 kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kwa ajili ya ukamilishaji wa Kituo cha Afya Mundindi kilichopo katika Kata ya Mundindi. Ujenzi wa jengo la la wagonjwa wa nje (*OPD*) na maabara umekwishakamilika na majengo mengine yapo kwenye hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeainisha maeneo ya kimkakati ya kujenga vituo vya afya katika Wilaya ya Ludewa kwa awamu kadri ya bajeti ya Serikali. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, pamoja na

hivyo naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa wananchi wa Ludewa wamevuja jasho sana kuanza ujenzi kwenye Kata 12, Je, ni lini Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuambatana na mimi ili kwenda kushuhudia jinsi wananchi walivyojitoa kutoa kujenga vituo vya afya na havijamaliziwa na Serikali?

Swali la pili, kwa kuwa Tarafa ya Mwambao haina usafiri wa magari na meli kwa muda mrefu haipo. Je, ni kwanini Serikali isitafute boti moja ya mwendokasi ambayo itasaidia wagonjwa kuanzia Lumbila, Kilondo, Makonde, Lifuma, Mkali mpaka Manda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Jimbo la Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kamonga, amekuwa akifuatilia sana miradi ya maendeleo kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Ludewa, ikiwemo vituo vya afya na magari ya magonjwa. Kwa kweli katika Kata hizi 12 ambazo wananchi wamechangia nguvu zao kujenga vituo vya afya, nimhakikishie kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuunga mkono juhudi za wananchi kukamilisha vituo hivi.

Mheshimiwa Spika, nitoe maelekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, kwa mwaka ujao wa fedha baada ya mwaka huu ambao tumeshaupangia bajeti atenge fedha kwa ajili ya kujenga maabara na kichomea taka kwenye vituo ambavyo wananchi wameshaweka nguvu zao, ili huduma za *OPD* zianze na Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na *ambulance*, boti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafanya tathmini maeneo yote ambayo ni magumu kufikika ya visiwa na ambayo yanapitiwa na mikondo ya maji, tuangalie uwezekano wa kupata *ambulance* hizi za boti kwa kadri ya upatikanaji wa fedha na tutatoa kipaumbele kwenye Wilaya ya Ludewa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kufahamu ni lini Serikali itatujengea Kituo cha Afya, katika Kata ya Bara ili kupunguza idadi ya vifo vya mama na mtoto katika Wilaya ya Mbozi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juliana Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mkakati, kwanza wa kukamilisha vituo vyote zahanati na hospitali za Halmashauri ambazo zimekamilika lakini hazijaanza kutoa huduma. Baada ya hapo tutakwenda sasa kujenga vituo vya afya kwenye maeneo ya kimkakati likiwemo eneo hili ambalo Mheshimiwa Juliana Shonza amelisema.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie kwamba tutakwenda kuhakikisha kwamba tunajenga pia kituo cha afya baada ya kukamilisha vituo vingine.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mnaopata fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza, swali la msingi linahusu ujenzi wa vituo vya afya, sasa tusije tukachanganya mambo hapa. Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Miula Jimbo la Nkasi Kusini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaweka mkakati wa kuainisha maeneo ya kujenga vituo vya afya, ikiwemo katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, kwa hivyo, kadri ya upatikanaji wa fedha katika bajeti inayofuata

tutahakikisha tunatenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo vya afya katika maeneo hayo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Jimbo la Tabora Mjini lenye Kata 29 kuna Kata ya Tumbi pamoja na Kata ya Misha tayari vituo vya afya vimeashaanza kujengwa na vipo katika hali ile ya kumalizia. Ni lini Serikali italeta fedha hizi za kumalizia vituo hivyo vya afya viwili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini kama ifutavyo: -

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba kata nyingi bado zinahitaji vituo vya afya, lakini Kata za mkakati tumekwishaziainisha na Waheshimiwa Wabunge, walileta Kata za kipaumbele tatu kila Jimbo, niwahakikishie kwamba Serikali inaendelea kuandaa bajeti kwa ajili ya kuendelea na ukamilishaji wa vituo hivi vya afya, vikiwemo hivi vituo vya afya viwili ambavyo vipo katika Jimbo la Tabora Mjini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Serikali ndiyo ilihamasisha ujenzi wa vituo vya afya katika maeneo mbalimbali nchi nzima na kuwahamasisha wananchi washiriki lakini leo hazijakamilisha. Je, mliamua kuwahamasisha wananchi bila kuwa na fedha za kutosha ndiyo maana kila Mbunge leo anaulizia kituo cha afya. Kwa nini sasa msikamilishe wakati ninyi ndiyo mliwahamasisha wananchi?

**SPIKA:** Swali ni moja Mheshimiwa la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tukubaliane kwamba kuhamasisha wananchi kuchangia nguvu zao katika ujenzi wa vituo vya afya ni dhamira njema na jambo jema kwa sababu wananchi wetu wamekuwa wanasafiri umbali mrefu sana kupata huduma za afya. Kwa hiyo, kwa kuanza tu jambo hilo lilikuwa ni jema na nia njema ya Serikali lakini tumeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma.

Mheshimiwa Spika, mwaka uliopita maboma 555 ya zahanati Bilioni 33.5 zilipelekwa, mwaka huu tumepeleka katika maboma zaidi ya 234 ya vituo vya afya na zahanati. Mwaka ujao tunayo maboma 300 ya zahanati ambayo yanakwenda kukamilishwa. Kwa hiyo, Serikali inafanya kazi ya kukamilisha maboma hayo kwa nia njema ya kusogeza huduma kwa wananchi, lakini safari ni

hatua, tutakwenda kwa awamu mpaka kukamilisha majengo hayo yote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi sasa aulize swali lake.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi, naomba sasa swali lake Namba 307 lipate majibu ya Serikali.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, inabidi nimtaje kwanza ndiyo aweze kuuliza swali. Mheshimiwa Florent Kyombo kwa niaba ya Mheshimiwa Dennis Londo.

Na. 307

**Kuunganisha baadhi ya Kata za Mikumi kwa Barabara**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO K.n.y. MHE. DENNIS L. LONDO** aliuliza: -

Je Serikali ina mpango gani wa kuunganisha barabara Kata za Ulaya, Kisanga, Malolo na Uleling'ombe katika Jimbo la Mikumi?

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Deniss Lazaro Londo Mbunge wa Jimbo la Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali inaifanyia matengenezo barabara ya Kidodi – Vidunda yenye urefu wa kilomita 4.14 ambayo itawezesha uunganishaji wa Kata za Vidunda na Kidodi. Pia, ujenzi wa daraja la Ruhembe kwa gharama ya Shilingi Bilioni 1.00 utawezesha kuunganisha Kata za Ruhembe na Kidodi.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2022/2023, *TARURA* imetenga Shilingi Bilioni 1.00 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Ulaya – Kisanga kilomita 42.1 ambayo itaunganisha Kata za Ulaya na Kisanga. Aidha, kiasi cha Shilingi Milioni 500.00 zimetengwa kwa ajili ya ukamilishaji wa daraja la Ruhembe linalounganisha Kata za Ruhembe na Kidodi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kuunganisha Kata ya Malolo na Uleling'ombe katika Jimbo la Mikumi kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Florent Kyombo swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Lazaro Londo, inaonekana fedha ambayo imetengwa kwa ajili ya barabara hiyo haitoshi. Sasa ni nini *comment* ya Serikali kuhakikisha kwamba barabara hiyo inatengewa fedha za kutosha ili iweze kujengwa na kukamilika na wananchi waitumie?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, barabara hii ya Kisanga, Malolo na Uleling'ombe ni barabara ambayo

inatumika kama barabara mbadala kipindi barabara ya kwenda Iringa ya lami inapokuwa ina hitilafu. Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba barabara hii inatengenezwa na inatumika kipindi chote cha mwaka? Ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. NDUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo yaliyoulizwa na Mheshimiwa Florent Kyombo kwa niaba yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii lakini fedha haitoshi. Kimsingi tunafahamu kwamba safari ni hatua, tunaanza na hatua moja tunakwenda na hatua nyingine, angalau Serikali imeanza kuweka fedha, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kutafuta fedha kukamilisha barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hii barabara nyingine ambayo inaunganisha maeneo haya muhimu ya Kata hizi mbili ya Kisanga na Uleling’ombe nayo iko kwenye mpango. Nimeeleza hapa na tutahakikisha kwamba tunaendelea kutafuta fedha kujenga barabara hizi kadri ya upatikanaji huo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kufuatia swali la msingi, Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Kilosa – Lumuma ambayo ni barabara muhimu kwa kuchukua vitunguu, iweze kupitika mwaka mzima bila ya matatizo?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ishengoma hiyo barabara iko chini ya *TARURA*, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali Mheshimwia Dkt. Christine Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya tathmini ya barabara muhimu zote katika halmashauri zetu zote kote nchini na tumewaelekeza mameneja wa TARURA katika wilaya hizo kuweka kipaumbele kwenye barabara zote muhimu kama ambayo hii ameitaja Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma. Kwa hiyo, nitoe maelekezo kwa meneja wa *TARURA* wa Wilaya hii ya Kilosa lakini pia wa Mkoa wa Morogoro kuhakikisha wanaipa kipaumbele barabara hii katika bajeti ili iweze kutimiza malengo ya kusafirisha bidhaa muhimu ambazo Mheshimiwa Mbunge amesema, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa barabara nyingi za ndani za *TARURA* ndani ya Jimbo la Kibamba zimeharibika sana na wananchi wanashindwa kufanya shughuli zao za maendeleo; je, ni upi mkakati wa Serikali kwenye kujenga barabara ya King'ong'o – Temboni - Saranga – Ukombozi - Goba – Majengo - Kwandogo – Kwashija na Luguluni – Mbokomu? Upi mkakatI wa Serikali wa kukamilisha barabara hizi?

**SPIKA:** Sasa hayo maneno yako ya hapo mwisho mimi mwenyewe sijayasikia, kwa hiyo, hata Naibu Waziri atakuwa hajayasikia. Lakini ulishauliza swali lako kwa hiyo hayo ya nyongeza hata hayahitajiki. Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtemvu, Mbunge wa Jimbo la Kibamba kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara nyingi za Jimbo la Kibamba zina hali mbaya na sisi kwenye bajeti ya *TARURA* ya mwaka ujao wa fedha tumeweka kipaumbele na bajeti imeongezeka sana ya Jimbo la Kibamba na namuelekeza pia Meneja wa Manispaa ya Ubungo kuhakikisha anazipa kipaumbele barabara za Jimbo la Kibamba ili ziweze kujengwa na kuhakikisha wananchi wanapata ahueni ya kupita katika barabara ambazo ziko bora, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pallangyo swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuunganisha kata zilizoko Mashariki na Kaskazini mwa Mlima Meru kwa kujenga barabara itakayounganisha barabara kuu ya Moshi na barabara kuu inayokwenda Namanga?

**SPIKA:** Hizo barabara zipo chini ya *TARURA*?

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hizi ambazo zinaunganisha Kata za Mashariki ya Meru na Moshi na maeneo mengine yote ni miongoni mwa barabara ambazo Serikali imeweka mpango, kwanza wa kuziainisha, kuzifanyia upembuzi yakinifu, lakini kutenga bajeti kwa ajili ya kuanza ujenzi wa ukamilishaji wa barabara hizo. Lakini jambo la msingi hapa Mheshimiwa Mbunge kushirikiana na Meneja wa *TARURA* katika Halmashauri hii ya Arusha wafanye tathmini ya barabara muhimu zaidi ambazo zinatakiwa kupewa kipaumbele ili Serikali itenge fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hizo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Swali langu ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga barabara kutoka Mji Mdogo wa Himo kupitia Sokoni kwenda Lotimu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, Mbunge wa Jimbo la Vunjo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii ya Mji Mdogo wa Himo ambayo inakwenda kuunganisha na miji mingine ni barabara muhimu na ni barabara ambayo tulishaelekeza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Kilimanjaro na Meneja wa *TARURA* wa Halmashauri ya Moshi kuhakikisha kwamba wanazifanyia tathmini na kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi ili Serikali itafute fedha kujenga barabara hizo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tuwahakikishie kwamba tutaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya barabara hizo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge ahsante sana.

Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Esther Edwin Malleko Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 308

**Msamaha wa Kodi ya Jengo kwa wale wanaostahili**

**MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza:-

Je, nini utaratibu wa Serikali kutoa msamaha wa kodi ya jengo kwa wale wanaostahili baada ya kodi kuhamishiwa kwenye za LUKU?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba majibu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutoa msamaha wa kodi ya majengo kwa wale wanaostahili unaendelea kutekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo Sura 289 ambapo mwenye jengo husika anatakiwa kuwasilisha maombi ya kupata msamaha wa kodi ya jengo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Baada ya *TRA* kujiridhisha kuwa muombaji anastahili msamaha kwa mujibu wa matakwa ya sheria, makato yake katika ununuzi wa umeme kupitia LUKU yatasitishwa. Aidha, kifungu cha 7(a) hadi (i) cha Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura

289, kimeainisha majengo yaliyosamehewa kulipa kodi ya majengo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutoa msamaha wa kodi ya majengo umeainishwa katika Kanuni za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Ukusanyaji wa Kodi ya Majengo, 2020 sehemu ya nne, Na. 16(1) hadi (6).

Mheshimiwa Spika, utozaji wa kodi ya majengo kupitia manunuzi ya umeme wa mfumo wa LUKU hauondoi haki ya msamaha wa kodi ya majengo kwa anayestahili kisheria bali umeongeza ufanisi katika kujiridhisha kuwa muombaji anastahili msamaha ili kuepuka kuwaondolea makato hata wanaostahili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Malleko swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER E. MALIEKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nina maswali mawili ya nyongeza; mwaka jana wakati wa Waziri wa Fedha akihitimisha hotuba ya bajeti ya mwaka 2021/2022 alisema kwamba wale wote ambao wana haki ya kupata msamaha huo watapata msamaha wa kodi hiyo, lakini mpaka sasa wanaendelea kutozwa.

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka *TRA* na *TANESCO* kuweza kubadilisha mifumo hiyo ili watu hawa waendelee kupata msamaha wa kodi hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha fedha hizo ambazo wamekuwa wakiwakata watu hawa ambao tayari walikuwa wamewaahidi kwamba fedha hizo hazitaendelea kukatwa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Esther Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Kilimanjaro, shemeji yangu huyu kwa kuwatetea sana Watanzania hasa wanyonge.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka wiki moja iliyopita alisimama kidete kuhusu ruzuku ya kahawa na Serikali tumechukua jambo hilo. Hata hili alilolileta, ni kweli tulipoanza tulianza tukiwa tuna ujaribisha mfumo huku tukiwa tunatekeleza sheria ya Bunge, kwa maana hiyo ni kweli kulitokea baadhi ya watu waliendelea kukatwa huku wakiwa wanastahili kusamehewa. Lakini tulirekebisha kwa kiwango kikubwa mifumo hiyo, kwa hiyo kama bado wapo ambao wamebakia wachache ambao wameendelea kukatwa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hilo tutalifanyia kazi na nielekeze Mamlaka ya Mapato kufanya haraka kumalizia wale ambao bado hawajanufaika na msamaha huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwaka wa fedha unakwenda kuanza tutafanyia kazi na hilo la kimfumo ili kuweza kufanya *sorting* zote ili tunapoanza mwaka mpya tuwe tumekamilisha jambo hilo kikamilifu, nakushukuru.

**SPIKA:** Swali lake la pili lilikuwa linataka kujua kama wale ambao sasa baada ya msamaha wameendelea kukatwa fedha, je, watarejeshewa zile fedha zao? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachelea kusema kiendacho kwa mganga hakirudi kwa sababu Kilimanjaro hata waganga walishakwisha, ninachoweza kusema tu ni kwamba kwa wale ambao kumbukumbu zao zinaonesha wamekatwa na walitakiwa wasilipe wawasiliane na Mamlaka ya Mapato kwa sababu kwenye kodi huwa kuna utaratibu wa kufanya *offsetting* kile ambacho ulishakilipa *in advance* ili kiweze kuwa *offsetted* wakati unalipa kinachofuata. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba mpaka wa Sirari ni mkubwa sana kutoka Sirari mpaka kule Nyanungu ambako ukimtaka mwananchi atoke aje apishe Sirari pale alipe kodi ya Serikali ni ngumu kidogo. Kwa nini kusiwe na kituo kidogo cha Forodha pale Witembe Itirio ili wananchi walipe mapato halali ya Serikali badala ya kufanya magendo kugombana na polisi? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango unao uhuru wa kulijibu hilo swali kama unayo majibu, kama huna hayo majibu yaje yatolewe likiwa swali la msingi.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nimpongeze babu yangu Mheshimiwa Mwita kwa kuleta swali hilo. Nilishapokea swali la aina hiyo pia kutoka kule Kakonko kwa ndugu yangu Aloyce, niunganishe tu kwamba baada ya Bunge wale Waheshimiwa Wabunge ambao kwenye maeneo

yao wangehitaji kuwa na mpaka mpya nizungukie mimi pamoja na Naibu wangu ama wataalam wetu ili tujiridhishe na zile sifa ambazo zinatakiwa kwa ajili ya kuanzisha mpaka mpya wa Tanzania na nchi jirani kwa upande wa ofisi ya Mamlaka ya Mapato ili tuweze kuwarahisishia wananchi wanapotaka kupata huduma ya Mamlaka ya Mapato.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda Mbunge wa Kigoma Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 309

**Kuendeleza Chuo cha Hali ya Hewa – Kigoma**

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukiendeleza Chuo cha Hali ya Hewa kilichopo Kigoma ili kiwe Chuo Kikuu kishiriki cha Dar es Salaam na kiweze kutoa taaluma nyingine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI, (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu

swali la Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania imeendelea na jitihada za kukiendeleza Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa kuwa Chuo Kikuu kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tayari andiko kwa maana ya dhana *concept note* kuhusiana na ushirikiano huo limeandaliwa na Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa *(NMTC)* na kuwasilishwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng’enda, swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, andiko la *TMA* kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni latokea mwaka jana mwaka wa 2021; na sasa tunakwenda kukaribia mwaka wa 2022. Nilitaka *commitment* ya Serikali kujua kwamba hatua hii inaweza ikakamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu, jambo hili litasaidia katika kuleta maendeleo ya wananchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mmejipangaje kuendelea na maboresho wakati mkisubiri maamuzi yale ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shabani Ng'enda, Mbunge Kigoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna ya kipekee kufuatilia Chuo hiki cha Hali ya Hewa pale Kigoma jimboni kwake.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza anasema maandiko yalianza tangu mwaka 2021; kimsingi maandiko tumeandika mwaka huu na tumepeleka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tarehe 14 Aprili, 2022 lakini mwaka jana tulianza mazungumzo na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hivi sasa tunavyosema tulitegemea Seneti itakapokaa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ndipo tupate mrejesho pengine ndani ya miezi miwili ijayo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili anataka afahamu tumejipangaje namna ya kuboresha chuo hiki. Ni kweli kwamba chuo hiki ni mkombozi mkubwa katika Mamlaka ya Hali ya Hewa na chuo ni kimoja na Serikali kupitia bajeti zake mwaka wa fedha 2021/2022 tulitenga kiasi shilingi milioni 450 na tumejenga majengo pale kwa maana ya madarasa, maabara pamoja na *computer room* ama *computer lab*. Lakini hata hivyo, mwaka wa fedha na Waheshimiwa Wabunge mlitupitishia hapa tumetenga kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kujenga jengo la utawala, na tunahakika mwakani chuo hiki kitaboresha zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar swali la nyongeza.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ninataka kujua ni mpango upi wa Serikali kuweka miundombinu shindani kwenye Chuo hiki cha Hali ya Hewa Kigoma; hasa ukizingatia kwamba chuo hiki kwa nchi za Afrika ni nchi chache sana ambazo zinatoa taaluma hii na sisi kuweza kulitumia hilo soko la kuweza kupokea wanafunzi kutoka nchi mbalimbali Afrika? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakar Hamad kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali tumejipanga vyema kukiboresha chuo hiki ili kiwe shindani katika nchi za Afrika Mashariki na Kati na ukizingatia kwamba hiki ni chuo pekee kinachotoa elimu hii ya hali ya hewa; na kwa msingi huo tumeingia makubaliano na Chuo cha Usafirishaji nchini *(NIT)* ili kianze kutoa elimu ya TEHAMA lakini zaidi ya yote kwa sababu pia Chuo chetu cha *NIT* kitaanza kutoa mafunzo ya urubani na mafunzo ya urubani yanaendana na hali ya hewa. Kwa hiyo, hata hiki pia kitakuwa sehemu ya hayo mafunzo; na zaidi ya yote pia chuo chetu tunakitangaza hata nchi jirani kwa maana ya Rwanda pamoja na Burundi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya wadau wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu Tanzania naomba swali lao namba 310 lipatiwe majibu ya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hanje hili ni swali lako, siyo swali lao, uliza swali lako tena.

Na. 310

**Mkakati wa Afrika wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STISA – 2024)**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza: -

Je, Serikali imetekeleza kwa kiwango gani Mkakati wa Afrika wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu *(STISA – 2024)* kufuatia maendeleo makubwa ya sayansi, teknolojia na ubunifu duniani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA,** alijibu:

Mheshimiwa Spika**,** ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianza kutekeleza Mkakati wa Afrika wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu uitwao *STISA*

*2024* mwaka 2015 kwa kuandaa mpango wa utekelezaji wa mkakati husika. Utekelezaji umejikita katika maeneo yafuatayo; eneo la kwanza ni kuweka mazingira wezeshi ya watafiti na wabunifu kwa ujumla kwa kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya utafiti na ubunifu kupitia Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia yaani MTUSATE; eneo la pili ni kuimarisha miundombinu ya utafiti na ubunifu kwa kuongeza idadi na kuwajengea uwezo watafiti na wabunifu kupitia miradi mbalimbali ikiwemo Mradi wa Vituo vya Umahiri yaani *ACE-II;* Mradi wa Kukuza na Kuendeleza Ujuzi *(ESPJ);* Mradi wa Afrika Mashariki wa Kuboresha Mafunzo ya Ufundi *(EASTRIP)* na Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Uchumi *(HEET)*; na eneo la tatu ni kuimarisha mahusiano kati ya Taasisi za ubunifu /utafiti na sekta za viwanda, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nusrat Hanje swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa tunafahamu wote kama Taifa hatuna Sera ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu lakini pia Sheria ya Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* imepitwa na wakati.

Je, Maonesho ya kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu MAKISATU yanatekelezwa kwa sera ipi?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Habari, Mawasiliano ya Habari na Teknolojia ya Habari yote yana masuala ya teknolojia jambo ambalo linasababisha tushindwe kuelewa nani hasa mhusika wa masuala ya teknolojia kwenye Taifa letu. Je, Wizara ipo tayari sasa kuanza kuishauri Serikali kwa vielelezo hatua kwa hatua

waanzishe Wizara mpya ambayo itashughulika na masuala ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu; ukizingatia mabadiliko ya sayansi na teknolojia ulimwenguzi lakini mapinduzi ya nne ya viwanda kama ilivyo nchi za Kenya, Afrika Kusini na Rwanda? *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali ni mawili Mheshimiwa, maswali ya nyongeza ni mawili. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Kipanga majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Nusrat kwa ufuatiliaji wake wa karibu wa masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu, lakini kipekee nichukue fursa hii kuwapongeza Wabunge wote ambao waliweza kufika na kutembelea kwenye mashindo yetu ya MAKISATU ambayo yalianza tarehe 16 – 20 Mei, 2022 katika Uwanja wetu wa Jamhuri pale Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba nimtuoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba dhana hii ya utekelezaji wa mashindano hayo ya MAKISATU ni msimamo au ufuatiliaji wa karibu wa Serikali kuhakikisha kwamba mashindano haya au ubunifu nchini unaweza kuimarishwa.

Mashindano haya yanatekelezwa kwa mujibu wa sera ya ubunifu ya mwaka 1996. Tunakiri kuna mapungufu machache kwenye sera hii, lakini ndio ambayo tunazingatia katika utekelezaji wa mashindano haya.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyozungumza katika kipindi kilichopita kwamba, sera hii tunakwenda kuifanyia maboresho makubwa, lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kupitia mashindano haya tumeweza kuibua bunifu zaidi ya 1,785, lakini vilevile zaidi ya bunifu 200 zimeweza kuendelezwa na zaidi ya bunifu 26 zimeweza kuingia sokoni kuona namna gani Serikali inasimamia kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini katika swali lake la pili anazungumzia suala la Wizara ya Elimu pamoja na Wizara ya Habari kuwa na suala hili la teknolojia.  Ni kweli, tunaomba tukiri kwamba, Wizara ya Habari na Wizara ya Elimu zote zina teknolojia ndani, lakini utekelezaji wa teknolojia hii unategemea na mawanda yale ambayo Wizara imepewa kupitia hati idhini ya uanzishwaji wa Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, kwa vile ametoa ushauri namna gani sasa Serikali inaweza kutenganisha maeneo haya ya ubunifu na Wizara hizi; basi tubebe ushauri huo, twende tukaufanyie tathmini na tuweze kuufanyia kazi ili tuweze kuona namna gani tunaweza tukatekeleza.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu mahususi hayo na niseme umeyajibu kwa ufasaha sana, isipokuwa teknolojia inayoshughulikiwa na Wizara ile nyingine ambayo sio ya kwenu, Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ile nyingine inaitwa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, sio teknolojia zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Ugunduzi na ubunifu ni miongoni mwa nyanja muhimu sana katika ukuzaji uchumi na maendeleo. Nini mkakati wa Serikali katika kuendeleza ugunduzi na ubunifu katika nyanja za vijijini na hasa kwa wanawake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Toufiq, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika majibu yangu ya msingi kwamba, kwanza tuna sera ya namna gani ubunifu na ugunduzi unasimamiwa au unaratibiwa katika maeneo yote. Katika kulisimamia hilo, Serikali baada ya kuona hii sera mwaka 2018 tumeandaa mwongozo wa namna gani masuala haya ya ubunifu yanaweza kusimamiwa na kuratibiwa kuanzia ngazi ya vijiji, kata, Tarafa, Wilaya, mpaka kufika katika ngazi ya Taifa ambako huko watu wote tunaweza tukawakuta.

Mheshimiwa Spika, ukitaka kuangalia kwa umakini kabisa katika mashindano yetu haya ya MAKISATU yameweza kubeba makundi yote, kuna makundi karibu saba tumeweza kuyazingatia tunapokwenda kuwagundua wagunduzi wetu au watafiti wetu katika maeneo yote ya vijijini mpaka katika ngazi ya Taifa. Kwa hiyo, katika eneo hili na wanawake vilevile wanaingia kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa. Je, Serikali ina mkakati gani kusaidia wabunifu kuhatamia teknolojia zao au ku-*incubate* wakati wakijiandaa kuanzisha viwanda vidogo vidogo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya…

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia…

**SPIKA:** Ngoja, subiri Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa kaka yangu, Profesa Ndakidemi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimejibu katika majibu yangu ya nyongeza kwenye maswali yaliyopita kwamba, katika kipindi cha miaka minne iliyopita Serikali ilianzisha mashindano ya MAKISATU ambayo tulianza mwaka 2019 na mwaka huu sasa ni awamu ya nne. Katika mashindano haya zaidi ya bunifu elfu moja mia saba na themanini na kitu yaliweza kuibuliwa na zaidi ya bunifu 200 zimeweza kuendelezwa au kuatamiwa na zaidi ya bunifu 26 tayari zimeshapelekwa sokoni, sasa kitu gani tunachofanya?

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwapata hawa wagunduzi au wabunifu tunawapeleka kwenye zile *hub* zetu, tuna *center* mbalimbali nchini kote ambazo zinawalea na Serikali sisi tumeweza kupeleka fedha katika maeneo haya. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tumeweza kupandisha bajeti ya kuwalea hawa wabunifu wetu kutoka bilioni 3.0 mpaka bilioni 9.0 katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali tayari imeshafanya eneo leke na katika kipindi hiki hizi bunifu tulizozipata katika mashindano haya yaliyopita, zaidi ya milioni 700 tumeshazipeleka tayari kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, hawa tunakwenda kuwaendeleza ili bunifu hizi ziende kuwa biashara na bidhaa ambayo tunaweza tukaipeleka sokoni.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa David Makiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 311

**Hitaji la huduma ya mawasiliano ya simu Kata za Mufindi Kusini**

**MHE. DAVID M. KIHENZILE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga miundombinu ya mawasiliano katika Kata za Idete, Kiyowela, Maduma, Idunda, Makungu na Ihowanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile Mbunge wa Mufindi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* inatekeleza miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano katika Kata za Idunda na Ihowanza, Wilayani Mufindi ambapo ujenzi wa minara unaendelea na utakamilika ifikapo Julai, 2022. Mwaka wa fedha wa 2022/2023, Serikali itafikisha huduma za mawasiliano ya simu katika Kata za Idete na Maduma. Aidha, Kata za Kiyowela na Makungu zitafanyiwa tathmini ya kiufundi kubaini changamoto halisi iliyopo ili kutatuliwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Kihenzile, swali la nyongeza.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Niishukuru kwanza Wizara kwa kazi kubwa sana ambayo wameifanya, wamekwishaanza. Maswali yangu mawili ya nyongeza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza; kwenye Kata ya Kasanga ndiyo Makao Makuu ya Tarafa yetu na ndipo kilipo kituo cha afya ambapo wanatibiwa wananchi wengi, hakuna mawasiliano. Je, Serikali ina mkakati gani kuweza kusaidia wananchi wetu ili hata mtu akiwa hospitali aweze kuwasiliana na ndugu zake?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni upi mkakati wa Serikali ili kupunguza *multiplicity* ya minara kila sehemu? Kwamba, tuwe na mnara mmoja pengine na *networks* nyingine waweze ku-*hire* pale, ni upi mkakati wa Serikali katika jambo hili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwakiposa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, tunapokea ombi la Kata ya Kasanga ambayo, kama alivyoeleza mahitaji yake ni makubwa na kwa sababu ya huduma ambazo ziko pale. Nimuahidi kwamba, kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote tunazo kata na tunayo maeneo ambayo tutayapelekea huduma maalum. Nalichukua hili eneo na tutawaagiza watu wa *UCSAF* kwenda kufanya tathmini na kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, tutajenga mnara kwenye eneo husika.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Ni kweli kwamba, si jambo zuri kuwa na minara mingi katika mazingira tuliyonayo. Sisi Serikali kupitia Sheria ya *EPOCA* tunawahamasisha na kuwashawishi watoa huduma

wachangie minara badala ya kila mtoa huduma kuwa na mnara wake. Changamoto iliyopo ni kwamba, baadhi ya maeneo na hasa ya vijijini ambayo watumiaji wa mtandao ni wachache, kiuchumi kuna changamoto ya ku-*share* mnara badala yake wana-*opt* kuachiana maeneo ili watoe huduma wasigawane wale watumia huduma wachache.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali tuko katika mchakato wa kuliwezesha Shirika letu la Mawasiliano - *TTCL* kumiliki minara na kwa sababu ni shirika la Serikali ni rahisi kuwabana wakawavutia wawekezaji watoa huduma wengine wakapanga kwenye minara ya *TTCL* badala ya ile ambayo inaendeshwa na watoa huduma ambayo kwa kweli, inaendeshwa kibiashara na inakuwa ngumu kwa maeneo ya vijijini ku-*share* kwa sababu ya gharama za uendeshaji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas William Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Jimbo la Mbinga Mjini, Kata ya Kitanda, Kikolo na Kagugu hakuna miundombinu ya mawasiliano. Je, lini Serikali itajenga miundombinu ya mawasiliano ili kuwarahisishia wananchi kupata mawasiliano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mbunge wa Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo aliyoyataja naamini yako kwenye orodha ya kata ambazo mwaka ujao wa fedha tunapeleka minara ya simu, lakini kama kata zote hazikuingia kama nilivyosema, baadhi ya hizo kata zitakuwa zimeingia, zilizobaki tuko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kufanya tathmini ya mahitaji yaliyopo, tuangalie uwezo wa bajeti yetu hasa kwenye maeneo yale ambayo yanahitaji huduma maalum na tutafikiria kuona namna ya kupeleka huduma kwenye maeneo aliyoyataja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya swali la nyongeza. Awali ya yote niishukuru Wizara hii kwa kuwezesha mawasiliano katika Kata ya Likawage, Jimbo la Kilwa Kusini. Swali langu, ni nini mpango wa Serikali kupitia Wizara hii kuhakikisha kwamba, Kata za Nanjilinji, Kikole pamoja na Limalyao na zenyewe zinapata mawasiliano ya uhakika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kata alizozitaja na ni kweli katika Wilaya na majimbo ambayo hali yake ya mawasiliano ni ngumu ni pamoja na Jimbo la Kilwa Kusini. Baadhi ya minara ambayo imejengwa ipo, lakini haijakamilika, ikikamilika itapunguza tatizo tulilonalo, lakini bila shaka Mheshimiwa Mbunge atakumbuka kwenye bajeti ya

mwaka huu tumeweka zaidi ya minara mipya 700 nchi nzima, kwa hiyo, naamini kwamba, baadhi ya kata zake zitakuwemo. Kata zitakazobaki, nimhakikishie kwamba, tutakwenda kuzimalizia kwa ule utaratibu wa maeneo maalum.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Vijiji vya Upendo, Kijiji cha Shoga pamoja na Sipa vina changamoto kubwa sana ya mawasiliano. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba, vijiji hivi vinaweza kupata mawasiliano katika mwaka wa fedha unaokuja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kasaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye majibu niliyoanza nayo mwanzo, mwaka huu wa fedha tumetenga minara mingi kidogo, lakini kwa maana ya eneo maalum analotoka Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ya shughuli za kiuchumi zilizopo kwenye eneo hili tunazipa kipaumbele cha pekee. Kama katika orodha yetu tuliyoitoa wakati wa bajeti hizi kata na maeneo aliyoyataja hayamo, basi na yenyewe tutayaingiza kwenye orodha ya yale maeneo maalum, kwa sababu ya shughuli nyingi za kiuchumi ambazo zinafanyika kwenye eneo lake na sisi tuko tayari kushirikiana kusaidia

katika ujenzi wa uchumi wa kidigitali, kwa maana ya kwamba, ule uchumi unaofanyika kwenye eneo lake uingie katika mfumo wa jumla wa uchumi wa kidigitali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, sasa aulize swali lake.

Na. 312

**Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga**

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA** aliuliza:-

Je, ni lini Wananchi wa Kata ya Bosha na Mhinduro watapata maji salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Jimbo la Mkinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha usanifu wa Mradi wa Maji wa Mhinduro utakaohudumia Kata za Bosha na Mhinduro na ujenzi utaanza mwezi Juni, 2022 na kukamilika katika mwaka wa fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dunstan Kitandula, swali la nyongeza.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pia naishukuru Serikali kwa majibu, naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza. Taarifa nilizonazo ni kwamba, mpaka sasa mkataba wa mradi huu haujasainiwa na kwa muda uliobaki Waziri anatuhakikishia kwamba, tutaweza kusaini mkataba huo na ujenzi wa mradi huu uweze kuanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dunstan Kitandula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ndio. Wizara tutaweza kusaini mkataba na kazi zitaanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa muda mrefu sana Serikali iliahidi kupeleka maji katika Shule ya Nanja, Kijiji cha Mti Mmoja na Lepurko vilivyoko katika Wilaya ya Monduli, Mkoa wa Arusha, lakini hadi leo haijatimiza ahadi yake. Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi yake katika vijiji hivi, ili wanafunzi hawa na wananchi waepukane na adha hii kubwa ya maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuliahidi eneo la shule hii pamoja na hiki kijiji alichokitaja viweze kupatiwa huduma ya maji. Hatujapeleka kwa sababu ya mtawanyiko wa majukumu, lakini ni lazima tutapeleka maji katika shule hii na hiki kijiji na maeneo ya shule nyingine zote katika Jiji la Arusha, lakini vilevile na vijiji vyote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Licha ya juhudi kubwa za Serikali za kutatua changamoto ya maji Mkoani Tanga, bado Wilaya ya Muheza inapata maji kwa mgawo tena saa 8.00 za usiku. Je, ni lini Serikali itawezesha maji yale kutoka mapema ili wanawake wa Muheza waweze kupumzika usiku?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Tanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la Muheza kutoa maji ya mgawo usiku wa manane, huu sio utaratibu mzuri na tunataka kukomesha hili. Naomba wananchi wawe watulivu na subira, tutahakikisha huduma ya maji inapatikana saa zote na kama ni saa chache basi muda rafiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, swali la nyongeza.

**MHE. LIVINGSTONE N. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakabidhi Mradi ulioko katika Kata ya Vuje, Wilaya ya Same, ambao ulianza tangu 2018 ambao uligharimu takribani Sh.1,300,000,000?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi ikishakamilika ni wajibu wa Wizara kukabidhi kwa wananchi na unaendeshwa na vile vikundi vidogo vidogo ambavyo vinaundwa na wananchi. Kwa hiyo na mradi huu ambao umeshatumia fedha ya Serikali zaidi ya bilioni ni lazima nao uje ukabidhiwe kwa wananchi, ili lengo la kufikisha huduma ya maji kwa wananchi liweze kutimia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Je, ni lini mkandarasi wa kujenga Mradi wa *Ngana Group* atapatikana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Mlaghila, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *Ngana Group* taratibu ziko mwishoni. Tunatarajia kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha, mkandarasi atapatikana na kazi ziweze kuendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, sasa aulize swali lake.

Na. 313

**Umuhimu wa kuyatangaza Maporomoko ya Kalambo**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha Maporomoko ya Kalambo yanatangazwa ili yawe na mchango wa kiuchumi kwa Taifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege Mbunge wa Jimbo la Kalambo kama ifuatavyo:-

Katika kuhakikisha maporomoko ya Kalambo yanatangazwa kikamilifu, hatua zifuatazo zimeanza kuchukuliwa. Hatua ya kwanza ni kutumia vyombo vya

habari kuandaa machapisho na majarida kushiriki katika maonyesho matamasha matukio na makongamano ya utalii na biashara yanayofanyika ndani na nje ya nchi. Aidha, jumla ya watalii 2,365 walitembelea maporomoko hayo mwaka 2021 ikilinganishwa na watalii 300 kwa mwaka 2016 na kuweka mabango katika viwanja vya ndege ikiwemo Uwanja wa Ndege wa Songwe na maeneo mengine katika Mkoa wa Rukwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kandege swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, maporomoko ya Kalambo ni miongoni mwa vivutio vilivyo Kusini Nyanda za Juu na ni ukweli usiopingika kwamba maporomoko haya kuachiwa chini ya *TFS* ambayo siyo kazi yake ya kutangaza vivutio vya kitalii ni kukosesha Taifa hili mapato sahihi.

Je, Serikali iko tayari kuyaondoa maporomoko haya kuwa chini ya umiliki wa *TFS* na kupeleka katika taasisi ambayo kazi yake mahsusi ni kwa ajili ya kutangaza vivutio vya utalii?

Swali la pili, kwa sababu kutangaza ni pamoja na uwepo wa bajeti na Wizara bado haijaleta bajeti yake. Je, watatuhakikishia kwamba kama maporomoko haya yataendelea kuwa chini ya *TFS* bajeti yake itaonekana ambayo iko mahsusi kwa ajili ya kutangaza vivutio vya utalii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Kandege hilo swali lako la pili utakuwa unamuweka Mheshimiwa Naibu Waziri mazingira

magumu kidogo, kwa sababu bajeti yake kama ulivyosema haijasomwa hapa kwa hivyo atajibu swali lako la kwanza halafu hilo lingine utasubiri bajeti yake isomwe hapa. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kandege, Mbunge wa Kalambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kuyapeleka haya maporomoko haya maporomoko katika taasisi ya TFS tuliona kuna mbinu nyingine ambazo zinahitaji kusimamiwa na taasisi hii ya huduma za misitu Tanzania. Kwanza, kuna misitu ndani yake lakini pia kuna uoto wa asili ambao ndani yake unatunza vyanzo vya maji, hivyo *TFS* ni sahihi kabisa kusimamia maporomoko haya.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii zote zinatangaza masuala ya utalii. Tumeanza kujenga miundombinu ya barabara katika eneo hilo, pia tumetengeneza ngazi za kufika chini, tunatarajia pia kuanzisha masuala ya *cable car* katika maporomoko hayo ambayo tunatarajia kwamba tutapata watalii wengi sana ambao watakuwa wanatoka nchi jirani na ndani ya nchi.

Sambamba na hilo, tunajenga daraja ambalo litaunganisha Zambia na Tanzania, hii yote ni mikakati ambayo imepangwa ndani ya bajeti ya *TFS*. Kwa hiyo nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaenda kufanya mambo mazuri na Kalambo inaenda kufunguka. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, bado swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 314

**Tembo kuvamia mashamba na kujeruhi –Tunduru**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Je, kuna mango gani wa kudhibiti Tembo wanaoharibu mazao na kujeruhi wananchi Kata za Mindu, Kahulu na Tinginya -Tunduru.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Vijiji vingi katika Wilaya ya Tunduru vinapakana na Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na ushoroba wa wanyamapori wa Selous Niassa ambao ni mapito ya wanyamapori kati ya Tanzania na Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, Wizara imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuomba kibali cha kuajiri Askari wapya 600 ambao watasambazwa kwenye maeneo hatarishi ili kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu. Sambamba na hilo, Wizara ina mkakati wa kuanzisha vituo vya kikanda vya

Askari katika maeneo yenye changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu;

(ii) Kutoa mafunzo kwa askari wa wanyamapori wa vijiji; na

(iii) Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna bora ya kupunguza athari zinazotokana na wanyamapori wakali na waharibifu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jaqueline Ngonyani swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa niulize swali moja dogo la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Je ni lini Serikali itaongeza fidia kwenye mazao ambayo yanaharibiwa na Tembo katika maeneo husika, itaongeza hiyo fidia kwa maana ya kwamba Serikali mpaka sasa hivi inatoa fidia ya Shilingi 100,000 kwa heka wakati kila kitu kimepanda bei, hata uzalishaji umepanda bei.

Kwa hiyo ni lini Serikali itaongeza kiwango cha fidia kwa hekari moja inayoharibiwa na tembo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, swali la pili samahani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jaqueline ulishakaa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Nilitaka kukaa lakini nilikuwa sijafika chini *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa, sasa kwa umbali huu mimi nitajuaje umefika chini ama hujafika Mheshimiwa Jacqueline? Haya uliza swali lako.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wananchi wanaoishi katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Tunduru na Namtumbo wamekumbwa na taharuki kubwa sana wakati wote wa maisha yao kuhusiana na hali halisi ya wingi wa tembo na uharibifu mkubwa unaofanyika, tembo wamefikia hatua ya kufika mpaka majumbani.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwavuna hawa tembo ili waweze kupungua na adha inayowakuta wananchi hawa ipungue? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jacqueline Msongozi Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la fidia Mheshimiwa Mbunge nimtoe wasiwasi na Wabunge wengine wote. Jana tulikuwa na semina tuliweza kuliongelea hili suala, tulichofanya sisi kama Serikali tumekubaliana na mawazo ya Waheshimiwa Wabunge kwamba tunayachukua kwa umoja wao, tunaenda kuangalia sheria ambayo ilipitisha mwanzo kiwango hicho tuifanyie *review* kisha tutaleta humu humu Bungeni tuone namna iliyobora ya kuangalia thamani ya hawa wananchi ambao wanapata hasara ya kupoteza mazao na wengine wanapoteza hadi

maisha ili angalau hii fidia au kifuta machozi na jasho kiweze kukidhi haja ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la kuhusu taharuki ya tembo, ni kweli hii ni changamoto kubwa na tunawapa pole sana wananchi ambao wamekuwa wakikumbana na changamoto hii ya wanyama wakali hususan tembo. Serikali ina mkakati mahsusi wa kuhakikisha kwamba tunaanzisha vituo viwe karibu sana na maeneo yaliyohifadhiwa ili angalau taharuki hii inapojitokeza basi Askari wawe karibu kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo tumeendelea kutoa elimu kwa wananchi ili tuwe na ushirikishwaji wa karibu na jamii ili kudhibiti hawa wanyama wakali na waharibifu. Ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge Wizara ya Afya, Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay Mbunge wa Mbulu Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 315

**Hitaji la majokofu ya kuhifadhia maiti nchini**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itahakikisha kuwa Vyumba vya kuhifadhi maiti nchini vinakuwa na majokofu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zakharia Paulo Issaay Mbunge wa Mbulu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hospitali zote 28 za Rufaa za Mikoa zina majokofu ya kuhifadhia maiti. Pia hospitali 16 za Mikoa zimepewa majokofu mapya kati ya hospitali 28 za Rufaa za Mikoa. Aidha, Serikali inatambua kuwa tatizo kubwa la upungufu lipo kwenye hospitali za Wilaya na vituo vya Afya vipya. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imepanga kununua majokofu 103 kwa ajili ya kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza swali hili lilikuwa limeulizwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu niliuliza mimi mwenyewe na ninakushukuru kiti chako kuamua Wizara ijibu na leo amekuja kuleta majibu.

Nina maswali madogo mawili ya nyongeza, swali la kwanza, kwa kuwa sasa Halmashauri ya Mji wa Mbulu haina jokofu kwa muda wa mwaka mmoja au zaidi ya mwaka sasa, na kwa mapato yetu ya ndani hatuwezi kununua jokofu hilo linalohitaji takriban Milioni 70.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutununulia hilo jokofu ili hospitali ya Mbulu ipate huduma hiyo na kuondoa adha hiyo kwa wananchi?

Swali la pili, kwa kuwa kumeonekana kuna gharama kubwa sana ya uagizaji wa dawa na vifaatiba nchini

kupitia Wakala wa *MSD* Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kutazama gharama hizo ili kuona namna mbadala ya kupunguza gharama kwa Serikali na kutoa huduma hiyo kwa umma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kwanza ninampongeza kwa ufuatiliaji wake makini wa hili suala kwa ajili ya Wilaya yake. Kwanza ameshafika Wizarani na nimhakikishie kwamba majokofu yameshafika *MSD* siku tatu zilizopita, kwa hiyo mpaka mwisho wa wiki itakuwa jokofu la kubeba miili 12 litakuwa limefika Kanda ya Kaskazini kwa ajili ya kuelekea kwenye hospitali yake ya Wilaya.

Swali lake la pili ni suala la gharama ya bei ya *MSD* kuwa ni ghali. Kwanza nimwambie *MSD* ni Shirika la Serikali na kweli huko nyuma kulikuwa na tatizo hilo lakini halipo sasa hivi, ndiyo maana Rais wetu Samia Suluhu Hassan ametoa fedha na tumejenga viwanda kule Idofi ambavyo vinazalisha dawa pamoja na *gloves* ukienda sasa hivi *MSD* ukilinganisha na bei zilizopo mtaani, *MSD* ni bei rahisi kuliko ilivyo mtaani. Kwa hiyo, hilo tatizo limesha tatuliwa na linaendelea kufanyiwa kazi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako niseme tu moja kwenye eneo hili la *mortuary,* Mbunge wa Meru amejenga yeye mwenyewe *mortuary* kwa asilimia 80 kwa fedha zake na niipongeze Halmashauri yake ikachangia asilimia 20 iliyobaki na katika majokofu yanayokuja, jokofu lako linakuja na Mbunge wa Makete.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka Serikalini, nawasubiri Wabunge wakae waliosimama, ahsante sana.

Tutaanza na tangazo la wageni walioko Bungeni siku ya leo, kama nilivyowatangazia utaratibu wetu wa kutangaza wageni matangazo yetu yatakuwa kwa kifupi, kwa hiyo kwa ujumla wageni wote tunawakaribisha sana hapa Bungeni kuja kutazama Wabunge wenu na Wawakilishi wenu namna wanavyofanyakazi karibuni sana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Wageni watakaotangazwa siku ya leo ni wageni 63 wa Mheshimiwa January Makamba ambaye ni Waziri wa Nishati na hawa ni Viongozi na Watendaji wa Wizara, Taasisi na Mashirika yanayosimamiwa na Wizara hiyo pamoja na washirika wa maendeleo wadau wa sekta ya nishati na Wakandarasi. Sasa hawa nitawatangaza kwa makundi hawa wote wameongozwa na Mhandisi Felchesmi Mramba ambaye ni Katibu Mkuu, karibu sana. Yupo pia Ndugu Heri Mahimbali ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, karibu sana.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kama nilivyosema ameongozana na watu wengi kwanza tuanze na Viongozi na Watendaji wa Wizara wasimame kwa pamoja karibuni sana Bungeni. Pia zipo Taasisi na Mashirika yanayosimamiwa na Wizara hii haya karibuni sana. Wapo pia washirika wa maendeleo karibuni sana.

Wapo pia wadau wa sekta ya nishati na Wakandarasi hawa wasimame pamoja, wadau wa sekta ya nishati na Wakandarasi karibuni sana na tunafurahi kwamba tulipata nafasi wakati mkiwa kwenye maonesho hapa ya kuwaona na kuzungumza nanyi karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wenu ambao wametembelea Bunge hili kwa mialiko yenu na wengine wamekuja wao wenyewe, lakini wapo wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge waliotembelea Bunge na wao wasimame wote kwa pamoja, wageni wa Waheshimiwa Wabunge karibuni sana, Wabunge wenu wanafanyakazi nzuri sana ya kuwawakilisha hapa Bungeni. *(Makofi)*

Tunao pia wageni walioembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo wapo wanafunzi 47 na walimu watano kutoka shule ya *The Voice* iliyopo *Usa River* Jijini Arusha karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa na hilo tangazo la wageni lakini jambo moja tu la kuwakumbusha Waheshimiwa Naibu Mawaziri wanapoamua nirejee tena, unapoamua kusifia Wabunge wasifie wote watakaokuuliza maswali siku hiyo. Ukiamua wewe kwamba leo nimeamua muda wangu sehemu yake nitatumia kusifia Wabunge wakaokuuliza maswali, usichague Mbunge wa kumsifia na mwingine ukamuacha. Pia tukumbuke tu kwamba hizo pongezi zinachukua muda na tunataka tuchukue muda mrefu zaidi Wabunge kupata fursa ya kusema changamoto zilizoko Majimboni kwao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba iliyopo mbele yetu, Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii sasa kumuita Waziri wa Nishati Mheshimiwa January Yusuf Makamba aje awasilishe hoja ya Wizara yake ya Nishati.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2021/2022 na kupitisha Makadirio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na fursa ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Nishati kwa mwaka ujao wa fedha. Tungependa taarifa tuliyoiweka mezani ndiyo iingie kama Kumbukumbu ya Bunge na hapa nitasoma muhtasari.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa na kuteuliwa katika kipindi hiki cha mwaka huu wa fedha pia natoa pole kwako na kwa Bunge lako Tukufu kwa

kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Elias John Kwandikwa aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Mheshimiwa William Tate Ole Nasha aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa Irene Alex Ndyamukama aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini katika nafasi hii, nampongeza kwa kuiongoza nchi yetu vizuri ambapo kuna amani, utulivu, maelewano na maendeleo yanaonekana. Nampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais naye kwa kuniongoza na kunielekeza pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusimamia utekelezaji wa kazi zetu.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya hotuba ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka ujao wa fedha. Hotuba hii ina sehemu kubwa mbili; sehemu ya kwanza ni taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Nishati kwa mwaka unaoisha wa fedha na sehemu ya pili ni Mpango wa Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka unaoisha wa fedha; bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2021/2022 ilikuwa ni shilingi trilioni 2.386

ambapo shilingi trilioni 2.359 sawa na asilimia 88.89 zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 27.22 sawa na asilimia 1.11 zilikuwa ni kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia mwezi Mei, 2022 Wizara ilikuwa ilipokea jumla ya shilingi trilioni 1.820, sawa na asilimia 76.29 ambapo shilingi trilioni 1.797 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 22.83 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka huu unaoisha pamoja na mambo mengine, uliongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Sera, Mikakati na Programu mbalimbali za Kisekta na Kitaifa pamoja na Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu *(SDGs 2030)* kuhusu upatikanaji wa nishati.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha, ikiambatana na vielelezo na takwimu mbalimbali inapatikana katika sehemu (b) ya hotuba yangu, kuanzia ukurasa wa pili hadi ukurasa wa 38.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu hiyo tumeripoti kazi zilizofanyika katika mwaka unaokwisha katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika kwanza miradi ya uzalishaji, usambazaji na usafirishaji wa umeme; pili tumeripoti kuhusu usambazaji wa umeme vijijini; tatu tuliripoti kuhusu uendelezaji wa rasilimali ya jotoardhi; nne tuliripoti kuhusu utafutaji wa mafuta na gesi katika vitalu vya kimkakati; pia tuliripoti kuhusu mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia *(LNG);* pia ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji na

usambazaji wa gesi asilia; saba, uagizaji na upatikanaji wa bidhaa za mafuta na petroli nchini; na nane udhibiti wa masuala ya nishati kupitia *EWURA*.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, taarifa ya kina ya masuala yote haya, ikiwemo vielelezo na viambatishi inaweza kupatikana na kusomwa kwa kirefu katika hotuba kamili ya bajeti yetu kuanzia ukurasa wa pili hadi ukurasa wa 38.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana mwaka huu unaoisha wa fedha kulijitokeza changamoto mbalimbali ambazo tulizielezea katika sehemu ya (c) ya hotuba yangu, ukurasa 38 hadi ukurasa wa 40 ambapo pia tumeelezea hatua mbalimbali tulizochukua kukabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijikite katika kuelezea mpango wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha unaokuja. Katika kutekeleza mpango wa bajeti wa Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha ujao, Wizara itaongozwa na vipaumbele 12 vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, cha kwanza ni kutekeleza miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ikiwemo kufikisha Gridi ya Taifa katika Mikoa ya Kigoma, Katavi na Kagera pamoja na mradi mkubwa wa Kuimarisha Gridi ya Taifa yaani *National Grid Stabilization Project*.

Kipaumbele cha pili ni kutekeleza miradi ya kupeleka Nishati Vijijini pamoja na kuanza utaratibu wa kupeleka umeme katika vitongoji vyote nchini.

Tatu, kukamilisha mazungumzo ya mradi wa kusindika na kuchakata gesi wa *LNG* kule Lindi na kuanza taratibu za utekelezaji wake; nne kutekeleza miradi ya nishati jadidifu ikiwemo jotoardhi, jua, upepo, tungamotaka, na matumizi bora ya nishati yaani *Energy Efficiency and Conservation*.

Tano kuhakikisha kwamba upatikanaji wa mafuta ya kutosha nchini, ikiwemo uanzishwaji wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta yaani *Strategic Petroleum Reserve* pamoja na Mfuko wa Kudhibiti Mabadiliko ya Bei za Mafuta *Fuel Price Stabilization Fund*.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha sita ni kuiimarisha *TPDC* na Kampuni zake tanzu yaani *TANOIL* na *GASCO;* saba ni kuboresha miundombinu ya kupokea, kushusha, kuhifadhi na kutoa mafuta katika Bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga pamoja na kuanzisha Ghala ya Dhamana ya Forodha yaani *Customs Bonded Warehouse* na Kituo cha Pamoja cha Kupokelea Mafuta kutoka Melini yaani *Single Receiving Terminal*.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha nane ni kuimarisha utendaji wa kazi na huduma zinazotolewa na taasisi zinazosimamiwa na Wizara ikiwemo *REA*, *TANESCO, EWURA PBPA* na taasisi nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha tisa ni kuongeza ushiriki na uwekezaji wa Sekta Binafsi katika sekta ya nishati; kumi ni Kuhakikisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia unaimarika; kumi na moja, kufufua shughuli za utafiti na utafutaji wa mafuta na gesi asilia nchini na  kumi na mbili ni kuongeza matumizi ya nishati ya kupikia hasa *LPG* majumbani na kwenye magari na viwandani nishati ya *CNG*.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Wizara katika mwaka ujao wa fedha pamoja na mambo mengine vimejikita katika kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020, Maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa aliyoyatoa kwa Wizara kwa nyakati tofauti ikiwa ni pamoja alipolihutubia Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021 lakini vilevile pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu *(SDGs 2030)* kuhusu nishati.

Mheshimiwa Spika, sekta ya nishati ni moja ya mihimili muhimu ya uchumi wa nchi na ustawi wa watu wake. Bila umeme wa uhakika na mafuta ya uhakika na ya kutosheleza, shughuli za uzalishaji mali zinazorota na uchumi unadumaa. Kwa kutambua haya Serikali katika mwaka ujao wa fedha imeweka vipaumbele vitakavyohakikisha kwamba sekta ya nishati inauhudumia uchumi wa nchi yetu na maendeleo ya nchi ipasavyo. Miradi yote na mipango na mikakati tutakayo ielezea hapa siku ya leo inatupeleka kwenye safari ya uchumi imara unaowanufaisha Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza dira hiyo na vipaumbele nilivyovitaja napenda sasa kufafanua miradi mbalimbali pamoja na majukumu mengine yaliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka ujao wa fedha kwa kila sekta ndogo ya Wizara.

Kwanza ni mradi wetu mkubwa wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere kule Rufiji; pamoja na kazi nyingine za kiufundi zilizopangwa kufanywa katika mwaka ujao wa fedha Serikali itaongeza umahiri na weledi kwenye usimamizi wa mradi ili kuhakikisha kwamba unamalizika

ukiwa katika usalama na viwango stahiki na malengo yake yanatimia kwa kazi hiyo jumla ya shilingi trilioni 1.44 zimepangwa katika kutekeleza mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ni wa kuzalisha umeme kwa gesi asilia pale *Kinyerezi I Extension* mradi huu utagharimu dola za Kimarekani milioni 188 hadi kukamilika kwake. Katika mwaka ujao wa fedha tumetenga shilingi bilioni 35 kwa ajili ya kazi za kukamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ni wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji kule Rusumo wa megawati 80, mradi huu ni wa nchi tatu, na utaongeza uzalishaji wa umeme kwa megawati 27. Tutakamilisha mradi huu katika mwaka ujao wa fedha ambapo tumetenga shilingi bilioni 9.94 kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia ipo miradi iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa kwanza ni mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji wa Ruhudji wa megawati 358 mradi huu hadi kukamilika kwake utagharimu dola za Marekani milioni 407.4, umezungumzwa kwa muda mrefu. Katika mwaka ujao wa fedha tumetenga shilingi bilioni 15 kwa ajili ya kazi mbalimbali kabla ya kuanza kwa mradi. Mradi mwingine ni wa kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kakono wa megawati 87 mradi huu utagharimu dola za Kimarekani milioni 287.6 hadi kukamilika kwake. Katika mwaka ujao wa fedha Serikali itakamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa mradi. Jumla ya shilingi milioni 150 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ni wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji wa Rumakali wa megawati 222 ambao unagharimu dola za Kimarekani milioni 388.22 na umetengewa shilingi bilioni nane katika mwaka ujao wa fedha ya kukamilisha kazi mbalimbali kabla ya kuanza taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mradi.

Mradi mwingine ni wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji wa Malagarasi – wa megawati 49.5. Kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu, sio tu umeme wa Gridi ya Taifa utafika Kigoma, bali pia umeme unaoingia kwenye Gridi ya Taifa utazalishwa pia Kigoma. Fedha dola za Kimarekani milioni 144.14 kwa ajili ya ujenzi wa mradi huu zipo zimepatikana. Taratibu za kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa mradi huu zimefikia ukingoni. Jumla ya shilingi bilioni 13.97 zimetengwa kwa ajili ya kazi za awali.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ni wa kuzalisha umeme wa maji wa Kikonge; mradi huu una sehemu tatu ambao ni umwagiliaji, utalii na uzalishaji wa umeme na utagharimu dola za Kimarekani milioni 795.4.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha tumetenga shilingi bilioni 1.45 ili kukamilisha tathmini ya athari za mazingira ili taratibu za kupata fedha kwa ajili ya mradi huu zifanyike.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ni mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wa Mtwara wa megawati 300, Serikali imedhamiria kuzalisha megawati 300 pale Mtwara kwa kutumia gesi ili pamoja na mambo mengine kuendeleza Maendeleo ya Mikoa ya Kusini. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa dola za Kimarekani milioni 421.1; fedha za mradi huu zimepatikana kutoka

Serikali ya Japan. Pia tutajenga njia ya kusafirisha umeme utakaozalishwa hapa hadi Somanga Fungu mkoani Lindi. Tumetenga shilingi milioni 600 kwa ajili ya kuanza kazi za awali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha pia tutaanza ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme jua wa megawati 150 kule Shinyanga unaogharimu *Euro* milioni 115.3. Tumetenga shilingi bilioni 9.55 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha cha kwanza cha kuzalisha megawati 50, na pia kukamilisha taratibu za ufadhili wa awamu ya pili ya megawati 100. Vilevile katika mwaka ujao wa fedha tumepanga kukarabati mitambo katika kituo cha kuzalisha umeme pale Hale ili kizalishe umeme kwa uwezo wake wa megawati 21 badala ya megawati 10.5 zinazozalishwa kwa sasa. Kwa ajili ya kazi hiyo tumetenga shilingi bilioni10.25.

Mheshimiwa Spika, kuzalisha umeme ni jambo moja, lakini kuusafirisha na kuupeleka kwa watumiaji ni jambo tofauti. Katika mwaka ujao wa fedha tutatekeleza miradi mbalimbali mikubwa ya usafirishaji wa umeme ambayo pia ipo katika hatua mbalimbali na ningependa niitaje miradi hiyo. Mradi wa kwanza ni wa kuzalisha umeme kutoka kwenye mradi wetu wa Julius Nyerere hadi Chalinze wa kilovolti 400 mradi huu unagharimu dola za Kimarekani milioni 51.4 na shilingi bilioni 31.9; upo katika hatua za utekelezaji na katika mwaka huu wa fedha tumepanga shilingi bilioni 180 kwa ajili ya kuendelea na kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa pili ni wa kusafirisha Umeme Msongo wa kilovolti 400 kutoka Singida - Arusha hadi Namanga mradi huu unaendelea kutekelezwa gharama ya mradi ni dola za Kimarekani milioni 258.82.

Katika mwaka ujao wa fedha tumetenga shilingi bilioni 7.65 kwa ajili ya kuendelea na kutekeleza wa mradi huo.

Mradi mwingine ni wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovolti 220 kutoka Geita – Nyakanazi, gharama za mradi huu hadi kukamilika ni *Euro* milioni 45 ambapo kazi mbalimbali kwa ajili ya kuutekeleza zinafanyika ikiwemo ujenzi wa kituo cha kupoza umeme pale Nyakanazi na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Geita pamoja na kuendelea kusambaza umeme katika vijiji na maeneo mbalimbali ambapo njia hii inapita. Jumla ya shilingi bilioni 6.53 zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ni njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovolti 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi ambapo kazi zitakazotekelezwa katika mwaka ujao wa fedha ni ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Rusumo hadi Nyakanazi ambapo tumetenga shilingi bilioni 3.30 kwa ajili hiyo. Pia katika mwaka ujao wa fedha tutajenga njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovolti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma mradi huu unagharimu dola milioni 35. Mradi huu ambao pia utapeleka umeme wa mkubwa wa gridi katika Mkoani wa Kigoma tumetenga jumla ya shilingi bilioni 7.14 kwa ajili ya kuendelea na kazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ni wa kusafirisha umeme wa msongo wa kilovolti 33 ambao unaendelea sasa hivi kutoka Nyakanazi, Kakonko, Kasulu hadi Kigoma. Katika mwaka ujao wa fedha Serikali itakamilisha mradi huu ambao pia utafikisha umeme wa Gridi katika Mkoa wa Kigoma kabla ya mwezi Oktoba mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunajenga njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovolti 400 kutoka Iringa kwenda Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga. Gharama za mradi huu ni dola za Kimarekani milioni 595; fedha hizi zimepatikana. Katika mwaka ujao wa fedha tumetengwa shilingi bilioni 34.71 kwa ajili ya kazi za awali ikiwemo ujenzi wa vituo vya kupozea umeme pale Risada, Mbeya, Tunduma na Sumbawanga na kazi hiyo inafanyika.

Mheshimiwa Spika, pia tuna ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovolti 220 kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya *SGR*. *TANESCO* na *TRC* wanashirikiana katika kazi hii na katika mwaka ujao wa fedha tutahakikisha kwamba kilometa zote 415 zinazopaswa kuwekwa umeme kwa sasa zinafanyika kwa msogo wa kilovolti 220.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ni wa ukarabati na uboreshaji wa Gridi ya Taifa *(Grid Rehabilitation and Upgrading);* mradi huu unalenga kuimarisha Gridi ya Taifa kwa kukarabati na kuboresha vituo vya kupoza umeme katika maeneo mbalimbali nchini na utaanza kutekelezwa katika mwaka ujao wa fedha ambapo tumetenga shilingi bilioni 8.43 kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ni wa kusafirisha umeme ni kutoka Chalinze kwenda Kinyerezi wa kilovolti 400 gharama za mradi huu ni dola milioni 42.882 kwa upande wa njia ya kusafirisa umeme na dola milioni 71.4 kwa upande wa kituo cha kupozea umeme. Katika mwaka huu wa fedha tumetenga shilingi bilioni 40 kwa ajili ya kulipia fidia na kuanza kazi za ujenzi.

Mradi mwingine ni wa njia mbili kutoka Chalinze hadi Dodoma na Chalinze hadi Segera yote ni ya kilovolti 400. Miradi hii inagharimu dola za Kimarekani milioni 285.02 ambazo zinajumuisha njia ya usafirishaji wa umeme na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme. Katika mwaka huu wa fedha tumetenga shilingi milioni 225 kwa ajili ya kazi za awali na kukamilisha taratibu za kupata ufadhili.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine wa njia ya kusafirisha umeme ni wa kutoka Chalinze hadi Bagamoyo na Segera hadi Tanga yote ya kilovolti 220 ambayo utakagharimu dola za Kimarekani milioni 163.21 ambapo jumla ya shilingi milioni 50 zimetengwa kwa ajili ya kuratibu shughuli za awali za utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine wa kusafirisha umeme ni wa njia ya kilovolti 400 kutoka Sumbawanga kwenda Mpanda hadi Kigoma pamoja na kituo cha kupoza umeme Mpanda.

Mheshimwa Spika, mradi huu pia unapeleka umeme wa gridi kwenye Mikoa ambayo haina gridi ya Kigoma na Katavi. Gharama za mradi huu ni dola milioni 200.4 kwa upande wa njia ya kusafirisha umeme, na dola milioni 50 kwa upande wa kituo cha kupoza umeme. Benki ya Maendeleo ya Afrika imeonesha nią ya kutekeleza mradi huu. Katika mwaka ujao wa fedha taratibu za kukamilisha ufadhili pamoja na kazi za awali za kuanza mradi zitafanyika.

Mradi mwingine wa njia ya kusafirisha umeme ni mradi wa kilovolti 400 kutoka Somanga Fungu hadi Mkuranga ambao utagharimu dola za Kimarekani milioni 150 ambapo Serikali kupitia *TANESCO* imetenga shilingi bilioni 4.85 kwa ajili ya kulipa fidia na kumtafuta mshauri

mwelekezi kwa ajili ya kuhuisha upembuzi yakinifu wa mradi.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine ni Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo kilovoti 220 kutoka Shinyanga kwenda Simiyu. Mradi huu utagharimu shilingi bilioni 75 na fedha hizi ni za ndani, zipo tayari tumeshazipanga, lakini katika mwaka huu wa fedha tumetenga shilingi milioni 725 kwa ajili ya kazi za awali ikiwemo kulipa fidia wananchi watakaopitiwa na njia ya umeme.

Mheshimiwa Spika, Mradi mwingine wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo kilovoti 220 kutoka Benaco hadi Kyaka na Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Benaco na kupanua Kituo kile cha Kupoza Umeme pale Kyaka. Mradi huu unatekeleza dhamira yetu ya kupeleka umeme wa gridi katika Mkoa wa Kagera. Gharama za mradi huu ni dola za Marekani milioni 119.4 ambapo katika mwaka ujao wa fedha kazi zitakazofanyika ni kukamilisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira; kuandaa zabuni; kufanya usanifu wa mradi na kumpata Mkandarasi kwa ajili ya kuanza kazi za ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mradi mwingine ni wa kusafirisha Umeme wa Msongo wa kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Urambo na kutoka Urambo hadi Kidahwe, Mkoani Kigoma. Mradi huu pia una dhamira ya kupeleka umeme wa gridi katika Mkoa wa Kigoma na utagharimu shilingi bilioni 69.7. Katika awamu ya kwanza, Serikali imetenga shilingi bilioni 25 ambapo shilingi bilioni 20 ni kwa ajili ya ujenzi wa njia na kumalizia Kituo cha Kupoza Umeme pale Urambo na shilingi bilioni tano ni kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi waliopitiwa na njia ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mradi mwingine ni wa ujenzi wa Njia ya Msongo wa kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Mpanda huu kupitia Ipole na Inyonga. Mradi huu utapeleka pia Gridi ya Taifa katika Mkoa wa Katavi. Utekelezaji wake, ambao utahusisha ujenzi wa njia ya umeme na vituo vya kupozea umeme pale Ipole na Inyonga, umekwishaanza. Kwa mwaka ujao wa fedha Serikali imetenga shilingi bilioni 124 kwa ajili ya kuukamilisha. Fedha hizi pia zinajumuisha malipo ya fidia kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pia katika mwaka ujao wa fedha Serikali imepanga kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa umeme katika Makao Makuu ya Nchi hapa Dodoma. Mradi huu utagharimu Dola za Kimarekani milioni 167.7. Katika mwaka ujao wa fedha tumetenga jumla ya shilingi bilioni 6.57 kwa ajili ya maandalizi ya kazi ya kutengeneza umeme kuimarisha mfumo wa usambazaji wa umeme katika Makao Makuu ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imesikia kilio hivi karibuni cha kukatikakatika kwa umeme na Serikali imeutafutia muarobaini kadhia hiyo ambayo inatokana kwa sehemu kubwa na uchakavu wa miundombinu na kutotosheleza miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme. Kwa hiyo, Serikali imekuja na mpango kambambe wa kuimarisha gridi ya Taifa ambao tunaouita *National Grid Stabilization Project*. Mradi huu unahusu maeneo yafuatayo ya utekelezaji:-

(i) Tutanunua na kufunga *transformers* 6,000 kwa mpigo; *(Makofi)*

(ii) Tutanunua na kusimika nguzo za kusafirisha umeme 380,000; *(Makofi)*

(iii) Tutanunua nyaya na kufunga nyaya za urefu wa kilometa 46,200; *(Makofi)*

(iv) Tutanunua na kufunga mita za Luku 700,000; *(Makofi)*

(v) Tutajenga vituo vya kupooza umeme vikubwa *(grid substations)* 14; *(Makofi)*

(vi) Tutanunua na kufunga mashineumba kubwa *(power transformers)* 27, na

(vii) Tutajenga njia za kusafirisha umeme za urefu wa kilometa 948 za msongo wa kilovoti 132 na 220. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kukamilika kwa kipindi cha miaka minne na unatarajiriwa kutumia takribani shilingi trilioni 4.42. Katika mwaka ujao wa fedha tumetengewa shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kuanza kazi ya Mradi huu wa *National Grid Stabilization*. Katika hotuba yetu kuna Kielelezo Na. 17 kinaeleza mchanganuo wa miradi mbalimbali iliyopo chini ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie Miradi ya Nishati Vijijini; katika mwaka mwaka ujao wa fedha Serikali kupitia *REA* itaendelea kutekeleza miradi ya kusambaza nishati vijijini na kuhamasisha matumizi ya nishati hiyo. Aidha, Serikali itakamilisha kupeleka umeme katika vijiji vyote Tanzania Bara na kuanza utekelezaji wa mradi

maalum wa kupeleka umeme katika vitongoji vyote vya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi wa miradi ya kupeleka umeme vijijini na kurahisisha upatikanaji wa taarifa ya maendeleo ya miradi hiyo. Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali kupitia *REA* itaajiri Waratibu wa Miradi ya Umeme Vijijini kwa kila Jimbo. Waratibu hawa watakuwa kiungo cha mawasiliano na taarifa kati ya Waheshimiwa Wabunge, viongozi wengine wa kisiasa, wakandarasi, *REA, TANESCO* na wadau wengine. Kwa kushirikiana na *TANESCO*, waratibu hawa watakuwa na wajibu wa kutoa taarifa za mara kwa mara kwa viongozi ikiwemo Waheshimiwa Wabunge kuhusu maendeleo ya miradi ya *REA*. Tunafanya hivyo ili kutibu changamoto tuliyoiona ya ukosefu na mkatiko wa mawasiliano kuhusu maendeleo ya miradi ya *REA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie bei ya kuunganishiwa Umeme; kumekuwa na kilio cha muda mrefu cha wananchi wanaoishi maeneo ya mjini lakini yana sifa zinazolingana na maeneo ya vijijini huku wakilipa bei ya kuunganishiwa umeme wanayolipa watu wa mijini. Serikali imesikia kilio chao na tayari tumeunda timu inayojumuisha Wizara ya Nishati, *TANESCO* na *REA*. Timu hii itazunguka nchi nzima kuyabaini maeneo yenye sifa hizo maeneo ya mijini yenye sifa za vijijini na itafanya kazi hiyo kwa kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge wa maeneo husika. Maeneo yatakayobainishwa na timu hiyo yatajumuishwa kwenye bei za vijiji, yaani Sh.27,000. Zoezi hili litafanyika nchi nzima na kukamilishwa ndani ya miezi sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumze Miradi itakayotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijiji katika mwaka ujao wa fedha; kwanza tutaendelea na Mradi wa Kusambaza Umeme wa awamu ya tatu, mzunguko wa pili. Mradi huu kama mnavyofahamu unalenga kupeleka umeme katika vijiji vyote nchini. Jumla ya vijiji vitakavyofikiwa na mradi vijiji vyote nchini 12,347. Kwa sasa wakandarasi wameshaagizwa kufanya tathmini ya kupeleka umeme katika vijiji vilivyokosekana kwenye wigo wa awali wa mradi. Kwa hiyo, kuna vijiji ambavyo mwanzoni havikujumuishwa kwenye wigo tumevijumuisha safari hii na hakuna kijiji hata kimoja katika nchi hii kitakosa mradi wa kupeleka umeme katika kijiji hicho.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko ambayo yana mashiko, kwamba umeme unaofika vijijini unawafikia wakazi wachache, kama ni nguzo chache tu, kilometa moja. Serikali imesikia kilio hicho na sasa tupo katika hatua za mwisho za kupata fedha kwa ajili ya kuongeza wigo. Kwa hiyo, tutaongeza kilometa mbili zaidi kwa kila kijiji katika mwaka ujao wa fedha tofauti na kilometa moja iliyopo sasa ili kuwezesha wananchi wengi zaidi kwenye kila kijiji kupata umeme. Fedha hizo zipo na tumezitenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, gharama nzima ya Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini awamu ya tatu, mzunguko wa pili ni shilingi bilioni 1,240 na wigo wa awali utatekelezwa katika katika kipindi cha mieze 18. Katika mwaka ujao wa fedha tumetenga shilingi bilioni 164.54 ikiwemo kugharamia nyongeza ya wigo nilioulezea.

Mheshimiwa Spika, baada sasa ya kila kijiji kuwa na mradi wa umeme, Serikali imeandaa mradi mahususi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote hapa Tanzania.

Tanzania ina jumla ya vitongoji 64,760 na kati ya hivyo vilivyopata umeme ni vitongoji 37,610, ndivyo ambavyo havijafikiwa na umeme. Gharama ya mradi huu ni kubwa inatarajiwa kuwa shilingi trilioni 6.5. Katika mwaka ujao wa fedha Serikali imetenga shilingi bilioni 140 kwa ajili ya utambuzi wa wigo halisi wa mradi na kuanza utekelezaji wa mradi huu kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, pia kuna Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa IIB, mradi huu utahusisha njia za usambazaji umeme za kilometa 4,246 za msongo mdogo na ufungaji wa mashineumba 1,277 na kuunganisha wateja wa awali 95,334 katika vitongoji 1,686 katika Mikoa ya Arusha, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Morogoro, Njombe, Simiyu na Songwe. Gharama za Mradi huu ni shilingi bilioni 227. Katika Mwaka ujao wa fedha tumetenga shilingi bilioni 24.08 kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, pia tunaendelea na Mradi wa Ujazilizi wa Mzunguko wa IIC kazi zitakazofanyika katika mradi huu ni kujenga njia za msongo mdogo wenye kilometa 6,562, kufunga mashineumba 1,932 na kuunganisha wateja wa awali 131,719 katika vitongoji 1,752 katika Mikoa ya Iringa, Manyara, Mara, Mtwara, Rukwa na Ruvuma. Gharama za mradi huu ni shilingi bilioni 100 na katika mwaka ujao wa fedha tumetenga shilingi bilioni 31.10 kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunatekeleza Mradi wa Kituo cha Kupoza Umeme pale Ifakara na Ujenzi wa Miundombinu ya Usambazaji. Mradi huu unahusisha ujenzi wa kilometa 299 za njia za msongo wa kati na mdogo na ufungaji wa mashineumba 26 na kuunganisha vijiji nane na vitongoji saba katika Wilaya za Kilombero na Ulanga.

Gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 23.62 na kwa mwaka wa fedha tumetenga shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kukamilisha mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Mradi mwingine ni wa Kupeleka Umeme katika Maeneo ya Vijiji-Miji awamu ya pili yaani *peri-urban*. Kazi zitakazofanyika ni kupeleka umeme katika maeneo 153 ya pembezoni mwa Majiji ya Arusha, Dodoma na Mwanza na kwa kazi hiyo tumetenga shilingi bilioni 31.33 katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, mwaka ujao wa fedha pia tutafunga Mifumo ya Umeme Jua katika Taasisi mbalimbali za Umma katika Wilaya nane na kazi hiyo ni awamu itaendelea katika awamu ijayo na tumetenga shilingi bilioni 1.5 kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha vile vile tumepanga kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa miradi midogo midogo ya *mini grids* ya kuzalisha na kusambaza umeme kutokana na vyanzo vya jua, upepo na maporomoko madogo madogo ya maji pamoja na tungamotaka katika maeneo yaliyo mbali na gridi ya Taifa. Mradi huu utahusisha ufungaji wa mitambo ya umeme kwenye vijiji 35 katika visiwa 47 katika Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Nyasa na *Delta* ya Rufiji.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie katika mwaka ujao wa fedha sasa tutapeleka umeme katika visiwa 47 hapa nchini ambavyo kwa hali ya kawaida haviwezi kupata umeme wa gridi, Gharama nzima ya mradi ni shilingi bilioni 54.48 na tumeanza kutenga bilioni 20 kwa ajili ya kazi hiyo katika mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama unafahmu asilimia kubwa karibu asilimia 89 ya kaya zote hapa nchini zinatumia kuni na mkaa kama chanzo kikuu cha nishati ya kupikia. Jambo hili husababisha uharibifu wa mazingira, lakini pia na uharibifu wa afya katika mwaka ujao wa fedha na hili jambo jipya Serikali itatekeleza mipango, mikakati na miradi ya matumizi ya nishati safi na salama ya kupikia katika maeneo ya vijijini. Kwa ajili hiyo, tumetenga shilingi milioni 500 ili kufanya kampeni kubwa ya kuhamasisha matumizi ya nishati bora ya kupikia pamoja na tafiti za kubaini nishati bora ya kupikia, mifumo sahihi na vivutio vya kusambaza nishati safi ya kupikia katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika mwaka ujao wa fedha tumepanga kutumia shilingi bilioni 10 kutekeleza Mradi wa Kupeleka na Kusambaza Gesi Asilia kwa wananchi walio karibu na mkuza wa bomba kuu la gesi katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani. Mradi huu wa maeneo ya vijijini ambao ni wa kwanza hapa nchini utakuwa wa majaribio. Serikali kupitia *REA* itaendelea kutoa ruzuku kwa *TPDC* na wadau wengine ili kupanua huduma hiyo ya kupeleka umeme wa gasi vijijini katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, inafahamika pia kwamba Watanzania wengi waishio vijijini wanalipa fedha nyingi zaidi kununua nishati ya mafuta, lakini pia wananunua mafuta ambayo siyo safi wala salama. Ili kutibu kadhia hii, Serikali imebuni katika mwaka ujao wa fedha Mradi wa Uwezeshaji na Uendelezaji wa Vituo Vidogo Vidogo vya Bidhaa ya Mafuta katika maeneo ya vijijini ambayo hayana vituo vya mafuta na tutafanya hivi kwa mkopo nafuu. Mradi huu ni mpya na kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuandaa wigo wa mradi, kutangaza zabuni

na kuwapata waendelezaji wadogo wadogo wa vituo vya vijijini ili kuanza ujenzi wa vituo hivyo. Katika Mwaka 2022/2023, Serikali imepanga kutumia Shilingi Bilioni 2.00 kutekeleza mradi huu. Mradi huu ni wa majaribio katika jitihada za kutafuta mbinu bora zaidi za kusambaza nishati ya mafuta salama na kwa bei nafuu vijijini.

Mheshimiwa Spika, tutakapofanikiwa katika mwaka ujao wa fedha tutapanua ili watu wengi zaidi wajenge vituo vijijini au kutafuta njia nyingine katika dhamira ya kufikisha nishati ya mafuta vijiji ambayo ni safi, salama na bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, pia tumebuni katika mwaka ujao wa fedha Mpango wa Kuimarisha Vyanzo vya Mapato kwa ajili ya kupeleka Umeme Vijijini. Kama nilivyoeleza hapo awali pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kupeleka umeme vijijini, bado vitongoji 37,610 kati ya vitongoji 64,760 hapa nchini, havijafikiwa na umeme. Baada ya kufanya tathmini ya mahitaji ya fedha, imebainika kwamba jumla ya shilingi trilioni 6.5 zitahitajika kupeleka umeme katika vitongoji vyote nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mwenendo wa bajeti inayopewa *REA* kila mwaka itachukua zaidi ya miaka 15 kufikisha umeme katika vitongoji vilivyosalia. Kwa muktadha huo, Serikali itahakikisha kwamba rasilimali fedha inapatikana ili kufikisha umeme katika vitongoji vyote. Ili kufikia azma hiyo, Serikali imeandaa Mpango Maalum utakaowezesha kuongeza fedha zinazoingia katika Mfuko wa Nishati Vijijini kwa lengo la kutekeleza miradi ya kupeleka umeme vijijini kwa muda mfupi zaidi. Mpango huo utahusisha kupata vyanzo vipya vya

mapato pamoja na kuongeza michango kwa kwa Washirika wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka ujao wa fedha Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha itaangalia uwezekano wa wakandarasi watakaowezesha upatikanaji wa fedha pamoja na utekelezaji wa miradi wao wenyewe katika mfumo ambao unaitwa *EPC+F* yaani *Engineering, Procurement, Construction Plus Financing*. Mfumo huu unatumika siku hizi Mkandarasi anakuja na fedha yake ambayo wanakubaliana na Wizara ya Fedha kwa masharti nafuu, anatoa fedha, anajenga mwenyewe, anawakabidhi mradi. Tumeamua katika mwaka ujao wa fedha tutazungumza na Wizara ya Fedha kwamba kwa miradi ya *REA* twende kwa mwendo huu ili tuweze kwenda haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Serikali imepanga kutumia shilingi milioni 500 ili kubuni, kuanzisha, kuandaa na kutekeleza mikakati na mipango ya upatikanaji wa fedha za kutosha kutekeleza miradi ya nishati vijijini kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya *REA* itakayotekelezwa katika mwaka ujao wa fedha; ni Kuwezesha Waendelezaji Binafsi wa Miradi ya Nishati katika Maeneo ambayo Hayajafikiwa na Gridi ya Taifa; pia tutakuwa na Mradi mzuri ambao tumeutengea shilingi bilioni 20 wa Kupeleka Umeme katika Maeneo ya Wachimbaji Wadogo wa Madini, katika maeneo ya Viwanda na maeneo ya Kilimo. Vilevile tunao mradi mwingine wa kupeleka umeme katika miradi ya shule vijijini pamoja na Mahakama za Mwanzo. Gharama za kutekeleza miradi hii na fedha zilizotengwa zinaonekana katika sehemu ya D3 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa rasilimali jotoardhi. Katika mwaka mwaka ujao wa fedha Serikali itaharakisha maandalizi ya uzalishaji wa umeme kwa kutumia rasilimali ya jotoardhi katika miradi minne. Mradi wa ngozi Mbeya, mradi wa Songwe kule Songwe, mradi wa Kiajo-Mbaka - Songwe na mradi wa *natron* kule Arusha ambayo kwa pamoja inauwezo wa kuzalisha megawati 200. Jumla ya Shilingi Bilioni 5.18 zimetengwa kwa ajili ya maandalizi mbalimbali ya kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia. Kwa miaka mingi imekuwa ni ndoto ya nchi yetu kuingia kwenye uchumi wa gesi ambao utakuza mapato ya Serikali na kuwanufaisha wananchi. Katika mwaka ujao wa fedha sasa, Serikali itachukua hatua madhubuti ili kuharakisha azma hiyo. Hatua zitakazochukuliwa na Serikali katika mwaka ujao wa fedha ili kutekeleza azma hiyo ni kama zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tutaendelea na udhibiti wa mkondo wa juu wa mafuta na gesi. Serikali kupitia *PURA* katika mwaka ujao wa fedha itasimamia uchorongaji wa visima mbalimbali vya gesi na mafuta hapa nchini na kufanya ukaguzi katika maeneo yote ya utafutaji na uzalishaji wa gesi asilia. Lengo ya kazi hii ni kuhakikisha kwamba sheria zinafuatwa katika mikataba ambayo imeingiwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali kupitia *PURA* itashamirisha shughuli za utafutaji, utafiti na uendelezaji wa mafuta na gesi nchini. Kwa ajili hiyo tutaanza katika mwaka ujao wa fedha, maandalizi za kunadi vitalu vilivyowazi katika maeneo ya nchi kavu na baharini kwa

kutumia mikataba maalum. Vilevile, Serikali kupitia *PURA* tutaandaa katika mwaka ujao wa fedha ramani ya kidigitali yenye taarifa za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi katika maeneo mbalimbali inaitwa *interactive digital petroleum activities map* ili kuongeza wigo wa utekelezaji wa shughuli za mkondo wa juu wa petroli nchini. Jumla ya Shilingi Bilioni 1.69 zimepangwa kwa ajili ya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee miradi ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kati. Serikali ilitenga huko nyuma vitalu vya mafuta na gesi vya kimkakati kwa ajili ya kuipatia *TPDC* ili kuijengea uwezo na uzoefu. Vitalu hivyo ni Mnazi Bay Kaskazini, Eyasi-Wembere, Songosongo Magharibi pamoja na Ziwa Tanganyika. Vilevile vitalu vinaitwa 4/1B na 4/1C kule Mtwara. Katika mwaka ujao wa fedha Serikali imetenga Shilingi Bilioni 102.167 kwa ajili ya kazi mbalimbali za maandalizi ya uchimbaji wa gesi na mafuta katika vitalu hivyo. Serikali, kupitia *TPDC*, pia itaharakisha mchakato wa kuwapata wabia wa sekta binafsi ili kushirikiana na *TPDC* katika kuendeleza vitalu hivyo.

Mheshimiwa Spika, pia vipo vitalu mbalimbali vya mafuta na gesi vinavyoendeshwa na sekta binafsi ambavyo *either* vinazalisha gesi au vimeonesha dalili kubwa ya kuwa na gesi. Vitalu hivyo ni Ruvu, Ruvuma, Songosongo, Mnazi Bay, Kilosa - Kilombero na vitalu Namba 1, 2 na 4. Katika mwaka ujao Serikali kupitia *PURA* na *TPDC* itasimamia kuhakikisha kwamba waendeshaji wa vitalu hivi wanaviendesha kwa mujibu wa ratiba ya uendelezaji iliyopo kwenye mikataba ili kuongeza uzalishaji wa gesi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee mradi wa *LNG*, mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia *(LNG)*. Imekuwa ni ndoto ya nchi yetu kwa miaka mingi sasa kuchakata gesi nyingi iliyogunduliwa kwenye bahari ya kina kirefu kwa ajili ya mauzo nje ya nchi na matumizi ya gesi hapa ndani. Mazungumzo kati ya Serikali na makampuni ya gesi na mafuta duniani yamekuwa mara kwa mara yakiendelea na kukwama.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba hatua ya kwanza na muhimu ya mazungumzo kati ya Serikali na makampuni ya mafuta na gesi kuhusu mradi huu wa *LNG* imefanikiwa. Naomba kurudia, naomba kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba hatua ya kwanza na muhimu ya mazungumzo kati ya Serikali na makampuni ya gesi na mafuta kuhusu mradi wa kuchakata na kusindika gesi kule Lindi – *LNG* imefanikiwa. Naomba nitamke rasmi kwamba baada ya tarehe 9 mwezi huu wa Juni tutakuwa tayari kusaini Mkataba Hodhi *(HGA)* kati ya Serikali na makampuni haya. Hii ni hatua muhimu sana tumekubaliana katika mambo ya msingi na kwa mara ya kwanza kuna dalili njema sasa kwamba tutatekeleza mradi wa *LNG* kule Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, katika mwaka ujao wa fedha kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha mazungumzo ya mwisho ya hatua za utekelezaji wa mradi na hatimaye kushirikiana na makampuni haya kwenye usanifu wa awali wa kihandisi wa mradi kabla ya hatua ya maamuzi ya mwisho ya uwekezaji yaani *NFID*.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kutokana na ukubwa na manufaa yatakayopatikana katika mradi huu wa *LNG*,

ikiwemo kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi lakini pia katika maeneo mradi utakapotekelezwa, Serikali ina mpango katika mwaka ujao wa fedha wa kuanzisha Ukanda Maalum wa Kiuchumi *(Special Economic Zone)* katika eneo la mradi kule Lindi ambapo maeneo yatatengwa na kuendelezwa kwa ajili ya uwekezaji, uzalishaji na biashara. Hatua hii ni pamoja na kuimarisha shughuli za uchumi wakati wa utekelezaji wa mradi, pia itawezesha manufaa ya mradi kuendelea, manufaa wakati wa ujenzi kuendelea hata pale ujenzi utakapoisha au mradi utakapoisha, utakapofikia ukomo wake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha Wizara ya Nishati itaendelea kuzungumza na wadau kufanya tathmini mbalimbali kuhusu utekelezaji wa azma hii ya kuanzisha *special economic zone* katika eneo la mradi wa *LNG*.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee kuhusu miradi mbalimbali ya ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa gesi. Katika mwaka ujao wa fedha Serikali imetenga shilingi bilioni 3.89 kwa shughuli za usambazaji wa gesi asilia katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam. Kwa upande wa Mkoa wa Pwani kwa ajili hiyo pia tumetenga shilingi bilioni 5.1 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi viwandani na majumbani tukiwa na nia ya kushamirisha na kuhamasisha matumizi ya gesi asilia. Vilevile, katika Mkoa wa Lindi tunampango huo na tumetenga Shilingi Bilioni 5.49 kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sasa kuhusu mradi wa ujenzi wa vituo vya *CNG*, gesi asilia iliyokandamizwa katika maeneo mbalimbali. Serikali katika mwaka ujao wa fedha kupitia *TPDC* tumepanga kutekeleza mradi wa

ujenzi wa vituo vya kujazia gesi kwenye magari katika Bohari Kuu za Serikali Dodoma na Dar es Salaam. Lengo ni kuwezesha magari mengi zaidi ya Serikali na watu binafsi kutumia gesi inayozalishwa nchini. Kwa kuanzia, magari yote ya Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zilizoko chini yake ndiyo yataanza kuwekwa mfumo wa kutumia gesi asilia mara tutakapomaliza kazi ya kufunga vituo hivyo. Na katika mwaka huu wa fedha tumetenga Shilingi Bilioni Moja kwa ajili ya maandalizi ya shughuli hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kupitia *TPDC*, tumepanga mradi mkubwa wa ujenzi wa kituo mama yaani *CNG mother station* cha kusindika gesi katika mgandamizo mkubwa kwa ajili ya kuhudumia wateja wa *CNG* katika magari na pia kusambaza katika vituo dada yaani *CNG daughter stations* vitakavyokuwa mbali na maeneo ya miundombinu ya mabomba. Sambamba na hilo, *TPDC* itajenga vituo dada vya kupokea na kuhifadhi *CNG* kwa ajili ya matumizi ya gesi asilia kwenye magari, viwandani pamoja na nishati ya kupikia. Tumetenga kwa ajili hii ya kujenga vituo dada na vituo mama shilingi bilioni 23.2 kwa ajili ya utekelezaji wake. Lakini siyo pesa tu za Serikali, tunayo makubaliano na makampuni kadhaa ya sekta binafsi pika na wenyewe kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi hii.

Mheshimiwa Spika, pia tunayo miradi kadhaa miwili ya kusafirisha gesi kwenda nchi jirani. Tunayo makubaliano na Kenya – *MOU*, tunayo makubaliano na Uganda vilevile ya *MOU* ya kujenga mabomba ya kupeleka gesi katika nchi hizo. Kazi zitakazofanyika katika mwaka ujao wa fedha ni maandalizi ya miradi hiyo, ambapo kwa upande wa bomba la kwenda Uganda, Serikali imetenga shilingi milioni 635 na kwa upande wa

bomba la kwenda Kenya tumetenga shilingi milioni 656.1 kwa ajili ya kazi mbalimbali za awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunafahamu kwamba tunao mradi wa bomba la kusafirisha mafuta kutoka Uganda kuja Tanzania *ICOP*. Kazi mbalimbali zitaendelea kufanywa katika maeneo mbalimbali ikiwemo kukamilisha fidia wananchi 9,122 waliopitiwa na mradi huo. Serikali imetenga shilingi bilioni 5.5 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali kwenye mradi huo.

Mheshimiwa Spika, pia tumebuni mradi kwa kushirikiana na wenzetu wa Zambia wa bomba la kusafirisha mafuta safi kutoka Dar es Salaam - Tanzania hadi Ndola - Zambia. Tunafahamu kwamba tunao mradi, tunalo bomba la *TAZAMA* ambalo ni jembamba lakini linasafirisha mafuta ghafi. Kwa hiyo, tumezungumza na wenzetu wa Zambia, tumebuni mradi ambao utapita katika mkuza wa bomba lilelile la *TAZAMA*. Tumefanya mazungumzo na wenzetu wa Zambia na tumetenga Shilingi Milioni 500 katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya maandalizi ya kazi mbalimbali za utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee kuhusu mafuta. Pamoja na mwenendo wa bei za mafuta duniani kuwa changamoto, nchi yetu imeendelea kufanya vizuri katika kuhakikisha kwamba mafuta yanakuwepo nchini wakati wote. Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itaendelea kuimarisha mfumo wa uagizaji na uingizaji wa mafuta ili kuhakikisha usalama wa mafuta hapa nchini wakati wote. Na katika kutekeleza azma hiyo, katika mwaka ujao wa fedha, Serikali sasa itatimiza ile azma ya muda mrefu ya kuanzisha hifadhi ya kimkakati ya mafuta

*(strategic petroleum reserve)* ambayo itakuwa chini ya *TPDC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa hifadhi hii ni muhimu ili kuwezesha usalama na uhakika wa upatikanaji wa mafuta wakati wote. Tunawashirikisha sekta binafsi katika eneo hilo. Kwa hiyo, kama sehemu ya maandalizi, Serikali kupitia *TPDC* tayari inayo maeneo mbalimbali, kwa sababu hii hifadhi ya kimkakati haiko eneo moja tu nchini, inatawanywa katika maeneo mbalimbali ya nchini na tayari *TPDC* inayo maeneo kama vile Kigamboni, Chongoleani - Tanga, Zuzu - Dodoma, Isaka - Shinyanga, Makambako - Njombe, Kibirizi - Kigoma na Mpanda - Katavi. Kwa hiyo, kazi hiyo inaendelea vizuri na miundombinu hii itashirikisha sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, pia katika mwaka ujao wa fedha Serikali itaiwezesha zaidi *TPDC* kushiriki katika shughuli ya uagizaji wa mafuta kwa jumla na itajengewa uwezo wa kimtaji na kitaalam na kupewa kipaumbele kama taasisi ya kimkakati kwa nchi, *TPDC*. Vilevile, *TPDC* inayo kampuni tanzu inayoitwa *TANOIL* ambayo imekuwa inanunua mafuta na kuyauza kwa wateja wa rejareja. Serikali itaendelea kuimarisha ushiriki wa *TANOIL* katika biashara ya rejareja. Tumewatengea shilingi bilioni mbili katika mwaka ujao wa fedha ili kujiimarisha. Lakini vilevile tumetenga shilingi bilioni 12.11 kukarabati tanki kubwa Namba Nane pale *TIPER* ambalo litamilikiwa na *TANOIL* kwa ajili ya kuhifadhi na kusambaza mafuta.

Mheshimiwa Spika, vilevile, tumeelekeza kwamba Serikali sasa kupitia *TANOIL* iwe na mtandao wa vituo vya mafuta nchi nzima, na kwa kuanzia katika mwaka ujao wa fedha *TANOIL* inatarajiwa kuwa na vituo vya mafuta 50 kwa mpigo katika maeneo mbalimbali hapa nchini

kama sehemu ya kujihakikishia usalama wa mafuta kama sekta binafsi itashindwa. Na kwa ajili hiyo tumetenga Shilingi Bilioni 2.5 kwa ajili ya kuanza kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika vipaumbele tulivyotaja ni kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji wa nishati, tumeanza na kwa sasa kwa upande wa uzalishaji wa umeme tunayo mazungumzo ya kuzalisha megawati 950 kwa kutumia jua, upepo na makaa ya mawe. Tuko katika hatua za mwisho za kuwaalika na kuwapa *award* kupitia tenda makampuni haya yanayofanyiwa upekuzi ili tuzalishe umeme sasa kwa kutumia mfumo huu kwa sekta binafsi. Vilevile, *TANESCO* inayo miradi 53 yenye muelekeo wa kuweza kutekelezwa na sekta binafsi. Na tumeorodhesha, mkienda kwenye kiambatisho 19 cha Hotuba yetu mtaona miradi hiyo na mpaka sasa tayari tuna majadiliano na tunaelekea kuingia mikataba na makampuni ya sekta binafsi katika miradi hii 53 kwa uzalishaji wa megawati 597. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya miradi hii, Wizara pia inayo mipango, mikakati na mambo mengineyo katika kutekeleza sekta yetu. Katika mwaka ujao wa fedha tutabuni na kutekeleza kwanza mkakati wa nishati jadidifu *(renewable energy strategy* na *roadmap)*. Lakini vilevile tutabuni na kutekeleza mkakati wa matumizi bora ya nishati na mpango wa utekelezaji. Lakini vilevile, tutabuni na kutekeleza mkakati wa tungamotaka yaani *biomass strategy*. Nchi hii asilimia zaidi ya 85 ya matumizi ya nishati ni *biomass* ni tungamotaka. Kwa hiyo, lazima tuwe na mkakati. Vilevile, tutapitia upya *power system master plan* yetu ili kuhakikisha kwamba inaendana na mahitaji ya sasa. Vilevile, tutaendelea kutekeleza mpango kabambe wa nishati vijijini *(rural energy master*

*plan)* ambao pia unahusisha usambazaji wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara inazo taasisi mbalimbali zinazotoa huduma moja kwa moja kwa wananchi ambazo ufanisi wa taasisi hizi una *impact* ya moja kwa moja na ufanisi wa shughuli na taasisi na wadau wengine nchini. Kwa hiyo, taasisi hizo ni *TPDC, EWURA, PURA, PBPA, REA na TANESCO*. Kwa hiyo, katika mwaka ujao wa fedha kama tulivyoeleza mbele katika kipaumbele tunao mpango wa kuchukua hatua mbalimbali za kuziimarisha taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa mahusus naomba niongelee kuhusu *TANESCO* Serikali italiwezesha na kulipa nafasi Shirika hili kuendelea na mageuzi makubwa yanayoendela sasa ya kuliimarisha na kuweza kutoa huduma bora zaidi kwa wateja wake. Katika mwaka ujao wa fedha, Shirika hili sasa linategemea kutekeleza mradi wa kubadilisha mita zote za *LUKU* kuanzia mwaka ujao tunaenda awamu kwa awamu na kuweka mita janja yaani *smart meter* ambazo zitakuwezesha kununua umeme na kuuingiza moja kwa moja bila kwenda kubonyezabonyeza kwenye mita. Kwa hiyo, kazi hiyo itaanza katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile, *TANESCO* itaendelea na mradi wake wa nikonekt ambapo utaweza kuomba kuunganishiwa umeme kwa kutumia simu yako kama vile ambavyo unaenda kwenye M-Pesa. Hutalazimika kwenda *TANESCO*, hutalazimika kugongewa mihuri, hutalazimika kuongea na kishoka na baadhi ya watu wameshaanza. Tumeanza majaribio, tunaamini mradi huu utakapofanikiwa nchi nzima tutaondoa ile adha ya ucheleweshaji wa kuunganishiwa, urasimu wa

kuunganishiwa lakini na rushwa na udanganyifu kwa watu wanaotaka kuunganishiwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, jingine kuhusu *TANESCO*. Serikali inatafakari namna sahihi ya kutekeleza mpango wa kubadilisha deni la *TANESCO* kwa Serikali na kuwa hisa za Serikali yaani *debt to equity conversion* ili kuweka vitabu vya *TANESCO* katika hali nzuri itakayoliwezesha Shirika hili kwenda kupata fedha za miradi bila kutegemea miradi ya Serikali. Tukipata nafasi tutaelezea vizuri. Sehemu kubwa ya deni la *TANESCO* kwenye vitabu vya *TANESCO* ni deni la makaratasi, ni deni ambalo liko kwenye upande wa Serikali lakini lipo pia kwenye upande wa *TANESCO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Serikali kuchukua nusu ya deni la *TANESCO* haitaingia gharama yoyote ni kubadilishana karatasi lakini vitabu vya *TANESCO* vitakuwa katika hali nzuri na miaka ijayo hapa hatutakuja tena kuomba hela za miundombinu ya *TANESCO* kwa sababu ina uwezo wa kuchukua hela kutoka kwenye sekta binafsi. Kwa hiyo, kazi hii tunaifanya kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na tutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitoe shukrani mbalimbali katika kazi hizi tulizofanya mwaka uliopita na tunazotarajia kufanya kazi mwaka ujao tumeshirikiana na washirika wa maendeleo wengi, jumuiya ya nchi wahisani na wadau mbalimbali. Naomba nitoe shukrani kwa niaba ya Serikali kwa wafuatao; Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, Shirika la Fedha Duniani *(IMF)*, Benki ya Ushirikiano ya Japan *(JBIC)*, *United Bank for*

*Africa* na *Economic Development Fund (EDCF)* ya Korea. *(Makofi)*

Wengine ni *Geothermal Risk Mitigation Facility* pamoja na *JICA, KfW, AFD* ya Ufaransa, *DFID* - Uingereza, *SIDA* - Sweden, *NORAD* - Norway; Umoja wa Ulaya, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP), CIDA* ya Canada na *USAID* ya Marekani.

Mheshimiwa Spika, shukrani za mwisho napenda nimshukuru sana Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Wakili usipomuita Wakili mnagombana. Wakili Stephen Byabato kwa kunisaidia kutekeleza majukumu yangu.

Napenda kumshukuru Katibu Mkuu - Mhandisi Mramba, Naibu Katibu Mkuu - Bwana Kheri Abdul Mahimbali katika kipindi chote ambacho nimefanya kazi hii wamenisaidia sana na wamenipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu na kweli wameonesha ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Napenda pia niwashukuru sana Wakuu wa Idara, Vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi mbalimbali na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara yetu na watumishi wote wa Wizara kuanzia madereva, wahudumu, makarani kwa kweli wao ndio wamewezesha kazi hizi zifanyike na ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kushukuru sana Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kwa msaada mkubwa ambao imetupa katika kipindi hiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kengele ya pili ilishagonga dakika mbili omba pesa.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa hiyo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa, lihidhinishe jumla ya shilingi 2,705,981,533,000 na hii kujumlisha na *addendum* ya shilingi bilioni 200 kama ilivyowasilishwa na Waziri wa Fedha na hivyo kufanya maombi yetu kuwa shilingi 2,905,981,533,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na taasisi zake mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo; shilingi trilioni mbili...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hebu tusomee hiyo jumla kwanza ya fedha zinazoombwa.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, sawa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa lihidhinisha bajeti ya jumla ya shilingi 2,905,981,533,000.

**SPIKA:** Laki tano na ngapi?

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, shilingi 533,000.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Waziri kabla hujavuka hapo.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ndio.

**SPIKA:** Taarifa tulizonazo ngoja nikusomee hizi takwimu ili uone tofauti na hiyo ya kwako hapo ili ujue fedha mahususi unazoziomba, hapa kuna jumla pamoja na hayo marekebisho au hayo mabadiliko yanaonekana ni 2,823,029,576,000 ndio taarifa mimi nilizonazo hapa mbele. Sasa kwa sababu tumejaribu kutazama ngoja nitakuletea hayo makaratasi hapo mbele ili kama ndio takwimu...

Uko nazo hizi karatasi pia hapo mbele?

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ndio.

**SPIKA:** Katibu hebu, kwa sababu katika mabadiliko yaliyoletwa kuna mabadiliko kwenye *Vote 58* inasema mabadiliko hapa yanatakiwa kusomwa shilingi 82,951,957,000; wakati huo huo mabadiliko mengine yaliyopo yanasema badala ya kusoma shilingi bilioni 2.1 ama tuseme shilingi 2,114,972,000 sasa isome shilingi 55,314,972,000 halafu mabadiliko mengine ambayo tunayo hapa mbele ya badala kusomwa shilingi 29,751,957,000 isomwe shilingi 82,951,957,000.

Sasa ukizijumlisha hizi na hii karatasi nadhani pia imetoka huko kwako nadhani haitakuja trilioni 2.9 isipokuwa itakuwa shilingi 2,823,029,576,000; kama hii ndio ambayo unakubaliana nayo basi uisome hii ambayo na sisi ndio tunayo kama marekebisho. Kama hii sio basi tuelezee kidogo hapo kwenye marekebisho ili na sisi turekebishe huku halafu tujue kiasi halisi kinachoombwa na Wizara ya Nishati.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, hii ambayo tumesoma shilingi 2,823,029,576,000 hizi ni pesa za maendeleo peke yake, kwa sababu hapo juu inasema *for development projects.* Sasa sisi tulielezwa kwamba ukijumlisha kwa sababu pesa tulizoongezewa ni shilingi bilioni 200 katika bajeti ambayo ilipitishwa na Kamati na hizi shilingi bilioni 200 zimegawanywa kwamba nyingine zitaenda kwenye maendeleo na asilimia 76 itaenda kwenye maendeleo katika hizi na asilimia 24 itaenda kwenye *OC*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo inawezekana kabisa kwamba ukichukua za maendeleo peke yake, ni dhahiri

zinaweza kuwa hizo, labda ukichanganya sasa na zile ambazo zimepelekwa kwenye matumizi mengineyo zinaweza kuwa shilingi bilioni 2.905 kama nilivyozungumza hapa awali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya sawa.

Katibu hapa pia amefanya hizo hesabu zikijumlishwa zote pamoja na hiyo shilingi bilioni 200 iliyoongezeka kwa hiyo inakuwa trilioni 2.9; kwa hiyo isome ile uliyokuwa unaisoma mwanzo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kutopunjwa kwa hiyo naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa liidhinishe bajeti ya jumla ya shilingi 2,905,981,533,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na taasisi zake katika mchanganuo ambao umeelezewa na utarekebishwa lakini hiyo ndio jumla.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara vilevile hotuba hii ina vielelezo mbalimbali ambavyo vimeambatishwa kwa ajili ya ufafanuzi wa masuala muhimu yanayohusu sekta.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

Sasa nimuite Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ili aje awasilishe maoni ya Kamati hii. Sioni yeyote akisimama kutoka upande wowote sasa Mheshimiwa Mwenyekiti alihitaji kubadili miwani kidogo. Mwenyekiti, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, karibu. *(Makofi)*

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Nishati, awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametujalia kuweza kuiona siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Julai 2022 naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati Fungu Namba 58 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, naomba nijeelekeze moja kwa moja kwenye uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022, katika uchambuzi wetu naomba nijeelekeze kwenye eneo la ukaguzi wa miradi ya maendeleo; Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya maendeleo iliyotekeleza na Wizara ya Nishati, ziara hiyo ilifanyika katika Mkoa wa Dar es salaam na Pwani ambako jumla ya miradi mitatu ilikaguliwa kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati kuanzia ukurasa wa tatu hadi ukurasa wa 11 ambayo miradi hiyo

ni mradi wa *REA* kwenye eneo la Mkuranga, mradi wa *Kinyerezi I Extension,* lakini vilevile mradi wa Julius Nyerere.

Mheshimiwa Spika, baada ya ukaguzi huo naomba nijielekeze kwenye maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kuhusiana na mradi wa *REA* kwa kuwa kasi ya miradi ya usambazaji wa umeme vijijini ni kubwa lakini haiendani na kasi ya idadi ya wananchi wanaounganishwa umeme, Kamati inasisitiza kuwa uhamasishaji ufanyike katika maeneo yote ambayo miradi ya *REA* imepitia ili wananchi waweze kuunganishiwa umeme na hivyo kuchochea maendelea katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili naomba Serikali iweke utaratibu utakaowezesha gharama za wakandarasi wa kufunga na kutandaza mfumo wa nyaya za umeme majumbani yaani *wiring* na ukaguzi, ziwe nafuu na ambazo wananchi watazimudu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mradi wa Kinyerezi, *TANESCO* ihakikishe inasimamia kikamilifu utekelezaji wa mradi wa *Kinyerezi I Extension* wa megawati 185 ili ukamilike kwa wakati na hivyo kusaidia kuongeza upatikanaji wa umeme nchini. Aidha kwenye eneo la mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere maoni ya Kamati kwamba kutokana na umuhimu wa mradi wa bwawa la kufua umeme wa Mwalimu Julius Nyerere kwa uchumi wa Taifa, Wizara ihakikishe inazipatia ufumbuzi kwa wakati changamoto zote zinazokwamisha utekelezaji wa mradi huu kwa mujibu wa mpango kazi ulioridhiwa na pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, aidha mazungumzo yoyote yanayohusu mradi huu yahusishe viongozi wakuu wa nchi

zinazohusika ili tusije tukakwama na kufikia hatua za kupelekana kwenye vyombo vya kisheria.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine utunzaji wa mazingira wa vyanzo vya maji vya Mto Rufiji visimamiwe ipasavyo ili visiharibiwe na kuleta athari katika mradi, lakini vilevile kutokana na mradi kuchelewa Serikali ihakikishe majadiliano yote yanazozungumzia ongezeko la muda wa ukamilishaji wa mradi ihakikishe yanazingatia kutoongeza gharama za mradi husika kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na uchambuzi wa hali wa ukusanyaji wa maduhuli kufikia Februari 2022; katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 Wizara ilijiwekea malengo yakukusanya maduhuli kiasi cha shilingi milioni 20.3; hadi kufikia Februari 2022 Kamati ilibaini kwamba zilikusanywa Shilingi bilioni 5.6 sawa na asilimia 28 ya lengo kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba mbili. Kamati inashauri wizara iendeleze kasi ya ukusanyaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa hali ya upatikanaji wa fedha kufikia Februari 2022 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Nishati iliidhinishiwa shilingi 2,385,980,809,000 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 27.2...

**SPIKA:** Mwenyekiti ngoja ngoja.

Mwenyekiti tusomee hapa trilioni mbili...

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 Wizara ya Nishati iliidhinishiwa shilingi 2,385,980,000,000...

**SPIKA:** Shilingi 2,385,980,809,000.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo shilingi 27,224,681,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 2,358,756,128,000 sawa na asilimia 98 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa kamati umebaini kuwa kufikia Februari 2022 Wizara imepokea shilingi trilioni 1.5 sawa na asilimia 65.7 kielelezo namba tatu na namba nne vinaonesha mchanganuo wake, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa wastani unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio kwa mwaka wa fedha 2022/2023; Kamati imebaini kuwa katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 Wizara inakadiriwa kukusanya shilingi milioni 20.39 kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba 5.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa mwaka 2022/2023; katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Nishati inakadiria kutumia jumla ya shilingi 2,905,981,513,000 kama ambavyo imewasilishwa hapa na mtoa hoja, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 29.75 au asilimia moja ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 2.9 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo; kielelezo namba 26 kinaonesha lakini naomba kielelezo hicho kihusishe na marekebisho yaliyotolewa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa bajeti ya Wizara kuna ongezeko la asilimia 13; Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, sasa nijielekeze kwenye hali ya umeme; kuongeza uzalishaji na kuboresha mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini ni moja kati ya malengo makuu nane ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2021/2022 na 2022/2023. Hata hivyo, pamoja na malengo hayo, hali ya umeme bado siyo ya kuridhisha kutokana na umeme kuwa unakatika mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, kufikia mwezi Februari, 2022, uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa gridi ya Taifa ulikuwa megawati 1,694.55 unaozalishwa kutoka vyanzo vinne kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.9. Hata hivyo mahitaji ya juu ya umeme katika mfumo wa gridi ya Taifa ni megawati 1,330.06 sawa na asilimia 78.49.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa, ziada ya umeme iliyopo ni ndogo sana kuweza kuhimili kasi ya ongezeko la mahitaji ya umeme nchini inayotokana na ongezeko la ukuaji wa shughuli za kiuchumi na changamoto zinazoweza kujitokeza kwenye mitambo ya kuzalisha na kusambazia umeme kama kuharibika kwa baadhi ya mitambo, kushuka kwa kiwango cha uzalishaji wa gesi na kushuka kwa kiwango cha maji kwenye mabwawa ya kuzalishia umeme na hivyo kulazimika kusitisha uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa kuboresha miundombinu ya kuzalisha na kusambaza umeme ili kuhakikisha changamoto ya umeme kukatika mara kwa mara inaisha.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze kwenye hali ya mafuta nchini; moja ya malengo ya Wizara ya

Nishati ni kuimarisha usambazaji na matumizi ya bidhaa za mafuta na gesi asilia nchini. Kwa upande wa mafuta, jukumu hili limeelekezwa kwa Wakala wa Uagizaji wa mafuta kwa pamoja *(PBPA)*. Majukumu mengine ya Wakala ni pamoja na kutathmini mahitaji ya mafuta nchini na kuratibu uagizaji wa mafuta hayo kwa Mfumo wa Manunuzi ya Pamoja (*Bulk Procurement System – BPS*). Vile vile Wakala umepewa jukumu la kuhakikisha mafuta yanayoletwa nchini yanakidhi mahitaji na ubora unaotakiwa. Aidha, Taasisi hii imepewa mamlaka ya kuhakikisha mafuta yananunuliwa kwa njia yenye ufanisi (*efficient procurement*) kwa manufaa ya Taifa, lakini pia kuhakikisha uhakika wa usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati kuhusiana na hali ya upatikanaji wa mafuta nchini umebaini uwepo wa akiba ya mafuta inayokidhi mahitaji ya nchi. Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2021hadi Februari, 2022, akiba ya mafuta nchini imeendelea kuwa juu ya wastani wa siku za matumizi kwa zaidi ya siku 37, ikiwa ni mara mbili ya matakwa ya Leseni ya biashara ya jumla ya mafuta inayotaka kuwa na akiba ya mafuta isiyopungua siku 15.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Februari, 2022, jumla ya tani milioni 3. 77 za mafuta ya dizeli, petroli, ndege na taa ziliingizwa kwa matumizi ya ndani ya nchi (*local*) na nchi za jirani (*transit*) kwa kipindi husika. Katika kiasi hiki cha mafuta, jumla ya tani milioni 2.06 sawa na asilimia 54.8 kilikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani, na tani milioni 1.70 sawa na asilimia 45.2 kwa ajili ya nchi za jirani. Kielelezo Na. 10 kinaonesha mchanganuo wa kiasi cha mafuta kilichoagizwa kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa *BPS* umeendelea kuaminika na nchi takriban saba ambazo ni majirani zetu kwa kuamua kuendelea kuutumia mfumo huu. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuendelea kuongezeka kwa kiwango cha mafuta yanayoagizwa na nchi hizo kupitia mfumo huu hapa nchini. Ni rai ya Kamati kuwa, kama nchi tusiruhusu jambo lolote liuvuruge mfumo huu kwani kuvurugika kwake kunaweza kusababisha mafuta haya kuondoka kwenye mfumo wetu na hivyo kupoteza faida za kiuchumi tunazopata kutokana na mafuta haya kupitia nchini. Pili ikumbukwe kuwa, uwepo wa mafuta haya kwenye hifadhi za nchi yetu kunatuhakikishia uhakika wa kuwepo kwa mafuta ya kutosha nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na akiba hiyo, lakini bei ya mafuta imeendelea kupanda hali ambayo imekuwa ni mzigo kwa wananchi kutokana na ukweli kuwa upandaji wa bei ya mafuta umekuwa ukichochea kupanda kwa maisha kutokana na bei za bidhaa na utoaji wa huduma kupanda.

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake wa kutoa Shilingi Bilioni 100 kwa ajili ya kupunguza makali ya bei ya mafuta nchini kwa mwezi Juni, 2022. Sambamba na hatua hiyo, ni imani ya Kamati kuwa, ahadi ya Serikali ya kuja na hatua za kikodi kwenye bajeti kuu inayotarajiwa kuwasilishwa Bungeni siku chache zijazo nayo itasaidia kuleta nafuu kweye bei ya mafuta kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizi ambazo zinalenga kupata utatuzi wa tatizo la kupanda kwa bei za mafuta katika kipindi cha muda mfupi na muda wa kati,

Kamati inaishauri Serikali kuufanyia kazi ushauri ilioutoa wakati wa kuwasilisha Taarifa ya Mwaka mwezi Februari, 2022.

Mheshimiwa Spika, sasa nijielekeze kwenye maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati; baada ya kupita na kufanya uchambuzi wa maeneo yote tunapojielekeza kwenye eneo la Wakala wa Umeme Vijiji ni maoni ya Kamati kuwa:-

(a) Kwa mujibu wa utekelezaji wa *REA,* awamu ya tatu, mzunguko wa pili, miradi hiyo inapaswa kukamilika Disemba 2022, Kamati inashauri Wizara/*REA* ihakikishe kuwa miradi hii yote inakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa;

(b) Ili miradi ya *REA* iwe na tija katika jamii, ipo haja ya kuwepo na usimamizi wa kutosha utakaohakikisha utekelezaji wa miradi unazingatia wigo (*scope*) na *REA* iwe inafanya ukaguzi kazi hizo;

(c) Kuongezeka kwa wigo (*scope*) baada ya usanifu wa awali imekuwa ni changamoto ya muda mrefu. Ili kuondokana na changamoto hii, usanifu wa awali uwe shirikishi kwa kuhusisha viongozi wa maeneo husika kuhakiki wigo unaopendekezwa kabla ya kuingia mikataba na wakandarasi; na

(d) Kwa miradi ya *REA,* awamu ya tatu, mzunguko wa pili, Serikali ione umuhimu wa kuongeza wigo wa mradi kutoka kilomita moja ya sasa hadi kilomita mbili ili wananchi wengi waweze kuunganishwa na huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, maoni kuhusu Shirika la Ugavi la Umeme - *TANESCO*:-

(a) Ili kuhakikisha nchi inaondokana na changamoto ya kukatikakatika kwa umeme mara kwa mara, Shilingi Trilioni 4.42 zinahitajika ili kuweza kukamilisha Mradi wa kuboresha Gridi ya Taifa kwa kipindi cha miaka minne. Katika Mwaka huu wa Fedha 2022/2023, *TANESCO* inaombewa Shilingi Bilioni 500 kwa ajili ya kuanza kazi ya kuboresha gridi ya Taifa. Kamati inasisitiza fedha hizi zitoke zote na kwa wakati. Aidha, utaratibu wa kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu na gridi kwa ujumla uendelee ili kuhakikisha miundombinu ya umeme inakuwa vizuri wakati wote;

(b) Wizara iisimamie *TANESCO* ili kuhakikisha kuwa miradi ya kuzalisha umeme inatekelezwa kikamilifu ili lengo la kuwa na MW 5000 ifikapo 2025 liweze kufikiwa kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa;

(c) Serikali ione namna ya kuiwezesha *TANESCO* kuilipa *TPDC* Shilingi Bilioni 512 inazodaiwa. Hii itasaidia *TPDC* kujiendesha kibiashara hususan katika biashara ya uagizaji na uuzaji mafuta na usambazaji gesi; na

(d) Serikali izisimamie Wizara na Taasisi za Umma zinazodaiwa na *TANESCO* madeni ya ankara za umeme kwa muda mrefu yenye thamani ya Shilingi Bilioni 444.59 yaweze kulipwa ili *TANESCO* iweze kutekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, maoni kuhusiana na Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere:-

(a) Kutokana na Mradi kuchelewa kukamilika, mambo yote yanayohusiana na mradi ambayo ni jukumu la Serikali utekelezaji wake ufanyike kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha Taifa haliingii katika hasara; na

(b) Miradi inayoambatana na Ujenzi wa *JNHPP* itekelezwe mapema ukiwemo Mradi wa kusafirisha umeme kutoka Rufiji kwenda Chalinze – Kinyerezi – Mkuranga kilovoti 400 ili kuwezesha umeme utakaozalishwa uweze kufika kwenye gridi na kutumika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni na mapendekezo yanayohusiana na Shirika la *TPDC*:-

(a) Tangu kuanzishwa kwa Mfuko wa Mafuta na Gesi jumla ya Shilingi Bilioni 295.55 zimeweza kukusanywa. Hata hivyo, licha ya *TPDC* kuwa na uhitaji mkubwa wa kuwezeshwa kimtaji, imeshindwa kutumia fedha hizi kutokana na matakwa ya Sheria kutaka fedha hizi zianze kutumika baada ya kufikia asilimia 0.3 ya pato la Taifa *(GDP)*. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kufanya mapitia ya sheria husika kuruhusu mapato yatokanayo na gasi ikibidi yaanze kutumika kabala hayajafikia asilimia 0.3 *GDP* uamuzi huu utaiwezesha *TPDC* kuwekeza katika biashara ya mafuta kwa kuwa imeonekana dhahiri kuwa kwa kiasi kidogo ambacho *TPDC* imeweza kushiriki imeweza kuongeza mapato makubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Eneo lingine ni Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa pamoja *PBPA*;

(a) Kwa kuwa uagizaji wa mafuta kwa kiasi kikubwa unasaidia kupunguza gharama, ni vyema sasa ujenzi wa hifadhi kubwa ya kutosha ya mafuta uanze ili kuondokana na changamoto ya kuagiza mafuta mara kwa mara;

(b) Kwa kuwa gharama ya uchelewaji wa meli katika kupakua mafuta zinachangia katika ongezeko la bei ya mafuta kwa watumiaji wa mwisho, ipo haja kwa taasisi zinazosababisha uwepo wa ucheleweshaji wa meli kubeka gharama hizo badala ya kubebeshwa mtumiaji wa mwisho;

(c) Serikali iweke mikakati ya muda mfupi na muda mrefu kuboresha miundombinu ya kupokea mafuta Bandari ya Dar es Salaam ili iweze kukidhi mahitaji ya kupunguza gharama za mafuta nchini;

(d) Kwa kipindi cha mpito wakati Serikali ikijipanga kujenga sehemu moja ya kupokelea shehena ya mafuta ghala la kuhifadhi mafuta la *TIPER* lianze kutumika ili kuondoa tatizo la meli kusubiri kwa muda mrefu kuingia bandarini na kupunguza gharama za ucheleweshaji wa meli; na

(e) Kwa kuwa Mfumo wa *BPS* umeweza kulihakikishia Taifa usalama wa upatikanaji wa mafuta katika kipindi hiki ambacho bei za mafuta duniani zimekuwa zikipanda kila baada ya kipindi kifupi. Ipo haja

kwa Serikali kuhakikisha inakuwa makini katika maamuzi ya kupata njia bora za kuleta mafuta nchini. Uamuzi wowote lazima utuhakikishie upatikanaji wa mafuta kwa uhakika wakati wote.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uwekezaji unaotarajiwa kufanyika nchini kupitia mradi wa kuchakata *gas* asilia *LNG* ni mkubwa sana kwa manufaa makubwa kwa uchumi wa nchi yetu Serikali ione umuhimu wa kuharakisha mazungumzo yanayoendelea sasa ili uwekezaji na utekelezaji wa mradi huu uweze kufanyika kwa haraka ili Taifa liweze kunufaika na rasilimali ya gesi tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni eneo linalohusiana na Kampuni ya Uendelezaji wa Joto Ardhi Tanzania:-

Mheshimiwa Spika, sheria ya sasa inatambua rasilimali ya joto ardhi kuwa ni madini. Hata hivyo, matumizi makubwa ya joto ardhi ni katika umeme. Mkanganyiko huu unasababisha wawekezaji kushindwa kuja kuwekeza nchini. Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali ione umuhimu wa kuleta Sheria itakayowezesha rasilimali ya joto ardhi kujulikana kama nishati ili kusaidia kupata uwekezaji wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho; napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, kwa kuliongoza Bunge hili kwa weledi mkubwa. Aidha, Tunamshukuru sana Naibu Spika Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliendesha Bunge letu vizuri. Tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yenu.

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa kushiriki vizuri katika Shughuli za Kamati na kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiutoa wakati wote kuhakikisha shughuli za Kamati zinaenda vizuri. Zaidi nawashukuru kwa kuhakikisha kwamba wamekuwa wanachambua kikamilifu Bajeti ya Wizara hii na kuandaa Taarifa hii ya Kamati. Kwa heshima kubwa naomba majina yao yote yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Januari Yusuf Makamba; Naibu Waziri, Mheshimiwa Stephen Byabato; pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Mramba kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiutoa kwa Kamati wakati wote.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuendelea kutuhudumia vizuri. Kipekee namshukuru sana Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc;* Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge - Ndugu Athuman Hussein; Kaimu Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu, Ndugu Dickson Bisile; pamoja na Makatibu wa Kamati Ndugu Pamela Pallangyo, Ndugu Onesmo Laulau, Ndugu Hosiana John na Msaidizi wa Kamati Ndugu Rukia Shaban

kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii ya Kamati inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati Fungu 58, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NISHATI (FUNGU 58) KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

***[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020]***

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati (Fungu 58) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 123 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo:-

a) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi na inaeleza kuhusu Msingi na Muundo wa Taarifa;

b) Sehemu ya Pili inaeleza kuhusu uchambuzi wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

c) Sehemu ya Tatu inaeleza kuhusu Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati; na

d) Sehemu ya Nne ni Hitimisho la Taarifa.

## 1.1 Msingi na Muundo wa uchambuzi wa Bajeti

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Fasili ya 6(9) (a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2022,[1] Kamati ya Nishati na Madini ina wajibu wa kusimamia majukumu yanayotekelezwa na Wizara ya Nishati. Aidha, kwa mujibu wa fasili ya 7(1)(a) ya nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, Kamati ya Nishati na Madini kama zilivyo Kamati nyingine za Kisekta inawajibu wa kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia ikiwemo bajeti ya Wizara ya Nishati (Fungu 58).

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020, Kamati ya Nishati na Madini ina wajibu wa kuchambua Taarifa za utekelezaji wa Bajeti inazozisimamia ikiwemo Wizara ya Nishati ambapo

---

[1] Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020

ilichambua bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha ulioisha wa 2021/2022 na kufanya ulinganisho kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaofuata wa 2022/2023.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022, UZINGATIAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

### 2.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Nishati. Ziara hii ilifanyika katika Mkoa wa Dar Es Salaam na Pwani, ambapo jumla ya miradi mitatu (3) ilikaguliwa. Lengo la ukaguzi kwa mujibu wa Kanuni lilikuwa ni kuona hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na kubaini mafanikio na changamoto zilizojitokeza ili kuweza kuishauri Serikali ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Miradi iliyokaguliwa na Kamati ni kama ifuatavyo;

a) Mradi wa upanuzi wa kituo cha kuzalisha umeme cha Kinyerezi I - *Kinyerezi I Extension* MW 185 (Namba ya Mradi 3164);

b) Miradi ya REA 3 Mzunguko wa II Mkoa wa Pwani, Wilaya ya Mkuranga (Namba ya Mradi 3113); na

c) Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere (*Julius Nyerere Hydro Power Project* 2,115 MW (Namba ya Mradi 3272)

## 2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

### a) Mradi wa upanuzi wa Kituo cha kuzalisha umeme cha Kinyerezi I - *Kinyerezi I Extension MW 185*) (Namba ya Mradi 3164)

**Mheshimiwa Spika,** Mnamo tarehe 14 Machi 2022, Kamati ilitembelea Mradi wa Upanuzi wa Kituo cha kuzalisha umeme cha Kinyerezi I (*Kinyerezi I Extension)* wa kuzalisha MW185. Mradi huu unahusisha usimikaji wa mitambo minne (4) ya kuzalisha umeme kwa kutumia Gesi (*gas turbines*) iliyotengenezwa na Kampuni ya *General Electric* (GE) kutoka nchini Marekani, vipoza hewa (*chillers*) sita (6) pamoja na viambata vyake; na tayari vifaa vyote vimeshafika eneo la mradi.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi ulianza kutekelezwa rasmi Novemba 2016 na Mkandarasi *Jacobsen Elektro* AS kutoka Norway kwa gharama ya **Dola za Marekani Milioni 188** sawa na **Shilingi Bilioni 435.48** ambazo ni fedha za ndani. Hata hivyo, kufikia Mei 2018 Mkandarasi Jacobsen Elektro AS alifilisika na hivyo kushindwa kuendelea na utekelezaji wa mradi. Kwa wakati huo, mradi ukiwa umefikia **asilimia 84**. Kufuatia hali hivyo mnamo, Tarehe 29 Novemba 2021 TANESCO iliingia Mkataba na Mkandarasi mpya *CSI Energy Group* Tanzania Limited ili kumalizia kazi zilizobaki kwa gharama ya **Dola za Marekani Milioni 52.**

Kazi za kumalizia ufungaji wa mitambo ulianza rasmi tarehe 5 Januari 2022 na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2022 na njia ya kusafirisha umeme kutoka Kinyerezi mpaka Gongo la mboto Novemba 2022[2].

**Mheshimiwa Spika**, wakati Kamati inatembelea mradi huu, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 86** na tayari **Dola za Marekani Milioni 133** zimeshalipwa. Inatarajiwa kufikia mwezi Agosti 2022, mitambo yote minne ya kuzalisha umeme tayari itakuwa imewashwa.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 mradi huu uliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 88,580,000,000.00**. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 hakuna fedha iliyokuwa imetolewa na hivyo kuathiri utekelezaji wa mradi huu kwa wakati. **Kamati inasisitiza kuwa ni muhimu mradi huu ukamilike kwa wakati ifikapo Agosti 2022 hii itasaidia kuongeza umeme kwenye Gridi ya Taifa; hasa ikizingatiwa kuwa kwa mujibu wa taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, kuna viashiria wa kuwepo kwa upungufu wa mvua unaotokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi hali ambayo inaweza kuleta upungufu wa maji kwenye mabwawa ya kuzalishia umeme.**

**b) Miradi ya REA Awamu ya 3 Mzunguko wa II Mkoa wa Pwani, Wilaya ya Mkuranga (Namba ya Mradi 3113)**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 15 Machi 2022 Kamati ilitembelea Miradi ya REA awamu ya 3 Mzunguko wa II katika Mkoa wa Pwani, Wilaya ya Mkuranga. Mradi

[2] Taarifa ya TANESCO kuhusu Utekelezaji wa Mradi wa kufua umeme wa Kinyerezi 1- Extension hadi kufikia tarehe 14 machi, 2022

unahusisha kusambaza umeme katika vijiji 43; ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 179; ujenzi wa njia za umeme wa msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 43; ufungwaji wa mashine umba 43 pamoja na uunganishaji wa jumla ya wateja wa awali 924. Mradi huu unatekelezwa na mkandarasi *China Railway Construction Electrification Bureau Group* (CRCEBG) na unatarajiwa kukamilika mwezi Disemba 2022.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla miradi ya REA nchi nzima iliidhinishiwa na Bunge Jumla ya **Shilingi 363,108,000,000.00.** Kufikia Machi 2022 **Shilingi 214,555,996,055.57** sawa na **asilimia 59** zilikuwa zimepokelewa. Aidha, kwa mradi huu wa Wilaya ya Mkuranga unaogharimu **Shilingi 8,181,637,998.34** (pamoja na ongezeko la VAT) Kamati ilifahamishwa kuwa, tayari kiasi cha **Shilingi 1,636,327,599.67** sawa na **asilimia 20** kimekwishalipwa kwa mkandarasi[3].

**Mheshimiwa Spika,** wakati Kamati inatembelea mradi mkandarasi alikuwa ametekeleza kazi zifuatazo:-

i) Amesimamisha nguzo za njia ya msongo wa kati urefu wa kilomita 40 kati ya 179;

ii) Amesimamisha nguzo za njia ya msongo wa chini urefu wa kilomita 10 kati ya 43;

iii) Amejenga mtandao wa umeme wa njia wa msongo wa kati wenye urefu wa kilomita 10.5 kati ya 179 alizopewa kwenye mkataba;

[3] Taarifa ya REA kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya usambaji wa umeme katika maeneo ya pembezoni mwa miji, ujazilizi, awamu ya tatu mzunguko wa kwanza na awamu ya tatu mzunguko wa pili Mkoa wa Pwani kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini

iv) Amefunga mashine umba 7 kati ya 43, kilomita 8 kati ya 43 za njia za msongo mdogo alizopewa kwenye mkataba; uunganishwaji wa wateja wa awali 10 kati ya 924 aliopewa kwenye mkataba sawa na asilimia 1; na

v) Amekamilisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika vijiji saba (7) katika wilaya ya Mkuranga ambavyo ni Mponga, Mikere, Mingombe, Mamdimpera, Mamdikongo, Makumbea na Misasa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kutembelea Vijiji viwili vya Mingombe na Mikere na kujionea hatua iliyofikiwa ikiwa ni pamoja na baadhi ya nyumba kuunganishiwa umeme. **Kamati inaipongeza Serikali kwa utekelezaji mzuri wa miradi hii ambayo ni chachu ya Maendeleo**. Hata hivyo Kamati imebaini changamoto zifuatazo:-

i) Mwamko mdogo wa wananchi kuunganishiwa umeme licha ya umeme kusogezwa karibu;

ii) Gharama kubwa za Wakandarasi waliosajiliwa kufunga/kutandaza mfumo wa nyaya za umeme majumbani (*wiring) na* ukaguzi ambazo zimekuwa zikiwafanya wananchi wengi kushindwa kumudu; na

iii) Baadhi ya sehemu za huduma za jamii kutounganishiwa umeme mfano ni Shule ya Msingi Mikere.

c) **Mradi wa kuzalisha umeme wa Maji wa Julius Nyerere (*Julius Nyerere Hydro Power Project* –JNHPP MW 2115)**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa kuzalisha Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (*Julius Nyerere Hydro Power Project* – JNHPP) unatekelezwa na Serikali kupitia TANESCO na unategemewa kuzalisha umeme kiasi cha **MW 2,115** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rufiji. Jumla ya gharama za utekelezaji wa mradi ni **Shilingi Trilioni 6.5**, ambazo zote zinagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa **asilimia 100**.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, mradi huu ulitengewa na Bunge kiasi cha **Shilingi 1,435,000,000,000.00**. Hadi kufikia Januari 2022 jumla ya **Shilingi 733,890,312,190.39** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 51.14**.

**Mheshimiwa Spika**, kufikia tarehe 28 Februari, 2022 mradi ulikuwa umetimiza siku 958 tangu ujenzi uanze rasmi tarehe 15 Juni, 2019. Utekelezaji wa Mradi katika maeneo yote kwa ujumla kimkataba umefikia **asilimia 56.79** ambapo kwa wakati huo ulipaswa kuwa umefikia **asilimia 98.83;** na hivyo kuwa nyuma kwa **asilimia 42.04**. Kwa ujumla maeneo muhimu ya mradi yamefikia katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

i) Ujenzi wa Tuta Kuu la Bwawa (*Main Dam*) **asilimia 59.25** ikilinganishwa na **asilimia 98.40** ya Mpango kazi;

ii) Ujenzi wa Njia za kupeleka maji kwenye Mitambo (*Power Water Ways*)**asilimia 69.36** ikilinganishwa na **asilimia 99.93** ya Mpango kazi;

iii) Ujenzi wa Jengo la Mitambo (*Power House*) **asilimia 42.88** ikilinganishwa na **asilimia 98.65** ya Mpango kazi;

iv) Ujenzi wa Kituo cha kupokelea na kusafirisha umeme (400kV *Switch Yard*) **asilimia 71.91** ikilinganishwa na **asilimia 99.92** ya Mpango kazi;

v) Ujenzi wa Kingo za bwawa (*Saddle Dams*) **asilimia 41.34** ikilinganishwa na **asilimia 99.98** ya Mpango kazi; na

vi) Ujenzi wa daraja la kudumu *(Permanent Bridge* 250mx11m) **asilimia 91.15** ikilinganishwa na asilimia 100 ya Mpango kazi;

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ni sehemu ya Miradi ya Kimkakati na unatarajiwa kuongeza upatikanaji wa umeme nchini na kuchangia fursa ya uvuvi endelevu. Aidha, mradi utaanzisha aina mpya za vivutio vya utalii wa majini kama vile kuvinjari majini kwa boti (*boat sailing*), Michezo ya majini (*water sports),* michezo ya kuvua *(sport fishing*) na ujenzi wa mahoteli na kambi za kitalii kwenye fukwe za bwawa na ndani ya visiwa vitakavyojitokeza; na kuongeza upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya wanyama. Vilevile visiwa vitakavyotokana na bwawa vitakuwa na faida katika ekolojia ya mbuga ya Selous na hifadhi ya Nyerere kwa kutengeneza mazingira mazuri ya mazalia ya samaki na wanyama waishio majini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na faida hizo, Kamati imebaini changamoto zifuatazo:-

i) Mkandarasi kuchelewa kupata watengenezaji wa Mitambo kutokana na kampeni za kuupinga mradi zilizoendeshwa na wanaharakati wa mazingira kabla ya kuanza kwa mradi;

ii) Kuchelewa kwa manunuzi ya mitambo kutokana na kujitoa kwa Wakandarasi/watengenezaji mahiri na wazoefu wa mitambo (*Turbines & Generators)* kutokana na kampuni hizo kuhofia kufungiwa kimataifa kwa sababu za masuala ya mazingira katika eneo la Mradi lilolopo ndani ya eneo la urithi wa dunia; na

iii) Mlipuko wa Uviko 19 uliosababisha nchi nyingi duniani kuweka zuio la kusafiri na hivyo kusababisha ucheleweshaji wa kazi mbalimbali hususan pale ambapo wataalamu walipaswa kusafiri kwenda katika nchi watengenezaji wa mitambo ya Mradi (China, Uswisi, Swedeni, Uhisipania n.k) kwa ajili ya ukaguzi na uhakika wa ubora. Aidha, hata walipofanikiwa kusafiri, walilazimika kukaa karantini kwa kipindi cha hadi mwezi mmoja, hali ambayo ilizidi kuchelewesha kazi iliyowapeleka. Halikadhalika, usafirishaji wa vifaa vya Mradi kutoka nje ya nchi hasa China umekuwa na ucheleweshaji.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya changamoto hizo, Kamati iliridhishwa na hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa mradi kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo ujenzi wa Tuta Kubwa (*Main Dam*), Njia ya kuendesha mitambo (*Water Ways*), Jengo la mitambo


(*Power House*), Kituo cha kusafirisha umeme (*Switch Yard*) na Daraja la kudumu (*Permanent Bridge*). **Kamati inaendelea kusisitiza kuwa utekelezaji wa Mradi huu una umuhimu mkubwa kwa uchumi wa nchi yetu; hivyo Wizara ihakikishe inazipatia ufumbuzi kwa wakati changamoto zote zinazokwamisha utekelezaji wa Mradi huu kwa mujibu wa mpangokazi ulioridhiwa na pande zote za mkataba.**

**Tathmini ya Miradi**

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia ziara hiyo, Kamati imeona kuwa, changamoto kwa baadhi ya miradi ni upatikanaji wa fedha kwa wakati lakini pia muda wa kukamilisha miradi umekuwa mrefu kulinganisha na ilivyotarajiwa kama ilivyoonekana kwenye maelezo yaliyowasilishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kielelezo Na.1 kinaonesha hali ya upatikanaji wa fedha kwa miradi ambayo Kamati ilipata fursa ya kuitembelea ambapo kwa wastani upatikanaji wa fedha kwa miradi hiyo ni **asilimia 56.**

**Kielelezo Na. 1: Upatikanaji wa Fedha za Miradi Mitatu iliyotembelewa**




| | REA 3 Phase II - Mkuranga | Julius Nyerere HPP | Kinyerezi I - Extension | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| BAJETI | 8,181,637,998 | 1,435,000,000 | 88,580,000,00 | 1,531,761,637 |
| UPATIKANAJI | 1,636,327,600 | 856,374,151,9 | - | 858,010,479,5 |
| ASILIMIA | 20 | 60 | - | 56 |

*Chanzo: Taarifa za Miradi zilizowasilishwa mwezi Machi 2022 na Usanifu wa Kamati*

## 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia tathmini hiyo na yale ambayo yamebainika katika ziara, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo:-

a) Kwa kuwa kasi ya miradi ya usambazaji wa umeme vijijini ni kubwa lakini haiendani na kasi ya idadi ya wananchi wanaounganishiwa umeme. Kamati inasisitiza kuwa:-

i) Uhamasishaji ufanyike katika maeneo yote ambayo miradi ya REA imepita ili wananchi waweze

kuunganishiwa umeme na hivyo kuchochea maendeleo katika maeneo yao;

ii) Serikali iweke utaratibu utakaowezesha gharama za Wakandarasi wa kufunga/kutandaza mfumo wa nyaya za umeme majumbani (*wiring)* na ukaguzi ziwe nafuu na ambazo wananchi watazimudu. Ukubwa wa gharama hizi umekuwa ni kikwazo kwa wananchi kuunganishiwa umeme;

iii) REA ihakikishe maeneo yenye kutoa huduma za kijamii kama Shule, Hospitali, Nyumba za ibada zinapewa kipaumbele katika kuunganishiwa umeme.

b) REA na TANESCO wahakikishe kuwa wanatumia nguzo zinazozalishwa nchini. Aidha, suala la ubora wa nguzo hizo lizingatiwe.

c) TANESCO ihakikishe inasimamia kikamilifu utekelezaji wa Mradi wa *Kinyerezi I Extension* wa MW 185 ili ukamilike kwa wakati na hivyo kusaidia kuongeza upatikanaji wa umeme nchini.

d) Kutokana na umuhimu wa Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Julius Nyerere kwa uchumi wa Taifa:-

i) Miradi inayoambatana kama Njia ya kusafirisha Umeme, Kituo cha Kupooza Umeme na *North East Grid*, ujenzi wake uende kwa kasi na ikamilike kwa wakati ili kuweza kupokea umeme utakaozalishwa na bwawa;

ii) Wizara ihakikishe inazipatia ufumbuzi kwa wakati changamoto zote zinazokwamisha utekelezaji wa Mradi huu kwa mujibu wa mpangokazi ulioridhiwa na pande zote;

iii) Wizara/ TANESCO ziimarishe zaidi kitengo cha Habari ili jamii iweze kufahamu hatua ambayo mradi umefikia;

iv) Changamoto za wafanyakazi wa kada za chini zishughulikiwe kikamilifu;

v) Utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji vya Mto Rufiji visimamiwe ipasavyo ili visiharibiwe na kuleta athari katika mradi; na

vi) Kutokana na Mradi kuchelewa, uongezaji wa muda wa ukamilishaji uzingatie kutoongeza gharama kwa Serikali.

**2.4 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka 2021/2022**


**Mheshimiwa Spika,** Ili kuhakikisha Wizara inatekeleza majukumu yake kikamilifu na kuhakikisha kuwa rasilimali za nishati zinachangia ipasavyo katika maendeleo ya nchi kijamii na kiuchumi, Kamati ilielezwa vipaumbele mbalimbali ambavyo Wizara ilijiwekea katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Wizara imeendelea kutekeleza vipaumbele hivyo ikiwemo kutekeleza miradi ya kuongeza uzalishaji wa umeme nchini, kuimarisha mifumo ya usafirishaji wa umeme nchini, kupeleka Umeme Vijijini, Kuimarisha shughuli za utafiti wa mafuta na Gesi asilia, Kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya kutosha nchini na kuimarisha utendaji wa Taasisi zake.

## 2.5 Uchambuzi wa Hali ya Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari 2022

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ilijiwekea malengo ya kukusanya maduhuli kiasi cha **Shilingi 20,393,000.00** kutoka vyanzo vyake mbalimbali. Kufikia Februari 2022, zilikusanywa **Shilingi 5,631,934** sawa na **asilimia 28** ya lengo[4] kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 2.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makusanyo hayo ya **asilimia 28** yametokana na chanzo kikuu cha makusanyo ambacho ni marejesho ya fedha za umma zitokanazo na masurufu (*imprest)* ambayo Watumishi hupewa na kufanya marejesho, hivyo basi makusanyo ya maduhuli yalitegemea marejesho hayo kwa kipindi hicho.

**Kielelezo Na. 2: Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari 2022**




*Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara ya Machi 2022 na Usanifu wa Kamati*

[4] Taarifa ya Wizara yaNishati kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa kipindi cha Mwaka 2021/22: Bajeti ya Makusanyo na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2021/22

## 2.6 Uchambuzi wa Hali ya upatikanaji wa Fedha kufikia Februari 2022


**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Wizara ya Nishati (**Fungu 58**)iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,385,980,809,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 27,224,681,000** sawa na **asilimia 1.14** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **2,358,756,128,000.00** sawa na **asilimia 98.86** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 12,198,860,000** sawa na **asilimia 44.8** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake na **Shilingi 15,025,821,000** sawa na **asilimia 55.2** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo, **Shilingi 2,178,756,128,000** sawa na **asilimia 92.4** ni fedha za ndani na **Shilingi 180,000,000,000** sawa na **asilimia 7.6** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kufikia Februari 2022, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 1,568,807,565,300.84** sawa na **asilimia 65.7** ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge.[5] Kati ya fedha zilizopokelewa **Shilingi 9,822,078,555.90** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) ambayo ni sawa na **asilimia 65** ya bajeti iliyoidhinishwa na **Shilingi 8,592,870,103.37** ni Mishahara sawa na **asilimia 70.4** ya bajeti iliyoidhinishwa kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.3. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa wastani unaotakiwa.**

[5] Taarifa ya Wizara ya Nishati kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa kipindi cha Mwaka 2021/22: Bajeti ya Makusanyo na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2021/22

**Kielelezo Na. 3: Upatikanaji wa Fedha Matumizi ya Kawaida**




*Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara Machi 2022 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 1,550,392,616,642** sawa na **asilimia 66** ya bajeti iliyoidhinishwa**.** Fedha zilizopokelewa zote ni fedha za ndani ambazo pia ni sawa na **asilimia 71** ya **Shilingi 2,178,756,128,000** zilizoidhinishwa na Bunge. Hakuna fedha yoyote iliyopokelewa kutoka nje kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.4.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihoji Wizara kuhusu matarajio ya kupata fedha za Miradi ya Maendeleo kutoka nje; na ilielezwa kuwa kwa utaratibu uliopo, fedha za nje za Miradi ya Maendeleo (DFUND) huwa zinakuja katika mfumo wa vifaa ambavyo hesabu zake huingizwa katika vitabu mwisho wa mwaka. Hivyo Wizara itaziweka hesabu hizo kwa kadri ya upatikanaji wa vifaa ifikapo mwisho wa Mwaka wa Fedha.

**Kielelezo Na. 4 Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo kufikia Februari 2022**




*Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara Machi 2022 na Usanifu wa Kamati*

## 2.7 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Katika Taarifa ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara ya Nishati (**Fungu 58)** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepokea Taarifa ya utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo hayo ya Kamati na kubaini kuwa, utekelezaji unaridhisha na kwa baadhi ya maeneo Wizara inaendelea kutekeleza ushauri huo wa Kamati kwa kuwa utekelezaji wake ni endelevu. Masuala ambayo utekelezaji wake unaendelea ni pamoja na usambazaji wa Gesi asilia majumbani na Gesi ya LPG kupatikana nchini kwa mfumo wenye tija kwa

watumiaji na Taifa kwa ujumla. Kamati itaendelea kuyasisitiza masuala haya katika Taarifa hii.

## 2.8 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023. Katika Uchambuzi huo, Kamati ilijikita katika maeneo yafuatayo:-

### 2.8.1 Uchambuzi wa Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Nishati (Fungu 58) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati imebaini kuwa, malengo na vipaumbele vya Wizara vimezingatia masuala mbalimbali. Masuala yaliyozingatiwa ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III) 2021/22 – 2025/26,[6] Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020[7], Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030 n.k. Malengo ambayo Wizara imepanga kuyatekeleza ni :-

a) Kuongeza uzalishaji na kuboresha mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme;

---

[6] Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano2021/22 - 2025/26, Uk 83-84

[7] Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 Uk 103- 105

b) Kuongeza mchango wa nishati jadidifu na mbadala katika matumizi mbalimbali ya nishati;

c) Kuimarisha na kuendeleza matumizi bora ya nishati;

d) Kuimarisha uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za mafuta na Gesi asilia;

e) Kuimarisha usambazaji na matumizi ya bidhaa za mafuta na Gesi asilia;

f) Kuimarisha utoaji huduma kwa wadau wa Sekta ya Nishati;

g) Kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Kuzuia Rushwa; na

h) Kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI sehemu za kazi na kuboresha utoaji wa huduma kwa waathirika.

### 2.8.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 20,393,000.00** kama zinavyoonekana kwenye Kielelezo Na.5. itakumbukwa kuwa, awali Wizara ilikuwa inakusanya mapato yatokanayo na shughuli za mafuta na Gesi asilia hususan yaliyokuwa yakitokana na Mkondo wa Juu (*Upstream Exploration Activities*), lakini kuanzia

mwaka 2021/22 mapato hayo ambayo huhifadhiwa katika Mfuko wa Gesi (*Natural Gas Revenue Funds*) uliopo Hazina, yameondolewa kutoka Wizarani na hivyo yanakusanywa na TPDC na kuwasilishwa katika Mfuko huo moja kwa moja.

**Kielelezo Na. 5: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli 2022/2023**

| KASMA | CHANZO | MAKADIRIO |
|---|---|---|
| **A: MAKADIRIO KUTOKANA NA SHUGHULI ZA MAFUTA NA GESI ASILIA** | | |
| **14220164** | Stakabadhi Nyinginezo | 1,000 |
| **B: SHUGHULI ZA UTAWALA** | | |
| **14220161** | Stakabadhi Nyinginezo | 1,000 |
| **14220211** | Recovery of Public Money | 20,391,000 |
| **JUMLA** | | **20,393,000** |


*Chanzo: Randama ya Wizara Machi 2022 na Usanifu wa Kamati*

### 2.8.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Nishati (Fungu 58) inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 2,705,981,533,000.00.** Kati ya Fedha hizo**, Shilingi 29,751,957,000.00** sawa na **asilimia 1.1** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara na **Shilingi 2,678,229,576,000.00** sawa na **asilimia 98.9** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, Mishahara inaombewa **Shilingi 14,726,136,000.00** sawa na **asilimia 49.5** na Matumizi Mengineyo (OC) **Shilingi 15,025,821,000.00** sawa na **asilimia 50.5.** Aidha, kwa upande wa fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo**, Shilingi 2,508,756,128,000.00** sawa na **asilimia 93.7** ni fedha za ndani na **Shilingi 167,473,448,000.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla mgawanyo wa fedha hizo kwa kila matumizi ni kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 6.**

**Kielelezo Na. 6: Mchanganuo wa Bajeti kwa Mwaka 2022/2023**




*Chanzo: Randama ya Wizara ya Machi 2022 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ulinganisho wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2021/2022 na 2022/2023 kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020 na kubaini kuwa, Bajeti ya Wizara imeongezeka kwa **Shilingi 320,000,724,000.00** kutoka **Shilingi 2,385,980,809,000.00** Mwaka 2021/2022 hadi kufikia **Shilingi 2,705,981,533,00.00** sawa na ongezeko la **asilimia 13.** Ongezeko zaidi linaonekana katika fedha za Mishahara kwa **asilimia 21** na Miradi ya Maendeleo hususan fedha za ndani kwa **asilimia 15.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini ongezeko hilo linatokana na sababu mbalimbali kama vile:-

i) Mishahara: Kutoka na mpango wa Serikali wa kuwapandisha vyeo baadhi ya Watumishi na kutoa ajira mpya; na

ii) Miradi ya Maendeleo: Kutokana na miradi mipya ukiwemo wa kV 400 Rufiji – Chalinze pamoja na mradi wa kuimarisha mfumo wa gridi na usambazaji (*grid stability*).

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na ongezeko hilo, Kamati imebaini kuwa, fedha za Maendeleo kutoka nje zimepungua kwa **asilimia 7** kutoka **Shilingi 180,000,000,000.00** Mwaka 2021/2022 hadi kufikia **Shilingi 167,473,448,000.00** Mwaka 2022/2023. Uchambuzi wa Kamati umebaini kupungua huko ni kutokana na Serikali kuendelea kujitegemea katika fedha za kutekeleza miradi yake. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza bajeti yake ya ndani kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo kama ambavyo tumeona asilimia**

**98.9 ya bajeti ya Wizara hii inaenda kutekeleza Miradi ya Maendeleo.**

**Kielelezo Na. 7: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2021/2022 na 2022/2023**

| FEDHA | CHANZO | 2021/2022 | 2022/2023 | ONGEZEKO/ UPUNGUFU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | OC | 15,025,821,000 | 15,025,821,000 | 0 | 0 |
| | MISHAHARA | 12,198,860,000 | 14,726,136,000 | 2,527,276,000 | **21** |
| **Jumla Ndogo** | | **27,224,681,000** | **29,751,957,000** | **2,527,276,000** | **9** |
| **MAENDELEO** | NDANI | 2,178,756,128,000 | 2,508,756,128,000 | 330,000,000,000 | **15** |
| | NJE | 180,000,000,000 | 167,473,448,000 | (12,526,552,000) | **( 7)** |
| **Jumla Ndogo** | | **2,358,756,128,000** | **2,676,229,576,000** | **317,473,448,000** | **13** |
| **JUMLA KUU** | | **2,385,980,809,000** | **2,705,981,533,000** | **320,000,724,000** | **13.4** |

*Chanzo: Randama ya Wizara ya Machi 2022 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa kulinganisha Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa kati ya Mwaka 2021/2022 na 2022/2023 ili kuona ni kwa kiasi gani Wizara hii inapewa umuhimu kulingana na

majukumu yake kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.8. Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini yafuatayo:-

a) Bajeti ya Wizara imeongezeka kutoka **asilimia 6.28** kufikia **asilimia 6.59.**

b) Bajeti ya Maendeleo ndani imeongezeka kutoka **asilimia 20.32** kufikia **asilimia 20.70**

c) Bajeti ya Maendeleo nje imeongezeka kutoka **asilimia 4.23** kufikia **asilimia 4.93**

d) Bajeti ya Matumizi Mengineyo imeshuka kutoka **asilimia 0.36** kufikia **asilimia 0.33.**

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa, fedha hizi zitoke zote kwa wakati ili kuwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake na Miradi ya Maendeleo iliyopangwa.**

**Kielelezo Na. 8: Ulinganisho wa Bajeti (Fungu 58) dhidi ya Bajeti ya Taifa**

| **2021/2022** | | | |
|---|---|---|---|
| **AINA** | **BAJETI TAIFA** | **FUNGU 58** | **ASILIMIA** |
| OC | 4,189,190,000,000 | 15,025,821,000 | 0.36 |
| MISHAHARA | 8,155,090,000,000 | 12,198,860,000 | 0.15 |
| MAENDELEO NDANI | 10,722,989,000,000 | 2,178,756,128,000 | 20.32 |
| MAENDELEO | | | 4.23 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| NJE | 4,254,626,000,000 | 180,000,000,000 | |
| DENI LA SERIKALI | 10,663,278,000,000 | - | - |
| **JUMLA** | **37,985,173,000,000** | **2,385,980,809,000** | **6.28** |
| | **2022/2023** | | |
| **AINA** | **BAJETI TAIFA** | **FUNGU 58** | **ASILIMIA** |
| OC | 4,493,500,000,000 | 15,025,821,000 | 0.33 |
| MISHAHARA | 9,740,800,000,000 | 14,726,136,000 | 0.15 |
| MAENDELEO NDANI | 12,122,100,000,000 | 2,508,756,128,000 | 20.70 |
| MAENDELEO NJE | 3,399,200,000,000 | 167,473,448,000 | 4.93 |
| DENI LA SERIKALI | 11,308,400,000,000 | - | - |
| **JUMLA** | **41,064,000,000,000** | **2,705,981,533,000** | **6.59** |

*Chanzo: Taarifa ya Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/2023, Randama ya Wizara ya Nishati 2022/2023 na usanifu wa Kamati*

## 2.9 Hali ya Umeme

**Mheshimiwa Spika**, kuongeza uzalishaji na kuboresha mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini ni moja kati ya malengo makuu 8 ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2021/2022 na 2022/2023. Hata hivyo, pamoja na malengo hayo, hali ya umeme bado siyo ya kuridhisha kutokana na umeme kuwa unakatika mara kwa mara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kufikia mwezi Februari, 2022 uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa ulikuwa MW 1,694.55 unaozalishwa kutoka vyanzo vinne kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.9.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba uzalishaji wa umeme ambao umeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa ni **MW 1, 69455** na mahitaji ya juu ya umeme katika mfumo wa gridi ya Taifa ni **MW 1,330.06** sawa na **asilimia 78.49**. Nidhahiri kuwa, ziada ya umeme iliyopo ni ndogo sana kuweza kuhimili kasi ya ongezeko la mahitaji ya umeme nchini. Kasi ambayo inatokana na ongezeko la kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi; na changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza kwenye mitambo ya kuzalisha na kusambazia umeme. Changamoto hizo ni pamoja na kuharibika kwa baadhi ya mitambo, kushuka kwa kiwango cha uzalishaji wa Gesi, na kushuka kwa kiwango cha maji kwenye mabwawa ya kuzalishia umeme na hivyo kulazimika kusitisha uzalishaji wa umeme. Ni kutokana na kuwepo kwa mazingira haya tunajikuta kwenye mazingira ya kuwa na umeme usio wa uhakika ambao unakatika mara kwa mara.

**Mheshimiwa Spika,** umeme unapokuwa wa uhakika manufaa ni makubwa kiuchumi. Kwa mujibu wa Maandiko ya *Energy and Economic Growth, State-of-Knowledge Paper Series* na hususan katika andiko lao Na.1.1 linaloitwa ***The Impact of Electricity on Economic Development: A Macroeconomic Perspective*** lililotolewa tarehe 8 Disemba 2017 inaonesha kuwa, nchi ya Vietnam ni mojawapo nchi zenye kuonesha mafanikio zaidi kutokana na kuongezeka kwa usambazaji wa umeme wa uhakika. Kufuatia Programu ya kusambaza umeme kutoka chini ya **asilimia 5** katika miaka ya 1970 (IEA, 2011) hadi **asilimia 98** Mwaka 2014, nchi hiyo imepata maendeleo makubwa, ikiwemo kupunguza umaskini uliokithiri kutoka karibu nusu ya wananchi wake mwaka 1990 hadi kufikia **asilimia 3** tu Mwaka 2014. (Benki ya Dunia, 2016).[8]

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, madhara ya kiuchumi yanayotokana na umeme kukatika ni makubwa. Kwa mujibu wa Jarida liitwalo *Review of Middle East Economics and Finance kuhusu "The Effects of Power Outages on the Performance of Manufacturing Firms in the Middle East and North Africa Region"* imeonesha kuwa, kukatika kwa umeme kwa ujumla kuna athari za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa utendaji wa jumla wa makampuni ikiwemo kusababisha ongezeko la gharama za kiuchumi, kupungua kwa kiasi kinachozalishwa, na hatimaye kupungua kwa mauzo na tija (Arnold, Mattoo, na Narciso 2008; Fattouh na El-Katiri 2013; Fisher -Vanden, Mansur, and Wang 2015)[9].


---

[8] https://escholarship.org/uc/item/7jb0015q

[9] https://www.degruyter.com/document/doi/10.1515/rmeef-2020-0011/html?lang=en#j_rmeef-2020

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa kuboresha miundombinu ya kuzalisha na kusambaza umeme ili kuhakikisha changamoto ya umeme kukatika mara kwa mara inaisha. Halikadhalika, ipo haja ya kuongeza kasi ya kukamilisha miradi ya kuzalisha umeme ambayo inaendelea nchini kwa sasa.

**Kielelezo Na. 9: Hali ya Upatikanaji wa Umeme**




*Chanzo: Randama ya Wizara ya Machi 2022 na Usanifu wa Kamati*

## 2.10 Hali ya Mafuta Nchini

**Mheshimiwa Spika,** moja ya malengo ya Wizara ya Nishati ni kuimarisha usambazaji na matumizi ya bidhaa za mafuta na Gesi asilia nchini. Kwa upande wa mafuta, jukumu hili limeelekezwa kwa Wakala wa Uagizaji wa mafuta kwa pamoja (PBPA). Majukumu mengine ya Wakala ni pamoja na kutathmini mahitaji ya Mafuta nchini na kuratibu uagizaji wa Mafuta hayo kwa Mfumo wa manunuzi ya pamoja (*Bulk Procurement System* – BPS). Vile vile Wakala umepewa jukumu la kuhakikisha mafuta yanayoletwa nchini yanakidhi mahitaji na ubora unaotakiwa. Aidha, Taasisi hii imepewa Mamlaka ya kuhakikisha mafuta yananunuliwa kwa njia yenye ufanisi

(*efficient procurement*) kwa manufaa ya Taifa, lakini pia kuhakikisha uhakika wa usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini (*Security of Supply*).

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati kuhusiana na hali ya upatikanaji wa mafuta nchini umebaini uwepo wa akiba ya mafuta inayokidhi mahitaji ya nchi. Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai 2021hadi Februari 2022 akiba ya Mafuta nchini imeendelea kuwa juu ya wastani wa siku za matumizi kwa zaidi ya siku **37** ikiwa ni mara mbili ya Matakwa ya Leseni ya biashara ya jumla ya mafuta inayotaka kuwa na akiba ya mafuta isiyopungua siku **15**.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2021 hadi Februari, 2022, jumla ya **Tani 3,774,312** za mafuta ya dizeli, petroli, ndege na taa ziliingizwa kwa matumizi ya ndani ya nchi (*local*) na nchi za jirani (*transit*) kwa kipindi husika. Katika kiasi hiki cha mafuta, jumla ya **tani 2,066,565** sawa na **asilimia 54.8** kilikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani, na **tani 1,707,747** sawa na **asilimia 45.2** kwa ajili ya nchi za jirani. Kielelezo Na. 10 kinaonesha mchanganuo wa kiasi cha Mafuta kilicho agizwa kwa kipindi husika.

**Kielelezo Na. 10: Kiasi cha mafuta kilichoagizwa kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Februari 2022**

| MWEZI/AINA YA MAFUTA | DIZELI | PETROLI | MAFUTA YA NDEGE/MAFUTA YA TAA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| JULAI 2021 | 277,203 | 143,551 | 14,668 | 435,422 |
| AGOSTI 2022 | 305,269 | 201,064 | 12,403 | 518,736 |
| SEPTEMBA | | | 22,747 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2021 | 312,743 | 125,550 | | 461,040 |
| OKTOBA 2021 | 327,342 | 199,636 | 31,306 | 558,284 |
| NOVEMBA 2021 | 324,220 | 164,160 | 29,116 | 517,496 |
| DISEMBA 2021 | 332,248 | 206,253 | 25,937 | 564,438 |
| JANUARI 2022 | 334,626 | 172,574 | 19,936 | 527,136 |
| FEBRUARI 2022 | 73,760 | 108,600 | 9,400 | 191,760 |
| **JUMLA** | **2,287,411** | **1,321,388** | **165,513** | **3,774,312** |

*Chanzo: Taarifa ya PBPA ya Machi 2022*

**Mheshimiwa Spika,** Mfumo wa BPS umeendelea kuaminika na nchi takriban saba ambazo ni majirani zetu (Uganda, Rwanda, DRC Congo, Burundi, Zambia, na Malawi) kwa kuamua kuendelea kuutumia mfumo huu. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuendelea kuongezeka kwa kiwango cha mafuta yanayoagizwa na nchi hizo kupitia mfumo huu hapa nchini. **Ni rai ya Kamati kuwa, kama nchi tusiruhusu jambo lolote liuvuruge mfumo huu kwani kuvurugika kwake kunaweza kusababisha mafuta haya kuondoka kwenye mfumo wetu nchini na hivyo kupoteza faida za kiuchumi tunazopata kutokana na mafuta haya kupitia nchini. Pia ikumbukwe kuwa, uwepo wa mafuta haya kwenye hifadhi za nchi yetu kunatuhakikishia uhahika wa kuwepo kwa mafuta nchini.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na akiba hiyo, lakini bei ya mafuta imekuwa ikipanda hali ambayo imekuwa ni mzigo kwa wananchi kutokana na ukweli kuwa upandaji wa bei ya mafuta umekuwa ukichochea kupanda kwa maisha

kutokana na bei za bidhaa na utoaji wa huduma kupanda.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake wa kutoa **Shilingi Bilioni 100** kwaajili ya kupunguza makali ya bei ya mafuta nchini kwa mwezi Juni 2022. Sambamba na hatua hiyo, **ni imani ya Kamati kuwa, ahadi ya Serikali ya kuja na hatua za kikodi kwenye bajeti kuu inayotarajiwa kuwasilishwa bungeni siku chache zijazo nayo itasaidia kuleta nafuu kweye bei ya mafuta kwa wananchi.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hatua hizi ambazo zinalenga kupata utatuzi wa tatizo la kupanda kwa bei za mafuta katika kipindi cha muda mfupi na muda wa kati, **Kamati inaishauri Serikali kuufanyia kazi ushauri ilioutoa wakati wa kuwasilisha Taarifa ya Mwaka mwezi Februari, 2022.**

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia uchambuzi huo na yale yaliyoabinika, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo:-

### 3.1 Wakala wa Umeme Vijijini – REA

a) Kwa mujibu wa utekelezaji wa REA awamu ya 3 Mzunguko wa II miradi hiyo inapaswa kukamilika Disemba 2022, Kamati inashauri Wizara/ REA ihakikishe kuwa miradi hii yote inakamilika kwa wakati kama ilivyo pangwa;

b) Ili kuondokana na changamoto ya malipo ya Wakandarasi kuchelewa, Wizara ihakikishe fedha za kulipa Wakandarasi zinakuwepo ili wakimaliza kazi waweze kulipwa kwa wakati.

c) Kamati inasisitiza katika utekelezaji wa miradi ni muhimu REA ikahakikisha Taasisi za Umma na Jamii zinapewa kipaumbele katika kuunganishwa na umeme;

d) Ili miradi ya REA iwe na tija katika jamii, ipo haja ya kuwepo na usimamizi wa kutosha utakaohakikisha utekelezaji wa miradi unazingatia wigo (*scope*) na REA iwe inafanya ukaguzi;

e) Upelekaji wa Umeme katika vijiji uzingatie mahitaji halisi ya eneo husika hususan mahitaji ya transfoma uendane na hali halisi ya eneo husika;

f) Kuongezeka kwa wigo (*Scope*) baada ya usanifu wa awali imekuwa ni changamoto ya muda mrefu. Ili kuondokana na changamoto hii, usanifu wa awali uwe shirikishi kwa kuhusisha viongozi wa maeneo husika kuhakiki wigo unaopendekezwa kabla ya kuingia mikataba na wakandarasi; na

g) Kwa miradi ya REA awamu ya 3 Mzunguko wa II, Serikali ione umuhimu wa kuongeza wigo wa mradi kutoka Kilomita 1 hadi 2 ili wananchi wengi waweze kuunganishwa na huduma ya umeme.

## 3.2 Shirika la Ugavi la Umeme - TANESCO

a) Ili kuhakikisha nchi inaondokana na changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara, kiasi cha **Shilingi Trilioni 4.42** kinahitajika ili kuweza kukamilisha Mradi wa kuboresha Gridi ya Taifa kwa kipindi cha miaka minne. Katika Mwaka huu wa Fedha 2022/2023, TANESCO inaombewa **Shilingi Bilioni 400** kwa ajili ya kuanza kazi ya kuboresha gridi ya Taifa. Kamati inasisitiza fedha hizi zitoke zote na kwa wakati. Aidha, utaratibu wa kutenga fedha kwaajili ya kuboresha miundombinu na Gridi kwa ujumla uendelee ili kuhakikisha miundombinu ya umeme inakuwa vizuri wakati wote;

b) Wizara iisimamie TANESCO ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme inatekelezwa kikamilifu ili lengo la kuwa na MW 5000 ifikapo 2025 liweze kufikiwa kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa;

c) Serikali ione namna ya kuiwezesha TANESCO kuilipa TPDC **Shilingi Bilioni 512.16** inazodaiwa. Hii itasaidia TPDC kujiendesha kibiashara hususan katika biashara ya uagizaji na uuzaji mafuta, na usambazaji Gesi;

d) Serikali izisimamie Wizara na Taasisi za Umma zinazodaiwa na TANESCO madeni ya ankara za umeme kwa muda mrefu yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 444.59** yaweze kulipwa ili TANESCO iweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi; na

e) Kutokana na malalamiko ya wateja kuhusu utoaji wa huduma za TANESCO, Kamati inashauri Wizara iisimamie TANESCO kikamilifu kuhakikisha inaondoa urasimu na kutoa huduma nzuri kwa Wateja. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa wananchi wanapatiwa namba za malipo(*control numbers)* na kuunganishiwa umeme mapema iwezekanavyo.

### 3.3 Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere

a) Kutokana na Mradi kuchelewa kukamilika, mambo yote yanayohusiana na mradi ambayo ni jukumu la Serikali utekelezaji wake ufanyike kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha Taifa haliingii katika hasara;

b) Miradi inayoambatana na Ujenzi wa JNHPP itekelezwe mapema ukiwemo Mradi wa kusafirisha umeme kutoka Rufiji kwenda Chalinze – Kinyerezi – Mkuranga Kv 400 ili kuwezesha umeme utakaozalishwa uweze kufika kwenye Gridi na kutumika.

### 3.4 Shirika la Maendeleo la Petroli (TPDC)

a) Tangu kuanzishwa kwa Mfuko wa Mafuta na Gesi jumla ya **Shilingi Bilioni 295.55** zimeweza kukusanywa. Hata hivyo, licha ya TPDC kuwa na uhitaji mkubwa wa kuwezeshwa kimtaji, imeshindwa kutumia fedha hizi kutokana na matakwa ya Sheria kutaka fedha hizi zianze kutumika baada ya kufikia **asilimia 0.3** ya Pato la Taifa (GDP). Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kufanya mapitio ya Sheria ili kuruhusu mapato yatokanayo na Gesi ikibidi yaanze kutumika kabla hayajafikia asilimia 0.3 ya GDP. Uamuzi huu utaiwezesha TPDC kuwekeza katika biashara ya Mafuta kwa kuwa imeonekana dhahiri kwa kiasi kidogo ambacho TPDC imeweza kushiriki imeweza kuongeza mapato makubwa kwa Taifa;

b) Kamati inaipongeza Wizara kwa kujipanga kuanza kutumia Gesi kama nishati katika Magari yake. Kamati inaishauri Serikali kuziagiza Wizara nyingine kuanza kutumia Gesi kama nishati kwenye magari ya Wizara zao. Aidha, Wizara ya Nishati ihakikishe vituo vya kujaza Gesi viwepo maeneo mengi ili kurahisisha upatikanaji wake;

c) Kwa kuwa Serikali inamiliki hisa kwenye kampuni ya TIPER, ni vyema ikaanza kutumia ardhi hiyo kujenga matenki kwa ajili ya hifadhi ya mafuta ya TPDC;

d) Kutokana na mradi wa LNG kuhitaji wataalam wengi wenye ujuzi, Serikali ije na mkakati wa haraka wa kuandaa rasilimali watu itakayotumika kwenye Sekta ya Mafuta na Gesi nchini; na kwa kuanzia, Serikali ichukue hatua za haraka za kuwatafuta na kuwatambua vijana wote waliosomea Sekta ya Mafuta na Gesi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ili taaluma yao iweze kutumika nchini; na

e) Kwa kuwa asilimia 60 ya umeme unaozalishwa nchini unatokana na Gesi, na ili kuendelea kuwa na uhakika wa uzalishaji wa umeme hapa nchini, ipo haja kwa Wizara kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha uzalishaji wa Gesi unaongezeka na hivyo kuondoa changamoto ya uhaba wa Gesi nchini.

**3.5 Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA)**

a) Kwa kuwa uagizaji wa mafuta kwa kiasi kikubwa unasaidia kupunguza gharama, ni vyema sasa Ujenzi wa hifadhi kubwa na ya kutosha ya mafuta uanze ili kuondokana na changamoto ya kuagiza mafuta mara kwa mara;

b) Serikali iweke mikakati ya muda mfupi na mrefu ya kuboresha miundombinu ya kupokea mafuta ya Bandari ya Dar es Salaam ili iweze kukidhi mahitaji na kupunguza gharama za mafuta nchini;

c) Kwa kuwa gharama za uchelewaji wa meli katika kupakua mafuta (*Demurrage Charges)* zinachangia katika ongezeko la bei ya mafuta kwa mtumiaji wa mwisho, ipo haja kwa taasisi zinazosababisha kuwepo kwa ucheleweshaji wa meli kubeba gharama hizo badala ya kubebeshwa mtumiaji wa mwisho;

d) Kwa kipindi cha mpito wakati Serikali ikijapanga kujenga sehemu moja ya kupokelea shehena ya mafuta (*Single Receiveing Terminal*), ghala la kuhifadhi mafuta la TIPER lianze kutumika ili kuondoa tatizo la meli kusubiri kwa muda mrefu kuingia bandarini na kupunguza gharama za ucheleweshaji wa meli;

e) Serikali iharakishe kukamilisha mabadiliko ya mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja kutoka zabuni ya shehena kwa shehena (*cargo by cargo*) kwenda zabuni ya bidhaa kwa bidhaa (*product by product*) kwa lengo la kuingiza shehena kubwa zaidi kwa kila aina ya mafuta na kupata unafuu wa gharama za uletaji wa mafuta; na

f) Kamati inasisitiza sheria ziendelee kufuatwa ili pale inapotokea meli imekuja na tenki lenye mafuta machafu basi meli yote irudi ili kutoruhusu huu mchezo. Aidha, suala la kujiridhisha na uhakika wa akiba ya mafuta pia ni muhimu sana.

g) Kwa kuwa Mfumo wa BPS umeweza kulihakikishia Taifa usalama wa upatikanaji wa mafuta katika kipindi hiki ambacho bei za mafuta Duniani zimekuwa zikipanda kila baada ya kipindi kifupi. Ipo haja kwa Serikali kuhakikisha inakuwa makini katika maamuzi ya kupata njia bora za kuleta mafuta nchini. Uamuzi wowote lazima utuhakikishie upatikanaji wa mafuta kwa uhakika wakati wote.

### 3.6 Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli – PURA

a) Ili PURA iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu, Serikali ione umuhimu wa kuiwezesha kifedha;

b) Mchakato wa kunadi Vitalu vilivyowazi maeneo ya nchi kavu na baharini haujafanyika kwa miaka mingi. Ili kuweza kuvutia uwekezaji wa mitaji katika utafutaji wa mafuta na Gesi nchini, Serikali ione umuhimu wa kutangaza Vitalu hivyo. Aidha, Mipaka ya Ziwa Tanganyika ipitiwe na ipimwe ili ijulikane kwa uhakika kabla ya awamu mpya ya utangazji wa Vitalu vya Mafuta na Gesi; na

c) Kwa kuwa uwekezaji unaotarajiwa kufanyika nchini kupitia Mradi wa kuchakata Gesi asilia (LNG *Project*) ni mkubwa na wa manufaa makubwa kwa uchumi wa nchi yetu, Serikali ione umuhimu wa kuharakisha mazugumzo yanayoendelea sasa ili uwekezaji na utekelezaji wa mradi huu uweze kufanyika kwa haraka ili Taifa liweze kunufaika na rasilimali ya Gesi.

### 3.7 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)

a) EWURA iharakishe uandaaji wa Kanuni kwaajili ya Leseni za mafuta vijijini ili kuondoa changamoto zinazojitokeza;

b) Kamati inapenda kuipongeza Serikali kupitia Mhe.Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumteua Ndg. Modestus Lumato kuwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA. Aidha, Kamati bado inaisisitiza Serikali

kukamilisha taratibu zake ili watumishi ambao bado wanakaimu ngazi mbalimbali waweze kuthibitishwa ili kuweza kuleta ufanisi wa utendaji kazi wa Mamlaka; na

c) Utaratibu wa TBS wa kusafirisha sampuli za mafuta kwenda Dar es Salaam kwaajili ya upimaji kwa mafuta yanayoshushiwa bandari za Tanga na Mtwara unasababisha meli kuchelewa kupakua mafuta na hivyo kuongeza gharama. Serikali ione umuhimu wa kuiagiza TBS kuweka maabara kwenye maeneo husika ili kuepusha usumbufu na urasimu usio wa lazima.

**3.8 Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania - TGDC**

a) Joto Ardhi ni rasilimali muhimu katika uzalishaji wa Umeme. Umeme unaozalishwa kwakutumia rasilimali hii huwa na gharama ya chini sana pindi uwekezaji wa awali unapokuwa umekamilika baada ya utafiti wa kina. Kwakuwa nchi yetu inayo rasilimali hii kwa wingi, Serikali inashauriwa kuiwezesha TGDC ili iweze kutimiza majukumu yake na hatimaye kuwezesha rasilimali ya Joto Ardhi kuweza kutumika kuzalisha Umeme wa uhakika na wa bei nafuu;

b) Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii na Sekta binafsi zione namna ya kuendeleza miradi mingine inayotokana na joto ardhi kama utalii, teknolojia ya ututoleshaji wa vifaranga kwa mashine(incubators); na

c) Sheria ya sasa inatambua rasilimali ya joto ardhi kuwa ni madini. Hata hivyo, matumizi makubwa ya joto ardhi ni katika umeme. Mkanganyiko huu unasababisha wawekezaji kushindwa kuja kuwekeza. Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali ione umuhimu wa kuleta Sheria

itakayowezesha rasilimali ya Joto ardhi kujulikana kama nishatii ili kusaidia kupata uwekezaji wa kutosha.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako Spika wetu Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb) kwa kuliongoza Bunge hili kwa weledi mkubwa. Aidha, Tunamshukuru sana Naibu Spika Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb) na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliendesha Bunge letu vizuri. Tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yenu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa kushiriki vizuri katika shughuli za Kamati na kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakitoa wakati wote kuhakikisha shughuli za Kamati zinaenda vizuri. Zaidi nawashukuru kwa kuhakikisha wanachambua kikamilifu Bajeti ya Wizara hii na kuandaa Taarifa hii ya Kamati. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Alaudin Hasham Salim, Mb
4. Mhe. Amina Bakari Yussuf, Mb
5. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb
6. Mhe. Hamis Mwagao Tabasam, Mb
7. Mhe. Iddi Kassim Iddi, Mb
8. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb
9. Mhe. Jesca Jonathan Msambatavangu, Mb
10. Mhe. John Marko Sallu, Mb

11. Mhe. Juliana Didas Masaburi, Mb
12. Mhe. Katani Ahmad Katani, Mb
13. Mhe. Kenneth Ernest Nollo, Mb
14. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb
15. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb
16. Mhe. Mussa Omari Salim,Mb
17. Mhe. Musukuma Joseph Kasheku, Mb
18. Mhe. Nicodemas Henry Maganga, Mb
19. Mhe. Nusrat Shaaban Hanje, Mb
20. Mhe. Saada Mansour Hussein, Mb
21. Mhe. Robert Chacha Maboto, Mb
22. Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya, Mb
23. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb
24. Mhe. Ameir Abdallah Ameir, Mb
25. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb
26. Mhe. Mohamed Said Issa, Mb
27. Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru sana Waziri wa Nishati Mhe. Januari Y. Makamba (Mb), Naibu Waziri Mhe. Stephen L. Byabato (Mb) pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndg. Felchesm Mramba kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiutoa kwa Kamati wakati wote.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuendelea kutuhudumia vizuri. Kipekee namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi (*ndc),* Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu Ndg. Dickson Bisile pamoja na Makatibu wa Kamati Ndg. Pamela Pallangyo, Ndg. Onesmo Laulau, Ndg Hosiana John na Msaidizi wa Kamati Ndg. Rukia Shaban kwa

uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii ya Kamati inakamilika.

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati (**Fungu 58)** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Dunstan Luka Kitandula, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**

01 Juni, 2022

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula kwa kuwasilisha maoni yetu sisi kama Wabunge kwa Wizara.

Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na ratiba yetu, lakini ataingia Mwenyekiti kuendelea na ratiba iliyo mbele yetu ila tutaanza na wachangiaji ambao hawajawahi kuchangia, watafuata waliochangia mara moja, watafuata waliochangia mara mbili, mara tatu wataendelea. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na uchangiaji wetu na Mheshimiwa Shanif Mansoor Jamal, Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza na Mheshimiwa Lucy John Sabu, atajiandaa.

**MHE. SHANIF M. JAMAL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye hotuba hii ambayo ipo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri yenye matumaini kwa wananchi ambayo ameitoa hapa mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda kuchangia katika maeneo machache matatu. La kwanza, ningependa kuchangia sehemu ya umeme vijijini *REA*. *REA* ni changamoto kubwa tuliyonayo sisi wananchi wa Jimbo la Kwimba. Tuna vijiji takribani 32 tunasubiri kupata umeme. Ilani ya Chama cha Mapinduzi inatangaza kwamba umeme utafikishwa mwaka huu mwishoni lakini bado kuna changamoto, ukimfuatilia mkandarasi amemaliza vijiji vinne kupata umeme, lakini hivyo vijiji vinne ambavyo ameshavimaliza bado hajawasha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli shughuli ya umeme vijijini inaenda taratibu sana, ningeomba sana Mheshimiwa Waziri aweke nguvu ya ziada, umeme vijijini ni siasa. Ni siasa kwetu sisi huko vijijini, hivyo, tunaomba tupate umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kusema kwenye bajeti ya mwaka huu mahitaji ya kupeleka

umeme vijijini kwenye bajeti yake Mheshimiwa Waziri amesema mahitaji ni shilingi trilioni 1.24, lakini fedha alizozitenga ni bilioni 164, ni asilimia 15 tu. Nasema hizi fedha ni ndogo sana anatakiwa aongeze bidii kwa sababu maana yake tutapata umeme vijijini asilimia 15 tu kwa mwaka ujao. Ningeomba sana hizi fedha za kupeleka umeme vijijini zingeongezwa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili pia kuna changamoto wakandarasi wanasema hata Mheshimiwa Waziri alitwambia kwamba kuna changamoto, vifaa vimepanda bei, wanaboresha mikataba na wakandarasi. Naomba tupate mwelekeo wa Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake wakati anatupa majibu, atuambie wakandarasi hawa anafunga nao mkataba lini, watarekebisha lini, ili hawa wakandarasi waweze kuendelea na kazi kwa *speed* kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la *subsidy*, suala la shilingi bilioni 100 ambayo Serikali imetoa kwenye mafuta. Naomba ku-*declare interest* mimi ni mdau, nataka nipongeze Serikali kwa kazi nzuri sana ambayo imefanya ya kutoa msaada kupunguza makali ya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *subsidy* ya bilioni 100 iliyotolewa kwenye mwezi Juni ina changamoto nyingi sana ambazo imekuja nazo, wafanyabiashara wa mafuta, kuna mafuta yamekaa kwenye maghala ambayo yalishalipiwa kodi sasa hivi yale mafuta yote yaliyokwishalipiwa kodi sasa inabidi uuze kwa pungufu ya sh.300 ambayo ni *subsidy*. Kuna hasara kwenye kwa makampuni ya mafuta takribani shilingi bilioni 50 inapatikana hasara kwa makampuni ya mafuta ambayo yamekutwa na *stock* ya aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba *subsidy* nasaidia kupunguza makali lakini kuna utaratibu, sasa maana yake mafuta ni biashara ni shughuli ambayo ni nyeti sana haitaki kuingiliwa sana. Maana yake sasa mwezi wa Sita tumeingilia mwezi wa Saba hatujui kinachoondelea, kutakuwa na utofauti tena, maana yake kuna mafuta utakuwa unalipia mwezi wa Sita utavuka nayo mwezi wa Saba. Sasa mwelekeo wa mwezi wa Saba haijulikani tena itategemea kwamba Makampuni tena yatapata hasara au itatokea nini. Mimi ningeshauri wazo la Serikali kupunguza makali ni mazuri lakini iwe endelevu, maana yake ifanyike kwa miezi mitatu au miezi sita. Kila miezi itakuwa ina changamoto yake. Kwa hiyo mimi ningependa kusema kwamba hii *subsidy* ni kitu kizuri lakini wakifanye kiwe kama Sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri kwenye suala la *subsidy* kama inaendelea basi Mheshimiwa Waziri alivyosema kwenye hotuba yake kwamba ataka aanzishe *stabilization fund,* maana yake basi wangetangaza ingekuwa ni *stabilization fund*. Mfano, wangetoa fidia kwa miezi mitatu wakati mafuta yanapanda bei basi baadae wakati mafuta yakianza kushuka mwezi wa Agosti, Septemba, mafuta yakianza kushuka bei wanaanza kurudisha ile *stabilization fund* kurudisha hii fedha. Kwa hiyo, maana yake kuwe na sera na kuwe na utaratibu mzuri wa kuweka wazi kwamba hili suala litaendaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ningependa kulisema leo ni suala la *Bulk Procurement Agency*. Mimi niwapongeze, *Bulk Procurement Agency* wanafanya kazi nzuri sana, wanasimamia kuagiza mafuta kwa niaba ya Makampuni ya mafuta. Leo takribani miaka 11, *Bulk Procurement Agency* wanafanya kazi ya kuleta mafuta

ndani ya nchi. Changamoto zipo lakini pia kazi nzuri wamefanya. Hapo nyuma nilisikia mara nyingi watu wakisema kwamba hii mafuta tungevunja *Bulk Procurement* tukaanza kufanya watu wafanye mafuta ya kuleta watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi duniani ambayo inaweza ikaacha mafuta ikafanywa na wafanyabiashara peke yao, lazima Serikali iwe na mkono wake isimamie, changamoto ipo lakini tunafanya kazi vizuri. Pia lazima tufahamu kwamba *Bulk Procurement tender* zinazotangazwa ndani ya nchi yetu zinaleta mafuta kwa ajili ya nchi nyingine Sita ambazo zimetuzunguka, nchi ya Rwanda, Burundi, *DRC*, Zambia, Malawi, Uganda wanategemea mafuta yanayoletwa kwenye *Bulk Procurement*. Kwa hiyo, mimi ningeshauri Serikali wanapofanya maamuzi waangalie kwamba nchi hizi Sita pia zinategemea mafuta yanayoletwa ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo tunavyoboresha tuangalie na nchi hizi Sita ambazo zinatuzunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ningependa kulisema pia Tanzania tumetoa *subsidy* nchi zinazotuzunguka zote Sita hizi hazijatoa *subsidy*. Itafika sehemu tutaenda tutakuta nchi za jirani mafuta ni bei nafuu kuliko mafuta ya Tanzania. Kwa hiyo, lazima tuangalie tuwe tunaenda pamoja na nchi za jirani kwa sababu mafuta yote yanayoingia ndani ya nchi yetu yanaenda pia kwenye nchi ya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ningependa kulisema ni kwenye *Bulk Procurement* tunafanya *tendering* ya meli takribani Nane au Tisa kwa mwezi. Naipongeza Serikali wamewapa uwezo *TPDC* toka mwaka jana Desemba, mwaka jana Oktoba wameanza

kushiriki, naomba *TPDC* waongeze *speed* ya kushiriki, wanashiriki kwenye *tender* moja moja tu za *diesel* kwenye petroli *TPDC* hawashiriki sijui kwa nini. Mimi ningeomba sana na ningeishauri Serikali *TPDC* pia inatakiwa ishiriki kwa undani zaidi maana yake inatakiwa *TPDC* inavyoshiriki unakuta na bei zinashuka kidogo. Kwa hiyo, *TPDC* tungeomba muwape nguvu ya ziada, *TPDC* ishiriki kwenye *tender* za kila mwezi. Kuna *tender* Nane unakuta *TPDC* ana *tender* moja tu ndiyo anashiriki au mbili zingine zote anaziachia. Mimi ningeomba sana Mheshimiwa Waziri *TPDC* washiriki kwenye *tender* zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi ya kusema nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja. Naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shanif Mansoor Jamal. Tunaendelea na Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mheshimiwa Lucy John Sabu, ajiandae.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nichukue nafasi hii kukupongeza wewe lakini ninamshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia nafasi leo kuwa ni miongoni mwa wachangiaji wa Bajeti yetu hii ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipende kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi ambayo wanaifanya na ambayo inaonekana. Pili, ningependa niwapongeze watu wa *TANESCO* kwa kushughulikia lile suala ambalo mara nyingi nikilisema zaidi ya miaka miwili mitatu la kuhusu bei ya umeme ambayo wanauzia Zanzibar. Kiukweli nataka niwapongeze nichukue nafasi hii, wamefanya kama ambavyo imekuwa tumetarajia na

hatua ambazo zimefikia kiukweli imebaki kidogo lakini watu wa Zanzibar wanasema ahsante sana na wanaipongeza *TANESCO* kwa kuwasikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka niliseme ni kuhusu kukatikakatika umeme. Zanzibar kumekuwa umeme ukikatikakatika sana sijui kwa nini, kwa hivyo nafikiria *TANESCO* kwa sababu wao ndiyo *source* ya umeme Zanzibar kupatikana walichukue hili halafu waangalie waone kuna nini ambalo linasababisha, kama ni miundombinu basi tuone tunarekebisha vipi ili tatizo la kukatika kwa umeme lisiwepo lakini kwa upande wa mwanzo wa bei tunashukuru na wazanzibar wamenituma kabisa wamesema ukipata nafasi ya kuongea basi jaribu kuwaambia kwa hili tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mama. Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anai-*support* Wizara hii na miradi ambayo iko ndani ya Wizara hii. Katika Wizara hii kuna mradi mkubwa wa Bwawa la Mwalim Nyerere, Bwawa la Mwalim Nyerere ambalo limekuwa mara nyingi ni gumzo kubwa ambalo linazungumziwa hapa, kwa *stage* ambayo imefikiwa sasa hivi, kwa mtu yoyote ambaye hajawahi kwenda chini ya miezi mitatu au minne akienda sasa hivi na akakuta asilimia ambayo imefikiwa basi hawezi kuamini. Mradi unakwenda vizuri, Mama amepeleka pesa ya kutosha, mradi mpaka sasa hivi umeshafikia zaidi ya asilimia 60. Mama ameshatoa zaidi 3.8 bilioni na mpaka sasa hivi hakuna Mkandarasi ambaye anadai wala deni la fedha lolote kuhusu hili Bwawa la Mwalim Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi nawapongeza Wizara na *TANESCO* kwa kuanza kujenga

*transmission* ya kutoka Rufiji kwenda Chalinze. Vilevile na kujenga *substation* ya Chalinze. Kwa sababu Bwawa hili pamoja na kuwa tunalihitaji na linaendelea kwa kasi hata lingekuwa limeisha leo bila *transmission line* maana yake pia tusingeweza kutumia umeme huu. *TANESCO* tumeaa nao na Wizara katika Kamati tukawashauri kwa nini vitu hivi visiende pamoja na sasa hivi wamevianza kwa hivyo tuna uhakika inapofika mwisho wa mradi wa bwawa basi na *substation* ambazo zitakuwa zinagawa umeme huu zitaweza kutumika na itakuwa yale malengo ambayo tunasema tuendelee katika kuhakikisha umeme mwingi unapatikana lakini unatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na umeme ni jambo moja lakini je tutautumiaji na hatuwezi kuutumia bila kuwa na *transmission* kuutoa kule ambako uko kuuleta kwenye *substation,* kwenye *substation* ndipo ambako tutakuwa tunaugawa kwa ajili ya matumizi. Niwapongeze sana *TANESCO* na Wizara mpaka sasa hivi kwa *stage* hiyo ambayo mmeifikia. Labda mimi nitoe ushauri tu mmoja ambao ningependa niwashauri *TANESCO* mambo mengine yapo kwenye Kamati nimechangia kama Mjumbe na michango yangu mingine nimeandika kwa maandishi, ningewashauri *TANESCO* sasa hivi umefika wakati wa kutafuta vyanzo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha bajeti yake, amesema Wizara imejipanga katika kuhakikisha inakuwa na vyanzo vingine tusitegemee zaidi maji ambapo ikitokea ukame basi inakuwa hali ya taharuki kama miezi mitano, sita ambayo ilipita tuliona wenyewe ambapo mabwawa yana upungufu wa maji basi ikabidi tuingie kwenye mgao wa umeme pasi na kuwa na sababu ya kuingia kwenye hiyo. Vyanzo vingi tunavyo hapa nchini kwetu lakini Wizara

napenda ijielekeze tuhakikishe tuna vyanzo vingine nje ya maji vya kupata umeme ili inapotokeza ukame au mvua kidogo basi tuhakikishe tunayo *reserve* ambayo tunaweza tukaitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine na si kwa umuhimu sana lakini ni umuhimu ni kwa ajili ya miradi hii ya *REA* ambayo inakwenda kwenye Vijiji. Vijiji vingi *REA* imefika, lakini watu wengi ambao wako kwenye vitongoji sasa ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema kuna mpango kabambe wa kupeleka kwenye vitongoji. Mimi ningependa tungehakikisha sasa kwenye vitongoji tunapeleka umeme kwa kiwango kikubwa kwa sababu watu wengi wanasema umeme upo lakini uko Mjini, walioko ndanindani kule wanashindwa kuupata, kwa hivyo *REA* ningependa niwapongeze. Jambo jingine na si kwa umuhimu sana, nichukue nafasi hii niipongeze Wizara nzima si Waziri tu, au Naibu, au Katibu ni Wizara nzima pamoja na ma-*technician* wao, ma-*engineer* ambao wanaweza kuisaidia sana hili Shirika letu la umeme *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache niliona na mimi nitoe mchango wangu huu japo mdogo, nawashukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza. Tunaendelea na Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mheshimiwa Vuma Augustine Holle na Mheshimiwa Jonas William Mbunda ajiandae.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii nami niweze kuchangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya. Kiupekee kabisa niipongeze Wizara ya Nishati wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa January Makamba na Naibu Waziri, Mheshimiwa Stephen Byabato na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Simiyu unapata umeme kutoka katika Mikoa ya jirani Mkoa wa Shinyanga, Mwanza na Mara wenye njia za umeme zenye msongo wa *Kilovolt* 33. Changamoto kubwa tulizonazo katika Mkoa wa Simiyu ni kiujumla njia hizi zimekuwa ni ndefu sana lakini kumekuwa na changamoto ya umeme kukatika mara kwa mara. Lakini ukiangalia Maswa *Feeder* ambayo ni njia ya umeme inasambaza umeme ukitoka kuanzia Kwimba, Mwanza na una-*supply* katika Wilaya za Bariadi tano. Sasa changamoto zikitokea katika Wilaya moja zinaathiri Wilaya zingine katika Mkoa huo. Na changamoto ya pili Mkoa huu hauna *grid substation,* hali hii inasababisha viwanda ambavyo vinaendeshwa katika Mkoa huu kunakuwepo na changamoto ya umeme, umeme haujitoshelezi na viwanda vingi ukiangalia tuna viwanda vikubwa saba vya pamba na vingine nane vimekufa kwa sababu ya kutokuwa na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya kutatua changamoto hii. Wizara ilipendekeza kuwepo na *grid substation* ambayo mradi ulishazinduliwa katika Kijiji cha Imalile Wilaya ya Bariadi na Mradi huu utagharimu kiasi cha shilingi bilioni 75. Lakini nimeona katika bajeti fedha iliyotengwa ni Milioni 725 fedha hii ni ndogo sana na ukizingatia wananchi tayari wameshalipa fidia lakini

mpaka hivi sasa bado mradi haujaanza na changamoto hii imekuwa ni ya muda mrefu sana. Tunamuomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake atueleze ana mpango gani na Mkoa wa Simiyu ili tuweze kupata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine tuliyonayo katika Mkoa wa Simiyu kuna baadhi ya maeneo ya migodi ambayo hayajapelekewa umeme hadi mpakahivi sasa kwenye Wilaya ya Busega na Wilaya Bariadi. Na maeneo hayo ni kama ifuatavyo, Dutwa, Halawa, Nyawa, malamata na Bulumbaka bado yote hayajapelekewa umeme, ukizingatia migodi hii inachangia mapato ya Serikali vizuri. Kwa mfano, katika Mgodi wa Gasuma wao wanatumia zaidi ya lita 2,000 ambayo hii inaongeza gharama za uzalishaji na inasababisha wao wasiweze kuzalisha kwa kiwango cha juu. Tunaiomba Serikali iweze kupeleka umeme katika maeneo haya ili hawa wachimbaji waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye bajeti wametenga Bilioni 100 katika mradi wa kupeleka umeme katika maeneo ya wachimbaji. Nikuombe Mheshimiwa Waziri katika hiyo Bilioni 100 nasi Mkoa wa Simiyu uweze kutuona na maeneo haya ya wachimbaji yaweze kupata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Simiyu tunavyo Vijiji 470 na Vijiji vilivyopata umeme ni Vijiji 269 na Vijiji 201 havijapata umeme. Nikuombe Mheshimiwa Waziri nimekusikia unasema utapeleka umeme kwenye Vitongoji kama huku kwenye Vijiji bado hatujaweza kufanikiwa kumaliza kupeleka umeme, nikuombe uweze kuja na mpango mzuri wa kuweza kuhakikisha kwamba Vijiji vyote vinapelekewa umeme kama tulivyoahidi katika

Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ifikapo mwaka 2025 tutaweza kusambaza umeme katika Vijiji vyote na katika vitongoji vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lucy John Sabu. Tunaendelea na Mheshimiwa Vuma Augustine Holle, Mheshimiwa Jonas William Mbunda na Mheshimiwa John Marko Sallu ajiandae.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia hoja hii ya Bajeti ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipende kumpongeza Mheshimiwa Rais lakini na Waziri mwenyewe. Leo tarehe 01 Juni, waliahidi kwamba watashusha bei ya mafuta, kweli tumeona tangu jana usiku mafuta yameshuka imepunguza angalau makali ambayo yale ambayo Watanzania walikuwa wanayapata. Hongera sana Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwana nataka nizungumzie *grid* ya Taifa Mkoa wa Kigoma, ni matamanio ya wananchi wote wa Mkoa wa Kigoma kupata umeme wa uhakika kama ambavyo watanzania wengine wanapata. Kwa bahati mbaya sana hatujawahi kupata *grid* ya Taifa tangu tupate uhuru Mkoa wa Kigoma. Tumekuwa tunasema muda mrefu humu ndani na kwenye *platform* tofautitofauti lakini bado utekelezaji wake unasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nimeona kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri, kwanza nishukuru kwamba kuna mawazo hayo ya kupeleka *grid* ya Taifa lakini nimeangalia *figures* bado *is not convincing,* ina maana huu mradi wa Urambo kwenda Kigoma ambao ni Bilioni 69.7 zimetengwa Bilioni 2.0. Nimeangalia huu wa Nyakanazi kwenda Kigoma ambao ni zaidi ya dola Milioni 35 ambao ni zaidi Bilioni 80 huko lakini tumetengewa Bilioni 7.4. Chondechonde Mheshimiwa Waziri unanisikia vizuri, wewe ni Kaka yangu, unajua hilo tunaheshimiana sana. Mkoa wa Kigoma tunaomba wakati tukiwa Waziri wa Nishati tuachie zawadi, tuachie *legacy,* Kigoma itakukumbuka wewe, itamkumbuka Mama Samia katika suala la umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kusema mengi lakini mengi wewe unajua tumeshazungumza, nakuomba sana Kigoma tunataka *grid* ya Taifa, tumesubiri mno, Mikoa yote *grid* ya Taifa imeunganishwa bado Kigoma tu, kuna nini? Tunahitaji tutengewe fedha za kutosha siyo Bilioni Mbili hizi, tupewe fedha za kutosha ili miradi hii iende kwa kasi kubwa, ikamilike na wananchi waweze kupata *grid* ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *REA* nashukuru vipo Vijiji ambavyo vimepata umeme lakini yapo maeneo makubwa hasa sisi Wabunge wa Vijiji, Kasulu Vijijini, kutokana na ile jiografia ya kule umbali wa kutoka Kijiji mpaka Kijiji yako maeneo mengi ambayo umeme kwa kweli haujafika. Ziko Kata kama saba Nyamwusi, Titie, Ungwempya, Kurugongo, ahsante Nyerere, Kitanga, Herushingo, Shunguriba hizi ni Kata kabisa ambazo umeme haujafika. Ningependa kasi ya kupeleka umeme Vijijini hasa Jimbo la Kasulu Vijijini yaongezeke kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la kukatikatika kwa umeme. Kama kuna jambo ambalo limekuwa linachafua Serikali ni la kukatikatika kwa umeme, tunaweza tukafanya mambo makubwa na mazuri sana lakini lazima tudhibiti jambo hili. Na nikupongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuja na mawazo haya ya kuimarisha *grid* ya Taifa. Umekuja kuomba Bilioni 500 hapa nimeona na *Inshallah* tutakupatia lakini nenda ukasimamie vizuri suala la kukatikakatika kwa umeme linachangia, linachafua mno Serikali kuliko kawaida. Umeme ukikatika tu watu wanatukanwa mno huko chini. Lazima tujitahidi sana hizi fedha ambazo utapatiwa uende ukafanye usimamizi mzuri sina mashaka na Mheshimiwa Waziri, naamini usimamizi utakuwa mzuri na hatimae suala la kukatikakatika umeme lilikuwa ni nchi nzima lakini sasa Kigoma lilikuwa ni balaa zaidi, ili kuhakikisha kwamba tunaweza kumaliza jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka nishauri jambo moja hii shilingi bilioni 500 nadhani kuna viwanda siku hizi vya kutengeneza vifaa mbalimbali vya umeme. Ningependa sana hii fedha sehemu kubwa ya fedha hii au chochote ambacho mnataka kununua ambacho kinapatikana hapa kwetu Tanzania vinunuliwe hapa hapa ili angalau kuweza kuongeza fedha kwenye mzunguko wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu ni hayo tu naunga mkono hoja *all the best* Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vuma Augustine Holle. Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mheshimiwa John Marko Sallu na Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka wajiandae.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Nishati.

Awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, lakini pili naomba nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutekeleza miradi ya kimkakati ikiwa ni pamoja na Bwawa la Mwalimu Nyerere na miradi mingine ya kugawa umeme nchini ile miradi mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze Waziri wa Nishati na Naibu Waziri, lakini Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa namna wanavyojitahidi kusimamia Wizara hii ya Nishati. Lakini vilevile kwa jinsi walivyoiandaa randama ambayo imeeleza mambo mengi na kama yatatekelezwa itatusaidia sana kuondokana na changamoto ya umeme hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya malengo ambayo Wizara wamesema watayatekeleza ni kuhakikisha kwamba wanaimarisha miundombinu ya usambazaji wa umeme nchini. Katika bajeti ya mwaka jana tulikubaliana kwamba Wizara itatekeleza mradi wa *REA* (kusambaza umeme vijijini) ndani ya miezi 18. Sasa hivi takribani ni miezi 11 sisi ambao tunatoka katika maeneo haya mradi unatakiwa utekelezwe kwa upande wangu mimi kwa Jimbo la Mbinga Mjini mradi umetekelezwa kwa asilimia 0.3 na huu ni mwezi wa 11 tumebakiza miezi saba. Najiuliza ni miujiza gani wenzetu wataifanya kuhakikisha kwamba hii miezi saba iliyobaki tutakamilisha kutekeleza miradi hii ya *REA* katika vijiji vyote vilivyobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Jimbo la Mbinga Mjini ninavyo vijiji 23 ambavyo havijapata umeme wa *REA* na katika vijiji hivyo kuna kata moja nzima haijapata umeme, lakini katika kata hiyo kuna umeme wa Masista wa Chipole megawati saba unatoka katika eneo hilo na umegawika katika maeneo mengine, lakini hiyo kata mpaka leo haijapata umeme. Huwa inanipa shida sana ninapopita kwenye hilo eneo naulizwa inakuwaje umeme umetoka katika hili eneo, lakini wale wahusika hawajapata umeme hata kijiji kimoja.

Kwa hiyo, nimuombe Waziri atakapohitimisha taarifa yake hii anieleze kwamba ni namna gani ndani ya hii miezi saba atatekeleza kupeleka miradi katika vijiji 23 vilivyopo katika Jimbo la Mbinga Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nilikuwa nataka nichangie ni upande wa *TANESCO*. Shirika letu la *TANESCO* linafanya vizuri katika kusambaza umeme nchini, lakini changamoto iliyopo kubwa ni kukatikakatika kwa umeme katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukatika huko kwa umeme mara nyingi changamoto inayojitokeza kutokana na miundombinu mibovu. Nilikuwa nawashauri Serikali iangalie uwezekano wa kuimarisha hiyo miundombinu ili wananchi waendelee kupata umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto nyingine ya upatikanaji wa vifaa vya kusambazia umeme katika maeneo mbalimbali. Wananchi wetu wanaomba kuingiziwa umeme katika maeneo yao, lakini unakuta

inaweza ikachukua wiki mbili au mwezi mzima hata wengine miezi mitatu hawapati umeme kwa wakati na changamoto inayoonekana iliyopo ni upatikanaji wa vifaa vya kuingiza umeme katika nyumba za wananchi wetu. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali ihakikishe kwamba hii changamoto inaondoka ili wananchi wetu waweze kupata umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ambao tunaishi maeneo ya mjini na ambayo yanapanuka kwa kasi shirika letu la *TANESCO* lina changamoto kubwa ya kushindwa kusambaza umeme kwenye maeneo yale ambayo wananchi wanaendelea kujenga nyumba mbalimbali. Kwa hiyo, nilikuwa naomba na nilishauri shirika liendelee kwenda na kasi ya miji yetu jinsi inavyopanuka.

Kwa upande wa Mkoa wa Ruvuma umeme umesambazwa katika maeneo mbalimbali, lakini kuna changamoto kubwa kwamba unakuta umeme umesambazwa kutoka Songea mpaka Nyasa, lakini hakuna *auto closure* zile ambazo zinasaidia umeme ukikatika sehemu moja au ikitokea hitilafu umeme ule usikatike eneo lote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naomba *TANESCO* iangalie uwezekano wa kudhibiti hiyo changamoto ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu kama umeme unakatika eneo moja, eneo lingine liendelee kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tunaendelea kusambaza umeme katika maeneo mbalimbali lakini nilikuwa naomba *TANESCO* au Serikali iendelee kufungua vituo vidogo vidogo katika maeneo yale ambayo umeme unapelekwa ili wawepo wasaidizi

ambao wanawasaidia wananchi kuondoa changamoto ndogo ndogo zinazojitokeza ikitokea hitilafu au ukikatika umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nichangie pia kidogo kwenye suala la mafuta; kwanza naomba niipongeze Serikali kwa kutoa ruzuku kwa ajili ya kupunguza ukali wa bei ya mafuta nchini na hiyo tunaiona kuanzia leo angalau kiasi fulani kuna unafuu. Lakini pamoja na hiyo nilikuwa naomba niishauri Serikali kwanza kuimarisha Shirika letu la *TPDC* ili kuhakikisha kwamba sasa tunakuwa na shirika ambalo litaendelea kutusambazia mafuta kwa bei nafuu. Lakini vilevile tuweke mkakati wa kuhifadhi mafuta ya kutosha nchini ili yaweze kutusaidia pale ambapo patakuwa na changamoto ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo mimi naomba niishie hapo mchango wangu na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jonas William Mbunda. Tunaendelea na Mheshimiwa John Marko Sallu, Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka na Mheshimiwa Suleiman Jumanne Zedi wajiandae.

**MHE. JOHN M. SALLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie kwenye Wizara hii nyeti ya Nishati.

Kwanza naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo anatupambania

na kuhakikisha tunapata fedha za kuendesha miradi ili kuimarisha nchi yetu. *(Makofi)*

Pili, nimpongeze ndugu yangu Waziri wa Nishati Mheshimiwa January Makamba pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na timu yote ya Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kupambania nchi yetu iweze kuwa na nishati bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naomba nijikite kwenye *Power Master Plan*. Kwenye *Power Master Plan* tunatakiwa ikifika mwaka 2025 tuwe na megawati zipatazo 5,000 sasa ukiangalia ni lazima tupate vyanzo vingi vya kujazia pale. Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri ametaja vyanzo vingi, lakini mimi nilikuwa napenda sana kusisitizia chanzo cha umeme joto. Umeme joto ni umeme unaopatikana chini ya ardhi, Tanzania tuna vyanzo vingi. Katika hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati amevitaja vyanzo vinne na katika vyanzo hivi vinne tunapata megawati 200. Lakini mpaka sasa mpangilio wa umeme joto bado uko nyuma sana, sasa hapa nilikuwa nataka kutoa ushauri kwamba umeme joto huu kinachosababisha ile mitambo ifanye kazi ni ule mvuke unaotoka chini ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mvuke ule kwa jinsi ilivyo sasa hivi uko chini ya Wizara ya Madini. Sasa unakuta wale wadau wa maendeleo ambao wao ni rahisi sana kuchangia kwenye miundombinu, wanakuwa hawawezi kutupa misaada ya fedha kuendeleza joto ardhi hili. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwenye sheria zetu za nchi tubadilishe sheria iwe kama vile kwenye mafuta na gesi, mvuke huu uwe nao chini ya Wizara ya Nishati isiwe

chini ya Wizara ya Madini. Kwa hiyo huo ulikuwa ni ushauri wangu. Lakini vilevile naomba kushauri tujipange vizuri kwa hizi *rare mineral stones* ambazo zenyewe zinatengeneza umeme jadidifu. Sasa hivi dunia inakwenda zaidi kwenye umeme jadidifu, umeme ambao unatumika kwenye magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nchini tuna madini mengi yakiwemo madini ya *nickel, niobium* pamoja na *graphite* na kwenye jimbo langu kuna *graphite* nyingi ya kutosha. Sasa nilikuwa nafikiri kwamba ni wakati muafaka Serikali kuja na mbinu sahihi ya kuangalia mwenendo wa madini haya na kuangalia sheria zetu zilivyokaa ili tuweze kujipanga, tuingie kwenye ushindani wa dunia wa huu umme jadidifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kwenda kuongelea suala la *REA*. Kwa kweli nashukuru sana kwa mipangilio mizuri ambayo Mheshimiwa Waziri ameitangaza hapa ya kuweza kutafuta mbinu sahihi ya kufanya umeme vijijini kwa mara moja ili wananchi wetu waweze kupata manufaa mengi. Kwa hiyo, namuomba kwenye *area* hiyo ambayo amekuja na hiyo mbinu ambazo amezitaja kwamba, kuna makampuni yatapewa yafanye *engineering, construction* na *finance* hilo ni jambo bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naomba juhudi hizo ziongezwe kwa sababu kwa kweli vijijini tuna vitongoji vingi sana, ni vikubwa ambavyo bado havina umeme. Kwa mfano, kwenye Jimbo langu kuna takribani ya vitongoji 400 ambavyo vimeshakuwa vikubwa na vinahitaji umeme na havina umeme. Vingine viko katika maeneo ambayo viongozi wakubwa wanapita, kwa hiyo mara nyingi vinatoa picha mbaya. Wananchi wakifika

pale wanalalamika hawana umeme na umeme unawekwa kwenye kila kijiji, lakini vile vitongoji havina umeme. Kwa hiyo, ni jambo ambalo nilikuwa naomba tulifanyie nguvu ili tuweze kuiboresha nchi yetu vijiji vyote vipate umeme, kwani kule itavutia maendeleo na viwanda vidogo vidogo ambavyo vitasababisha maendeleo kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni *TANESCO;* kwa kweli wananchi wanajitahidi sana kutaka kujiunga na umeme. Nikichukulia mimi kwenye Jimbo langu kwenye hizi *center* kubwa za Mkata, Kabuku na Segera kuna wananchi wengi wameshaweza kuweka umeme kwenye nyumba zao na wameomba, lakini vifaa havijakuwa vya kutosha vya kuwaunganishia umeme. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara yetu hii ya Nishati ifanye mbinu ya haraka kuhakikisha wananchi hawa ambao wako tayari na ni wateja ambao wataongeza pato kwenye *TANESCO* na nchi yetu kwa ujumla waweze kupatiwa umeme haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache nashukuru sana ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa John Marko Sallu. Tunaendelea na Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi na Mheshimiwa Jesca David Kishoa wajiandae.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nami nafasi ya kuchangia katika Wizara muhimu hii ya Nishati na mimi nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan hasa kwa hili la leo kwamba hata mafuta sasa yamepungua bei kwa kiasi fulani. Lakini Mheshimiwa

January Makamba unafanya kazi nzuri hongera sana. *(Makofi)*

Mimi nadhani nianze na hili la leo kupungua bei ya mafuta, hili liende na kwenye Wizara zingine. Wakati mafuta yamepanda bei na vitu vingi vilipanda bei kwa kisingizio cha haya mafuta. Kwa mfano, Wizara nyingine litachukua hata hili kwamba kwa mfano kwenye kilimo sasa mazao nayo, yaonekane yanaanza kupungua bei kwa maana ya kwamba vitu tuvione vinaanza kupungua bei. Kama vitu mitaani vitazidi kuwa na hali ile ile wananchi hawawezi kuona unafuu wa kupungua bei ya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia usalama wa mafuta wapo ndugu zetu Kampuni mbalimbali na mashirika ambayo yanashughulika na usalama wa mafuta. Vituo vingi vya mafuta vina mafuta mazuri, lakini baadhi ya vituo vinaharibu sana magari ya watu. Kuna vituo ambavyo ukishaweka mafuta sijui huwa wanachanganya au namna gani, lakini baada ya hapo unakuta umeweka mafuta gari imekuwa na matatizo, kwa hiyo, wananchi pia wanapata tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye suala la *REA;* maeneo mengi yalishaahidiwa na Serikali kwamba yatapewa umeme wa *REA* katika mwaka huu mpaka mwaka kesho kwamba karibu vijiji vyote vitapata umeme, nchi hii ni kubwa na kuna majimbo mengine ni ya mjini kama mimi Tabora Mjini ni mjini, lakini kwa kutamka ni mjini, ila Tabora Mjini ina vijiji 41 na vijiji vile vingine vinakwenda mpaka masaa mawili kufikia hivyo vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna baadhi ya watendaji wakishaona neno mjini wanasema wote hawa kuunganishiwa *REA* ni shilingi 27,000 kitu ambacho wanakuwa hawajawatendea haki wananchi. Mheshimiwa Makamba uzuri Tabora umeshafika, umefika Nisha kule na sehemu zingine, lakini kuna Mawaziri wawili akiwemo Mheshimiwa Mgalu kuna siku moja nilikuwa nataka nimpeleke kijiji kimoja Itema, alivyofika njiani wakati ule akiwa Naibu Waziri akasema huku kote pia ni Tabora Mjini, naomba tuishie hapa hapa, hatukuweza kufika kwa sababu ni mbali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna mwongozo mlitoa kwamba hata vijiji vile viweze kupatiwa umeme wa *REA*. Sasa nina taarifa kwamba kwa sababu neno mjini linasemwa wananchi wa vijijini kule wanataka kupewa umeme kwa gharama ambayo sio ya *REA*. Kwa hiyo, naomba hili Mheshimiwa Waziri January uliangalie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala hili la uunganishwaji umeme, nimesikia hata kwenye taarifa ya Kamati ya Nishati, hawa wakandarasi ambao wanaunganisha umeme kwenye nyumba mbalimbali gharama zao ni kubwa sana. Nadhani ni vizuri Serikali ikaangalia namna ya kuwa-*control* hao wakandarasi, hakuna faida Serikali ipunguze namna ya kufanya *installments* za umeme, halafu hao wakandarasi wawe wanazidisha bei, yale makali ya fedha za uunganishwaji umeme yatabaki pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna hawa waratibu ambao watakuwa wanatoa taarifa hizi za uunganishwaji wa umeme hasa katika suala hili la *REA*. Naomba ndugu yangu January katika hili hao waratibu wenu ambao watakuwa wanatoa hizi taarifa muwafuatilie ili kuona

kwamba taarifa zao je, zitakuwa sahihi? Maana yake mara nyingi hamuambiwi taarifa ambazo ni sahihi. Vijiji vingi kweli na vitongoji havijapata umeme na wananchi muda tuliowaahidi kwamba ukifika muda fulani watapata umeme, wanasikiliza tu muda ule ukifika hawakupata huo umeme Mheshimiwa January tutakuwa katika hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala hili la kubadilisha nyaya za umeme sehemu mbalimbali nchini, Tabora kuna shida sana ya kukatikakatika umeme kama walivyosema wenzangu hapo. Wananchi wanapata shida ya umeme lakini pia kwa wafanyabiashara ambao ni walipakodi wazuri kwa Serikali, mitambo yao muda mrefu inapokuwa haifanyi kazi wanapata wao hasara, lakini pia na Serikali inapata hasara kwa kutopata zile kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni-*declare interest* katika eneo hili na mimi ni mhusika. Mimi nina mashine mbalimbali za kusaga, kukoboa na ku-*grade,* lakini muda mrefu unaweza kukuta kwa wiki mara nne hazijafanya kazi kabisa umeme haupo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, unapata hasara mfanyabiashara, lakini pia Serikali inapata hasara, lakini umeme ule unaporudi mara nyingine unaunguza vyombo mbalimbali, kwa sababu unarudi ukiwa hauja-*stabilize* na gharama hiyo *TANESCO* kulipa sio rahisi huwa hawalipi, kwa hiyo wananchi na wafanyabiashara wanapata hasara sana, kwa hiyo naomba muangalie katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa January aliongelea hapa suala kuhusu mkataba ule wa gesi

ambao umesema mazungumzo yameendelea vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hii gesi watakapokuwa wamefanikiwa ionekane kweli ina faida kwa wananchi kwa sababu inaweza ikaletwa gesi lakini gharama zake ni kubwa na huku tunasema tuondoe utumiaji wa nishati hizi halisia kama miti na nini kwa sababu ya uharibifu wa mazingira, lakini kama hii gesi ambayo wanaendelea kufanya mchakato wake itaendelea kuwa ghali itakuwa hakuna faida, wananchi wataendelea kukata miti na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, naunga mkono hii hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka. Tunaendelea na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi na Mheshimiwa Jesca David Kishoa ajiandae.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene niweze kuchangia hotuba hii muhimu ya Wizara ya Nishati. Nitaanza na Miradi ya Umeme Vijijini *(REA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Bukene kabla ya mwaka huu, mwaka uliopita lilikuwa limeunganishiwa umeme vijiji 25 kati ya vijiji 81 vilivyopo katika jimbo langu na vijiji 56 vilikuwa bado havijapata umeme, lakini kuanzia mwaka jana mkandarasi *Silo Power* yuko *site* na anaweka umeme kwenye vijiji vyote 56 vilivyokuwa vimebaki. Nafahamu kwamba, *speed* yake

kwa sasa sio nzuri, nilitembelea maonesho ya nishati wiki iliyopita hapa Bungeni nikakutana na mkandarasi na alitoa maelezo kwamba, ana changamoto ya mabadiliko ya bei kulingana na mkataba wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina taarifa kwamba, Wizara ya Nishati imeshakaa na wakandarasi ili kupata ufumbuzi wa tatizo hilo, kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba, tatizo hilo litakwisha na kasi ya mkandarasi sasa kuweka umeme kwenye vijiji hivi 56 itaendelea kama ilivyoanza. Matumaini yangu ni kwamba, mwisho wa mwaka huu vijiji vyote vitakuwa vimeshapata umeme kwa hiyo, kimsingi ni kwamba, kazi hii ikikamilika jimbo langu lenye vijiji 81 vyote vinakwenda kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na vipaumbele ambavyo Mheshimiwa Waziri amevitaja kwenye hotuba yake na kipaumbele kimojawapo ni kwamba, sasa wanakwenda kuanza kazi ya kupeleka umeme kitongoji kwa kitongoji. Ilivyo sasa hivi, tunapeleka umeme kwenye vijiji, lakini kimsingi kijiji kinakuwa na vitongoji kadhaa. Kwa mfano, jimboni kwangu kuna Kijiji kinaitwa Kagongwa, Kijiji ni Kagongwa, lakini Kagongwa ina vitongoji saba na hapa mkandarasi anapeleka umeme kwenye vitongoji viwili. Kwa hiyo, unakuta Kijiji cha Kagongwa vitongoji viwili ndio vina umeme, vitano vitakuwa havina umeme, lakini ukihesabu vijiji vilivyopata umeme Kagongwa utaihesabu, lakini kumbe Kagongwa yenye vitongoji saba ni viwili tu ndio vinakwenda kupata umeme. Kwa hiyo, naunga mkono hicho kipaumbele cha Wizara cha kuhakikisha kwamba, sasa inaondoka kwenye ngazi ya vijiji, inakwenda kupeleka umeme kitongoji kwa kitongoji na hicho ndio kitakuwa kipimo sahihi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la kupandishwa kwa bei ya kuunganishwa umeme. Wote tunafahamu kwamba, maeneo ya vijijini gharama ya kuunganisha umeme ni Sh.27,000, lakini hivi karibuni yalitokea mabadiliko kwa baadhi ya maeneo ya vijijini yakapandishiwa hiyo gharama. Kwa mfano, katika Jimbo langu la Bukene kuna vijii vitatu, Kijiji cha Bukene, Kijiji cha Itobo na Kijiji cha Mambali, vimepandishiwa bei ya kuunganishiwa umeme kutoka Sh.27,000 sasa hivi mtu ambaye yuko ndani ya mita 30 ambaye hahitaji nguzo kutoka Sh.27,000 anatakiwa alipe Sh.320,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwatendei haki kwa sababu, haya ni maeneo ya vijijini. Bukene bado ni kijiji, kina Mwenyekiti wa Kijiji, kina Serikali ya Kijiji, Itobo hivyohivyo, Mambali hivyohivyo, maeneo yote haya ni vijiji, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake nafurahi kwamba, ametambua kwamba hii ni kero na amepata malalamiko mengi na ametuma timu ya wataalam na ametoa *time frame* ya miezi sita kwamba, hawa wataalam wampe *feedback*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, haya maeneo yote ambayo ni vijiji, kwa mfano Bukene, Mambali, Itobo, pamoja na kwamba, ukiyaona yanafanana na miji, lakini bado ni vijiji. Yana Serikali za Vijiji, yana Wenyeviti wa Vijiji, kwa hiyo, yalipishwe sawa na vijiji vingine gharama ya Sh.27,000 ili kuondoa ubaguzi wa kijiji kwa kijiji kwa sababu, wote wanalingana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nimeliona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati ni kuwa, Wizara imetenga bilioni tano kwa ajili ya kuanza sasa utekelezaji wa mambo kadhaa katika Mradi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima mpaka Tanga. Kama ambavyo

nimekuwa nikisema jimboni kwangu pale ndio kuna kituo kikubwa cha *courting yard* ambako mabomba yote, vipande vyote vya mabomba elfu 86, vitalazimika kufika pale Sojo, jimboni kwangu kupakwa rangi maalum ili vitakapofukiwa chini visioze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya kazi ambazo Mheshimiwa Waziri amezizungumza kwenye Wizara yake ni kwamba, mwaka huu amepata fedha ambazo zitatumika kutoa elimu kwa jamii inayozunguka mradi ule ili kuwafahamisha kuhusu fursa mbalimbali zinazokuja na mradi ule. Sasa pale jimboni kwangu wananchi wafanyabiashara tuko tayari kuchangamkia hizi fursa. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba, Wizara ya Nishati ikishirikiana na Wizara nyingine, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara za Uwezeshaji kwamba, sasa hivi shughuli pale imeanza kidogokidogo kuna kampuni imeshaanza pale kufanya shughuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kuwatambua sasa hawa wafanyabiashara wa ndani, wazawa wa maeneo yale, kuwaeleza fursa zilizopo pale na kuangalia wana changamoto gani. Wengine wana changamoto za kimitaji, waweze kusaidiwa wapate mitaji ili waweze kushindana na kupata kazi zitakazokuja na fursa ya hili bomba la mafuta. Pale kutakuwa na kazi za usafirishaji, kutakuwa na kazi za kulipa vyakula, kazi za ulinzi na kazi mbalimbali, kwa hiyo, matumaini yetu ni kwamba, sisi ambao ni wakazi ambao tunazunguka maeneo yale ndio tuwe wa kwanza kunufaika na fursa ambazo zitapatikana pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kunufaika na hizo fursa kama tutaachwa tu tushindane na watu wengine, kwa hiyo, kuna kila haja kama Mheshimiwa Waziri

alivyozungumza kwenye hotuba yake kwamba, amepata fedha sasa ambazo wataalam watakuja katika maeneo yale, watatueleza fursa zilizopo, watatambua sasa wafanyabiashara, wazabuni na wazawa mbalimbali ili kutatua changamoto zao na kuwawezesha kuchangamkia hizo fursa. Sisi tuko tayari kabisa kuchangamkia fursa hizo ili tuweze kunufaika na uwekezaji mkubwa wa Serikali katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hofu na hili, uwezo wa Mheshimiwa Waziri Makamba naufahamu siku nyingi na najua haya mengi ambayo amesema ataya-*deliver,* lakini chini ya usimamizi makini wa Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, sina hofu, najua changamoto zilizopo zitatatuliwa ili sekta hii ya nishati iweze kupatiwa msukumo unaohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwetu kule hii nishati maana yake ni uchumi. Maeneo ya vijijini kule, kwa mfano, sasa hivi jimbo langu kutokana na uwepo wa nishati ya umeme sasa hivi shughuli nyingi za uzalishaji, kuongeza thamani ya mazao zinaongezeka. Kule kwangu miaka mizuri ya fedha sisi ni wakulima wazuri sana wa mpunga, lakini miaka yote kabla hatujapata umeme, mpunga wote tulikuwa tunaupeleka Kagongwa kule, Kahama Mjini kwa ajili ya kuchakatwa kuwa mchele. Kwa hiyo, tulikuwa tunapoteza fursa za kiuchumi, lakini sasa hivi maeneo ya jimbo langu kule baada ya umeme kupatikana, wawekezaji wamekuja, wamewekeza, wana mashine kubwa za kisasa za kuchakata mchele na sasa hivi hatuuzi mpunga tena tunaongeza thamani, tunauza mchele na kupata faida kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Selemani Zedi. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu ni Mheshimiwa Jesca David Kishoa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza kabisa niuelekeze mchango wangu katika Shirika letu la *TPDC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemo unasema hivi, *to realize the value of what you have imagine you have lost it.* Ili tuweze kujua mchango wa *TPDC* kwenye sekta ya nishati tufikirie kuipoteza *TPDC* kwenye sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovyote vile tusitegemee *TPDC* inaweza kufanya vitu vikubwa na vizuri kama haijawezeshwa vya kutosha. *TPDC* leo hii inadai *TANESCO* zaidi ya bilioni 500, hizi ni fedha nyingi sana. Wakati inadai *TANESCO* deni la bilioni karibu 600 wanamchukua *TPDC* kupitia kampuni tanzu ya *TANOIL* wanamwingiza kwenye *market sharing* kwenye biashara ya mafuta. Tafsiri yake ni kwamba, ni kama unamchukua mtoto wako unamfunga miguu na mikono, halafu unampeleka kwenye ulingo akapambane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TPDC* kupitia kampuni tanzu ya *TANOIL* inaagiza *only 2%* ya mafuta yote yanayoletwa nchini kila mwezi, yaani katika tani laki tatu zinazokuja kwenye nchi kila mwezi *TPDC* wanaingiza tani elfu ishirini peke yake. Huyu *TPDC* kupitia kampuni tanzu ya *TANOIL* anawezaje kupata *muscles* kwenye *negotiation* ya *price* kama asilimia ya kuingiza mafuta ni *only 2%? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri mambo kadhaa; kwanza ni muhimu sana Serikali ikaingilia kati deni hili la *TPDC* kudai *TANESCO*. Wanaweza wakatenga kiasi kidogo cha ruzuku wakaweza kupunguza ukubwa wa deni hili. Pia kuna haja ya kubadili sheria zetu kwenye *Petroleum Act* tukaona kwamba, badala ya fedha yote inayopatikana *TPDC* kupelekwa Hazina, basi ikishafika Hazina irudi kwa ajili ya kusaidia shughuli za *TPDC*. Ni muhimu sana kwa sababu *TPDC* ikiwezeshwa ndio muarobaini wa kudumu wa changamoto ya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa mwisho kwa upande wa *TPDC,* ni muhimu sasa ule ujenzi wa vituo vya uhifadhi wa mafuta ukamilishwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kwa ufupi ucheleweshwaji wa Mradi wa Bwawa la Julius Nyerere. Taarifa ya Kamati iko *very clear,* sababu zinazotolewa na Serikali ambazo zinaonesha ucheleweshwaji wa Mradi wa Julius Nyerere, sababu hizi hazitoshi. Sababu hizi hazitoshi kwa sababu leo tunaambiwa Mradi wa Julius Nyerere umechelewa kukamilika eti kwa sababu za kimazingira. Ninavyofahamu hakuna mradi wowote ambao unaweza ukatekelezeka bila kufanyika *feasibility study,* lakini pia najua hakuna mradi wowote ambao unaweza ukakamilika bila kufanya *environment impact assessment*. Haiwezekani mradi wa *over six trillion* uwe na kikwazo cha kimazingira, kwanza ni aibu hata taarifa hii kuwepo kwenye *documents* za Serikali kwa sababu, inaonesha namna ambavyo hatuko *smart. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa sababu nyingine ni *Covid-19*. Leo naomba niseme *Covid-19*

imekuwa ikitumika mara nyingi kama kichaka cha kuficha uovu ambao unaendelea kushindwa kutekeleza miradi mbalimbali ya Serikali. Kama kweli sababu ni *Covid-19* basi tuambiwe, ile *scope time* kwa sababu, inaonekana ule muda ambao wanasema umesababishwa na *Covid-19* hauendani kabisa na uchelewaji, tumechelewa zaidi ya mwaka mzima. Tunahitaji tuambiwe *very specifically,* hiyo mitambo wanayosema kwamba, imeagizwa na ikachelewa kuja kwa sababu ya *Covid-19* kwanza ni mitambo gani na *evidence* tupewe kwa sababu, inasikitisha sana miradi mikubwa kama hii ambayo ina nia ya kutaka kututoa kwenye changamoto ya umeme kushindwa kutekelezeka kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa haraka haraka nijielekeze sasa kuchangia eneo la *global agenda* kubwa ya duniani kwa sasa inayohusiana na masuala ya *energy transition.* Wote tunajua katika hii dunia tumekuwa tukiishi na kunakuwa na vipindi vinapita; kulikuwepo mwanzoni kuna kipindi cha *renaissance,* wanaojua historia karne ya 14, kikaja kipindi cha *enlightment* karne ya 17, kikaja kipindi cha *industrial revolution,* kikaja kipindi cha *globalization,* kimekuja kipindi sasa cha *fourth industrialization* ambapo hapa tunazungumzia masuala ya *artificial intelligence,* tunazungumzia masuala ya *internet* na tunazungumzia masuala ya *energy transition.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika kipindi hiki unapozungumza *energy transition* haya ni makubaliano ambayo yamefanywa na Wakuu wa Nchi mbalimbali duniani kutaka kuangalia njia mbadala ya kuweza kuokoa dunia na athari hasi za tabianchi na mazingira na ndio maana kumekuwa kukifanyika mikutano mikubwa duniani.  Umefanyika mkutano wa *Paris Agreement*

mwaka 2016, lakini pia kuna Mkutano wa *Scotland Cop26* wa mwaka 2021 ambao lengo kubwa la mikutano hii na huu Mkutano wa *Scotland Cop* wa *26* alihudhuria Mheshimiwa Rais mwaka jana, lengo kubwa la makubaliano haya wamesema kwamba, wanataka sasa dunia iwe na joto lisilozidi *1.5 centigrade*. Njia wanayoitumia wanasema wanataka kutumia njia ya kusitisha matumizi ya nishati chafu ambayo ni *fossil.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nina vitu nataka nishauri hapa. Kama kuna kipindi tunatakiwa kuipa kipaumbele kwa nguvu zote taasisi ya Serikali ya *GST* ni sasa. Nasema hivyo kwa sababu gani; sisi tuna *critical minerals,* hizi *critical minerals* ndio zinazohitajika sana kwenye soko la dunia sasa hivi kwenye madini, kwa sababu moja, ndio madini yanayotakiwa kutumika kutengeneza miundombinu ya nishati safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia umeme wa upepo unatengenezwa kwa kutumia *turbines. Turbines* inatumia madini ya *copper,* ukiangalia mabetri ya magari yanatengenezwa kwa kutumia madini ambayo yanaitwa *graphite,* kwa hiyo, haya madini yote na mengi sana yapo nchini Tanzania, lakini tuna changamoto kubwa moja, *GST* ambao ndio watafiti wakubwa wa madini katika nchi yetu hawawezeshwi. Ndio kwanza bajeti yao wametengewa bilioni 3.5 na hii ni *OC* peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri, ile *helicopter* iliyokuwa inazurura majuzi hapa kwenye mikoa mbalimbali ipelekeni *GST* ikafanye kazi kwa ajili ya kuchunguza madini haya yanapatikana wapi. Itakuwa sio mara ya kwanza, tuliwahi kuwa na *helicopter* sisi 1990 huko miaka ya nyuma na ilifanya kazi kubwa. Ni vizuri sasa hivi tunapotaka kutafuta madini haya ambayo

yanaweza kutunufaisha kwenye nchi yetu, vitu kama hivi vitumike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Tanzania ni watano duniani kwa madini ya *graphite* ambayo ndio yanahitajika sana kwa sasa, lakini yako wapi? Ni jitihada gani Serikali imefanya kuyatafuta? Tunategemea taarifa kutoka kwenye kampuni za madini, haiwezekani. Tutafute madini haya ili yaweze kutusaidia kwenye kutengeneza miundombinu ya nishati safi ambayo ndio agenda kubwa duniani kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna changamoto *GST* hakuna watumishi. Ni vema idadi ya watumishi ikaongezeka ili wafanye kazi kwa uhakika zaidi. Itakuwa ni aibu sana pamoja na rasilimali kubwa hii ambayo Mwenyezi Mungu ametupa ya kuwa na madini ambayo ndio yanahitajika kwa sasa, *critical minerals,* halafu bado tukaendelea kuyakalia, tukaendelea kuyafunika na tusijue namna ya kutumia na wakati kufikia mwaka 2025 kama tutakuwa vizuri kwenye kuyatafuta, nchi ya Tanzania ndio inakwenda kuongoza dunia nzima kwa kutoa madini ya *graphite,* hizi ni tafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, naomba nigusie umeme wa upepo Mkoa wa Singida. Tumekuwa tukiimba wimbo huu kwa muda mrefu sana. Naomba tu ku-*declare,* pamoja na kwamba, duniani kwa sasa agenda ya matumizi ya nishati safi ni pamoja na nishati ya umeme wa upepo, lakini nashindwa kuelewa ni kwa nini Serikali imekuwa na kigugumizi kwenye utekelezaji wa Mradi huu wa Umeme wa Upepo Singida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka nenda miaka rudi tumezungumza, toka miaka ya 2011/2012 mpaka leo

hakuna kitu kilichofanyika hata nguzo moja hakuna. Tunaahidiwa miaka yote umeme wa upepo, umeme wa upepo, hakuna kilichofanyika. Watafiti wametafiti wakaona kwamba, umeme wa upepo wa uhakika katika ukanda wa *East Africa* unapatikana Singida na Makambako na una uwezo wa kuzalisha nishati ya kutosha, kwa nini kunakuwa na kigugumizi kwenye utekelezaji wa nishati ya umeme wa upepo Mkoa wa Singida? Wananchi wa Singida tumewakosea nini Serikali hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inazungumza vyanzo vingine vya umeme wa upepo inaacha kutaja Singida kwenye umeme wa upepo na wakati inajua kuna umuhimu wa kuwa na *energy mixing* kwenye uzalishaji wa umeme. Naomba Serikali kwa dhati kabisa na Mheshimiwa Januari Makamba aji-*commit* kwenye hili, wenzake wengi waliji-*commit* kwenye hili, lakini hakuna utekelezaji wowote. *Do your part* Mheshimiwa Waziri kwenye hili, afanye hili ili wananchi wa Singida wamkumbuke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jesca David Kishoa na huyo ndio mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu.

Nawashukuru kwa michango yenu yote mizuri ya kistaarabu leo hii. Basi tutaendelea na wachangiaji wengine jioni, nitawataja wachache; kuna Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mheshimiwa Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mheshimiwa Shally Joseph Raymond, Mheshimiwa Ahmed Shabib na Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali na wengine tutaendelea nao.

Baada ya kusema hayo, nawatakiwa mchana mwema na mapumziko mema na nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano yetu tutaanza na Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mheshimiwa Dkt Christina Christopher Mnzava na Mheshimiwa Shally Raymond wajiandae.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia mawazo yangu na wananchi wapiga kura wa Jimbo la Kondoa Mjini kama namna wanavyopenda itokee katika Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema na niishukuru Wizara kwa kazi kubwa

ambayo inafanywa katika maeneo mbalimbali. Mimi ninaomba nichangie *specifically* kwenye Jimbo langu kwa sababu zipo changamoto ambazo zinawakumba wananchi wa Jimbo wangependa wapate majibu ya Serikali Wizara na mimi kama Mbunge wao nipate majibu hasa ya kuwajibu baada ya kuwa na changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja *specifically* nakwenda kwenye Kata inaitwa Bolisa kwanza ifahamike naongoza Jimbo la Mjini, Halmashauri ya Mji wa Kondoa kwa hiyo mimi nina mitaa sina vijiji. Ninayo Kata inaitwa Bolisa hii Kata ina mitaa mitatu ilipata mradi wa *REA* toka mwaka 2019, Mkandarasi aliyepewa kazi ile aliondoka mpaka wiki hii ndiyo niliambiwa amerudi lakini pamoja na kurudi kwenyewe bado kuna viporo ambavyo hakuvimaliza. Lakini ukiacha viporo ambavyo hakuvimaliza nimeambiwa kwamba *scope* yake imeisha lakini kuna mitaa miwili katika hiyo mitatu haikupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wananchi wa Kata ya Bolisa mara zote wanaipigia simu wakitaka kujua kwamba kwenye mradi wa *REA* ndiyo umeishia pale? Kwa sababu hata nilipohudhuria kwenye maonesho pale nilikutana na meneja wangu na watu ambao tumekuwa tukihangaika namna ya kuona tunaweza tukaukwamua ule mradi. Kwa hiyo, ningependa Mheshimiwa Waziri anisaidie kupata kujua ule mradi umeishia pale? Kama umeishia pale maana yake ni mtaa mmoja tu ambao ni nguzo zimefika pale, wananchi walishafanya *wiring* toka mwaka 2020 mpaka leo wanasubiria umeme, wana mashaka pia wanataka kujua mradi ule wa *REA* kama umeishia pale nyumba namba moja imewekewa umeme kwa Shilingi 27,000. Je, ile ya pili mradi ulipokomea wao watawekewa kwa 27,000 au watawekewa kwa hiyo 300,000?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka tupate kujua kwa sababu kuna changamoto kuna Kata inaitwa Suruke, Kata hii ina mitaa yake, Kata pamoja na mitaa hakuna nguzo hata moja iliyowahi kwenda. Kwa hiyo, ni Halmashauri ya Mji lakini Kata yote haina hata nguzo iliyosimama kwenye ardhi ya Kata ile. Katika kufuatilia sijaona hasa mpango hasa wa kuona kwamba Kata ile ni lini hasa itapelekewa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekutafuta Mheshimiwa Waziri sikupata bahati ya kukutana na wewe lakini nilikutana na Mheshimiwa Naibu Waziri, akawa amewasiliana na Mkurugenzi Ndugu yetu Seif lakini nawashukuru yeye *Engineer* Seif pamoja na Kasomambutu walifanya mawasiliano walikwenda kutembelea hiyo mitaa ninayoisema waliona hali halisi. Sasa nitaka kujua hii Kata hasa ya Suruke na yenyewe itapelekewa umeme kwa maana ya *REA* au tunategemea kuwapelekea kwa zaidi ya shilingi 300,000 au shilingi 600,000, shilingi 900,000 au shilingi 1,000,000? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni hili la utata wa bei ya kuwaunganishia wananchi umeme, ni kweli ile ni Halmashauri ya Mji ina mitaa badala ya vijiji lakini ndugu yangu kutoka katikati ya mji unakwenda hizo Kata ni kilometa nyingi na kazi pekee inayofanyika kwenye Kata zile ni kilimo na mifugo. Maana yake siyo tu vijiji vinavyokua bado ni vijiji mno, mwananchi anajenga nyumba yake kwa kipindi cha miaka mitatu au minne sana katumia gharama kubwa 200,000 leo ukimwambia mwananchi huyu ukamuunganishie umeme kwa shilingi 300,000 bila nguzo akiongeza mita 60 shilingi 600,000 yule mwananchi hana uwezo wa kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia hata watumishi tu Walimu hivi kweli mtu anaweza kuunganisha umeme kwa hali ilivyo katika vijiji vyetu, hii mitaa yetu ambayo miji tunataka tuikuze kwa gharama hiyo? Kwa hiyo nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri hebu ule mpango mlioutaja kwenye hotuba yenu ya kufanya utafiti kuona kama watu hawa wanaweza wakagharamia hiyo ni vema ukafanyika mapema. Hapa mimi ninashauri Kamati utakayoiunda itakwenda miezi sita lakini wananchi tayari walishajiandaa miaka mitatu iliyopita kuupokea umeme na ninaamini nchi hii ni kubwa mimi nikurahisishie tu kwa Jimbo langu la Kondoa Mjini. Jimbo la Kondoa Mjini ni Mji ambao unakua bado hauna ile hadhi kubwa ya kusema kwamba wananchi wenye kuishi hapa ni watu wenye uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mitaa ambayo naomba niitaje sasa hivi ni mitaa ambayo ipo vijijini kabisa ambapo hakuna mwananchi nikiangalia mmoja mmoja wa kulipa zaidi ya hiyo 300,000 au 600,000 kwa sababu asilimia kubwa watu hawa wanahudumiwa na mpango wa *TASAF*. Sasa najiuliza mtu unamsaidia kula asubuhi, mchana na jioni kwa kutumia *TASAF* anawezaje kuingiza umeme kwa hiyo pesa? Lakini sote tunakubaliana ukipeleka umeme kijijini maana yake unakwenda kuinua uchumi wa wanavijiji wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia maeneo mengi ambayo mmepeleka umeme vijiji vile vimebadilika kabisa katika shughuli za kiuchumi, badala ya watu kulima wameweza kufungua viwanda vidogo vidogo, wameweza kufungua *saloon* na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, kwa sababu nchi yetu ipo katika uchumi wa kati ni vema sasa mitaa hii tusiibague kwa kusema tuwafungue umeme kwa gharama kubwa kwa sababu kuwapelekea

huduma ya umeme ni kuwasaidia kuwakwamua kiuchumi, kwa sababu nchi yetu ipo katika uchumi wa kati tunaamini sasa tutaendelea kuulinda huo uchumi wa kati kwa kuwapelekea wananchi umeme maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa naona aibu sana ninapofanya ziara kwenye Jimbo la Mjini halafu unakwenda Kata nzima hata nguzo haina kwangu inakuwa ni shida sana. Tunaitaje Mji hali ya kuwa hakuna mwanga kuna giza wakati wote? Naomba niitaje hii mitaa ili Mheshimiwa Waziri ayachukue mambo haya yangu siyo mengi ni matatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni huo mradi wa *REA* Kata ya Bolisa lazima ufike mwisho na wananchi wapelekewe umeme ili kupunguza kero kwa wananchi, jambo la pili ni kuiangalia hiyo Kata ya Suruke ambayo yenyewe Kata yote na mitaa yao hakuna hata nguzo iliyosimama kwenye ardhi ya Kata hiyo, maana yake siyo umeme tu hata nguzo haijasimama. Tuna mtaa wa Damai, tuna mtaa wa Kwantisi, mtaa wa Gubali, mtaa wa Hachwi, mtaa wa Chandimo, mtaa wa Serya, mtaa wa Dumi, mtaa wa Kwamtwara, mtaa wa Chemchem, mtaa wa Tampori, mtaa wa Ausia, mtaa wa Suruke, mtaa wa Guluma, mtaa wa Tungufu pamoja na mitaa ya Unkuku pamoja na Choyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa fikiria ni Jimbo lenye Kata Nane peke yake mitaa yote hii haina umeme na tunasema hii ni Halmashauri ya Mji. Mimi Mheshimiwa Waziri ninakuomba ndugu yangu hakikisha waelekeze *REA* wakawasaidie, ule mpango wa *TANESCO* wa kwenda kusema unakwenda kujaziliza, *TANESCO* yenyewe bajeti yao ni ndogo wakipata nguzo 20 hazifiki popote. Leo Mji unapanuka maeneo ya karibu ya Mji,

*TANESCO* wanaweza wakamudu kwa hizo nguzo 30, 20, 40 lakini mtaa mzima hauna umeme, Kata nzima na mitaa yake haina umeme hawa wanahitaji wasaidiwe mradi wa *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kuna hii nini *Peri-urban,* tunaisikia Dodoma tunaisikia Dar es Salaam, tunaisikia Arusha kwenye miji yetu ya Halmashauri huko kwa kweli hatuna matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nina mashaka makubwa sana na kuwa na Halmashauri za Mji, leo mambo ya Halmashauri ya Mji yamekuwa ni ya kusubiri ninaogopa tutasubiri na huu umeme mpaka vijiji vyote vitakamilika. Kwa hiyo tutakuza vijiji tutasahau kuikuza mitaa yetu. Leo ukija kwenye maji Miji 28 tunaendelea kusubiri ukija kwenye *tactic* masuala ya barabara tunasubiri, ukija kwenye umeme tunaambiwa kuna huo mradi tofauti na *REA* ambayo tunajua ndiyo wanafanya vizuri sisi tunaendelea kusubiri! Hivi ni dhambi kuwa na Halmashauri ya Mji? Ninaunga mkono hoja na wala sina haja ya kushika Shilingi na nitaitikia ndiyo bajeti yao lakini wafahamu kilio hiki cha Mbunge mwenzao kinanisababishia mimi wakati mwingine nakimbia Jimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Juma Makoa, tunaendelea na Mheshimiwa Dkt Christina Mnzava, Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali na Mheshimiwa Charles Paul Mwijage wajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nimshukuru Mwenyezi Mungu kupata

fursa ya kusimama kwenye Bunge lako Tukufu kuchangia Wizara ya Nishati. Ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya katika Taifa letu. Tulikumbwa na tatizo kubwa sana la mfumuko wa bei ya mafuta lakini Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyotuthamini Watanzania aliweza kutoa ruzuku ya Bilioni Mia Moja, kwa kweli tunampongeza sana kwa kazi kubwa ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwashukuru Wizara ya Nishati Mheshimiwa Kaka yangu Makamba, Watendaji wote na Wasaidizi wako wote kwa kweli mnafanya kazi kubwa sana. Tunajua dunia nzima ina changamoto nyingi na imepelekea mafuta kupanda bei, hili ni janga la dunia siyo janga la Tanzania peke yake. Baada ya Mheshimiwa Rais kutoa fedha kama ruzuku Shilingi Bilioni 100 leo Dodoma nimeenda kununua mafuta angalau yameweza kushuka bei kidogo kama Shilingi 120 hivi, kwa kweli ni juhudi kubwa ambayo inafanywa na Serikali yetu tunajua katika kila mafanikio changamoto hazikosekani tuwaombe sasa kwa bajeti hii ambayo iko mbele yetu ile mipango ambayo mmepanga, nimeona katika jarida hili ambalo mmetupatia mmeweka vipaumbele, ukivisoma hivi vipaumbele unapata matumaini kabisa kwamba Wizara hii inakwenda kufanyakazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijielekeza tu kwenye kipaumbele Namba Mbili cha bajeti hii ambacho kinasema kutekeleza miradi ya nishati vijijini pamoja na kuanzisha utaratibu wa kupeleka umeme katika vitongoji ndani ya nchi. Kwa kweli, suala la umeme hasa huu umeme wa *REA* vijijini imekuwa ni changamoto kubwa

sana. Unakuta kuna Kata ambazo ziko kwenye Manispaa mfano kule Shinyanga, kuna Kata ambayo iko karibu kabisa na *grid* ya Taifa, pale Ibadakuli ambapo umeme uko pale *grid* ya Taifa iko pal,e lakini vijiji na vitongoji vya pembeni havina umeme. Hili suala kwa kweli linaumiza sana wananchi wakati mwingine anakuuliza swali unashangaa, anakwambia *grid* ya Taifa hii hapa ambayo inasambaza umeme kwenda Mwanza, ambayo inapeleka umeme Kahama, ambayo inapeleka umeme Mikoa mingine sisi hapa tunaotoka katika kata ya Ibadakuli hakuna umeme! Kwa kweli huwa inaumiza sana kuona kwamba wananchi wanapata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa nyingine ni nini? Ni kwa sababu wale wako ndani ya Manispaa wanahesabika kama wako Mjini lakini kiukweli ni kwamba wako kijijini. Vijiji vile ambavyo viko ndani ya Manispaa ningeomba huo utaratibu wa *Peri-urban* ambao tunausikia mnausema kila wakati lakini utekelezaji wake bado unasuasua. Tunaomba vijiji vyote ambavyo viko ndani ya Halmashauri za Miji au Halmashauri za Manispaa ziweze kupatiwa umeme ili hawa wananchi na wenyewe waweze kufaidika na suala zima la kukuza uchumi. Kwa sababu tunajua umeme ndiyo chanzo kikubwa cha kuhakikisha kwamba vijana wetu wanajiajiri, wengi wamefungua viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya kutengeneza mageti, wengine wanachomelea magari, wengine wanatengeneza majiko bila kuwa na nishati ya uhakika ya umeme hawawezi kufanya kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nataka kukizungumzia ni suala zima la kukatika umeme. Kwa kweli inasikitisha, Wizara mnatufanya tunapata hasara, kwa sababu kama una kiwanda na una *shift*

unalipa wafanyakazi, unategemea wafanyakazi wengine waingie Saa 12 mpaka saa Nane, wengine waingie Saa Nane mpaka usiku, wengine waingie usiku Saa Nne mpaka asubuhi, umeme unapokatika ina maana uzalishaji unadorora, lakini mwenye kiwanda hataacha kuwalipa wale wafanyakazi, matokeo yake nishati inazorota umeme unakatika wanaamua kuwapumzisha vijana ili kubana matumizi. Wenye viwanda wakishabana matumizi tayari wale vijana wanarudi mtaani wanakuwa hawana ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tujue Mheshimiwa Waziri unapokuja kuhitimisha, tunataka tujue utaratibu wa kudumu mpango mkakati wa kudumu ambao utawezesha huu umeme ukawa *stable,* kwanza mnatutia hasara unawasha TV, umewasha friji baada ya muda umeme umekatika unarudi unakatika unaweza ukakatika hata mara nane kwa siku, kwa kweli hii haikubaliki ninaomba kabisa Wizara ya Nishati ije na majibu mazuri na mpango mkakati mzuri, umeme wa uhakika mwanzoni tulikuwa tunajua labda wakati mwingine maji sijui katika Bwawa la Mtera yamepungua, mara sijui vitu gani! tunataka mtuambie gesi asili inatusaidiaje kuhakikisha umeme unakuwa *stable*, mabwawa yanatusaidiaje kuhakikisha umeme unakuwa *stable,* hizi *grid* zetu za Taifa zinatusaidiaje kuhakikisha kwamba umeme unakuwa *stable? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi wameyafanya katika hii Wizara, kwa kweli hata maneno mengi ya kuongea ninakosa kwa sababu hapa wametu-*pre-empty* wametupa mpango mzuri, wametupa vipaumbele, wametupa *way forward,* sasa tunaomba haya mliyoyaandika yatekelezeke, mwaka kesho tukiwa hai kipindi cha bajeti hii ya Wizara ya Nishati, hii itakuwa

*reference* na mkishindwa kuitekeleza hii itabidi tuwaulize tushikiane Shilingi hapa, tuminyane tushikane mashati ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wananufaika na nishati ambayo Mwenyezi Mungu ametujaalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ninahitaji kusikia majibu ya uhakika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt Christina Mnzava tunaendelea na Mheshimiwa Seif Hamis Gulamali, Mheshimiwa Charles Paul Mwijage na Mheshimiwa Venant Daud Protas wajiandae.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami leo niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Nishati. Kwanza binafsi nimpongeze Mheshimiwa Rais lakini pia nipongeze Wizara kwa kazi nzuri ambazo zimeendelea kufanyika na pongezi hizi zinaenda hasa kwenye uendelezaji wa Bwawa letu la Mwalimu Nyerere, sisi kama Wajumbe wa Kamati tumeweza kufika kule *site* na tumeona *development* kubwa sana ya ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Kwa kweli tunapongeza kwa sababu tumeona kazi zinazoendelea kufanyika pia tumeona fedha ambazo zinatolewa kwa hiyo binafsi tunawapongeza sana na tunaamini kama Kamati tumewaomba Wizara walisimamie na Bwawa hili liweze kukamilika kwa haraka zaidi. Kwa hiyo, tunaomba sana Wizara mlichukulie kwa umakini na kuhakikisha kwamba mwakani 2023 tuweze kupata *megawatt* 2,115 kutoka kwenye Bwawa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi changamoto ambazo tunazo leo tukipata megawati hivi kutoka kwenye hili Bwawa la Mwalimu Nyerere tutaongeza umeme mwingi sana kwenye Gridi ya Taifa. Lakini pia katika *master plan* yetu ya Taifa hadi kufikia mwaka 2025 tunatakiwa tuwe na umeme megawati 5000. Kwa hiyo hadi sasa hivi tunazo megawati 1,600 tukichukua na lile la Bwawa la Mwalimu Nyerere 2,100 maana yake tutakuwa na *around* 3,000 na *something,* lakini pia kutokana na hivi vyanzo mbalimbali tulivyonavyo tumeona kabisa tunakaribia 4,000 bado tuna upungufu wa megawati karibu 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaiomba Wizara ihakikishe kwamba vyanzo vinavyosababisha kuzalisha umeme wa ziada hasa kwenye gesi, lakini pia kwenye vyanzo vingine vya jotoardhi tuwekeze kule kwenye maeneo hayo ili tuweze kupata megawati za kutosha kwa sababu kuwepo kwa umeme mwingi utatusaidia kuhakikisha kwamba kunakuwa na uhakika wa upatikanaji wa umeme, lakini pia tutahakikisha kwamba hata miradi yetu mikubwa kama *SGR* inaweze ku-*operate* bila kuwa na kukatikakatika au kutokuwepo kwa umeme wa kutosha, lakini pia hata kusambaza kwa nchi jirani lazima tuwe na umeme wa kutosha kusambaza na kuwauzia nchi jirani ambazo zinatuzunguka kama Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi lakini pia Malawi ni masoko ambayo lazima tuyachukue kama Taifa na hasa ukizingatia mipango ambayo tunayo kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine Mheshimiwa Waziri nikupongeze tu, tunajua sasa hivi tuna changamoto kubwa ya mafuta katika soko la dunia, lakini pia kumekuwepo na upandaji wa bei ya mafuta duniani kote, tumeona changamoto hizi katika nchi kama

Marekani, lakini pia tumeona nchi kama Uingereza, lakini pia tumeona nchi kama Nigeria, pia wameweza kusimamisha ndege zao zisiweze kuruka kwa sababu ya changamoto hizi.  Ukiachilia mbali huko lakini hata hapa nchi jirani ya Kenya tumeweza kuona ndugu zetu wakibeba madumu kwenye pikipiki wakipeleka sheli kuweka mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo unaweza kuona kwamba tatizo hili si dogo, ni tatizo kubwa tuwapongeze tu Wizara kwa kuhakikisha kwamba mafuta yameweza kupatikana ndani ya nchi yetu, uhaba ambao tulitarajia kwamba tungeupata, tungekuwa katika vituo vya mafuta hakuna hilo halijatokea. Kwa hiyo binafsi ninawapongeza kwa kazi nzuri, tumepata changamoto ya upandaji wa bei ya mafuta, tunatambua kwamba bidhaa yoyote inapokuwa na mgogoro duniani ni lazima changamoto zitokee katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu haizalishi mafuta na sisi tunaagiza kwa hiyo tunapoagiza ziko hizo changamoto tunawaomba tu *PBPA* waendelee kusimamia uagizaji wa mafuta na mafuta haya yaendelee kupatikana isitokee nchi yetu ikakosa mafuta, zipo nchi tumezishuhudia zinapata uhaba wa mafuta kama nchi ambayo nimeitolea mfano ya Kenya, nchi inakosa mafuta, nchi inapokosa mafuta maana yake unaangusha uchumi wa nchi, lakini sisi kama Taifa nchi yetu haijakosa mafuta hilo tunakiri na mafuta yanapatikana hadi kwenye maeneo yetu ya vijijini. Changamoto ni bei ambayo tunaishukuru pia Serikali kwa kuweka fedha shilingi 100,000,000 kuhakikisha kwamba ina-*control* upandaji wa bei hili suala kwa kweli tunawaomba sana liendelee kusimamiwa kwa ukaribu na kwa umakini kwa sababu ikitokea tu tukakosa mafuta

kwenye nchi yetu ninaamini uchumi wa Taifa hili utaanguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hawa *PBPA* wamefanya kazi ambayo ni nzuri kwa sababu tumeweza kuona nchi kama Zambia, Malawi, Rwanda, Burundi na Uganda wanatutumia sisi kama Tanzania kwa kupitia hii *PBPA* kuingiza mafuta yao kwenye nchi zao. Kwa hiyo wangeweza kutumia nchi nyingine, lakini wametumia nchi yetu maana yake tuna utaratibu mzuri wa kuagiza mafuta katika Taifa letu. Changamoto zilizopo au zinazojitokea nyinyi kama Wizara mzisimamie kuhakikisha kwamba mnadhibiti changamoto hizo kwa sababu ikitokea tukaacha ikawa holela tunaweza tukapata mafuta mengine machafu, tunaweza tukapata mafuta mengine yakawa sio bora yakaua magari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii ndio ambayo imesababisha tulipotoka huko kuwa na magari ambayo yanaharibika, tumetoka huko kulikuwa kuna malalamiko hadi tumefikia hatua tumepandisha mafuta ya taa kufikia bei ambayo ipo sawa au zaidi ya petroli na dizeli ni kwa sababu ya kudhibiti uchakachuaji wa mafuta. Hivyo basi tunawaomba udhibiti uendelee kusimamiwa kwa ukaribu, lakini pia uadilifu uendelee kuwepo kuhakikisha kwamba bidhaa hii adimu katika taifa letu inaingia na wananchi wanapata kile ambacho wanastahili ili kuweza kuhuisha uchumi wa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimia Waziri katika hilo tunakupongeza, lakini uangalie changamoto zilizopo ili tunapoelekea tuweze kuziboresha na kuwa imara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine ambacho nilitaka nizungumzie Mheshimiwa Waziri gharama za

umeme katika maeneo yetu ambazo mlizitangaza hivi karibuni, lakini pia kwenye bajeti yako umeeleza kwamba utaunda Tume, itembelee maeneo yote nchini kuangalia bei za umeme. Nikushauri Mheshimiwa Waziri yapo maeneo ya kupandishwa kwa bei wakati mnapandisha bei mlivyosema tunapandisha basi hata ile bei ya zamani iliyokuwepo ikawa mmefanya *double* maana yake pale Igunga tulikuwa tunaingiza umeme kwa mita 30 shilingi 170,000; mlivyosema bei turudishe nchi nzima tulitangaziwa shilingi 27,000 ikashuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mlivyosema turudi kama zamani haikurudi ile shilingi 170,000 imeenda shilingi 320,000; kwa hiyo imekuwa tena gharama zaidi. Nikuomba Mheshimiwa Waziri haikuishia hapo, imeenda sasa hii bei hadi kijijini kwetu, kijiji cha Tomachankola na wao walipe shilingi 320,000, kijiji cha Nkinga na wao walipe shilingi 320,000, kijiji cha Simbo hivi kweli Mheshimiwa Waziri kweli vijiji hivi mnaenda kuwawekea shilingi 300,000 eti kisa tu wana kituo cha afya, eti kisa tu wana sekondari ya kata, eti kisa…

Mheshimiwa Waziri kuwa na sera ya kuwa na shule za sekondari za kata ni sera ya nchi nzima ni kwamba kila kata kuwepo na sekondari. Sasa isiwe adhabu kwa watu wetu, lakini pia kuwepo kwa vituo vya afya, tumepata fedha nyingi sana za vituo vya afya kwenye vijiji vyetu, kwenye kata zetu isiwe sababu ya kutuadhibu tukaenda kwenye bei ya shilingi 320,000. Nakuomba sana vijiji vinavyofanana na Chomachankola, Nkinga na Simbo visipelekwe kwenye hiyo bei, tunakuomba Mheshimiwa Waziri uturudishie kwenye shilingi 27,000 fedha hii tumeshaunganisha hii nchi umeme karibu maeneo yote hivi tunavyomalizia tumeshakula ng'ombe mzima

tumebakiza mkia, tusiende kwenye lawama ambazo hazina sababu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri rudisha kwenye vijiji vyetu bei ya shilingi 27,000; peleka kwenye makao makuu ya kata shilingi 170,000; peleka Manispaa paleka majiji lakini kwenye vijiji vinavyotambulika vijiji rudisha bei ya shilingi 27,000 kuhakikisha kwamba wananchi wanaweza kufurahia maisha yao.

Lakini nikuombe Mheshimiwa Waziri sisi pale Igunga umeme unakatika kama ambavyo maeneo mengine wamezungumza, lakini katika bajeti ambayo inatembea hii tuliwekewa kwamba tungejengwa *sub-station* ya kuweza ku-*supply* umeme pale Igunga. Lakini *sub-station* ile haijajengwa, tunaamini kwenye bajeti inayokuja tutapata hiyo *sub-station* ambayo ilikuwa imeshawekwa ijengwe pale Mbutu katika Wilaya ya Igunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba *sub-station* hii ijengwe ili kupunguza usafiri na usafirishaji wa umeme kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine umeme wa Igunga tunaupata kutoka Nzega yaani unatembea zaidi ya kilometa 150 kwenda kusambazia kufika Makao Makuu ya Wilaya, lakini pia kusambazia Wilaya nyingine zinakwenda mpaka Wilaya ya Uyui. Mheshimiwa Waziri hili suala kwa kweli kama ndio Igunga inafanyika hivi na maeneo mengine katika nchi ipo hivi maana yake ni changamoto kubwa sana na uhakika wa umeme hauwezi kuwepo kama hatutojenga *sub-station* kwenye maeneo haya nikuombe sana *sub-station* ijengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Mheshimiwa Waziri sisi katika *line* hiyo kunapita nguzo zinapita kwenye majaruba na mji ya Igunga nguzo zinapita kwenye

majaruba sio Igunga peke yake naamini maeneo mbalimbali katika nchi hii ambako nguzo zinapita kwenye majaruba, matokeo yake ni nguzo kuanguka kipindi cha masika, lakini pia kukatika kwa umeme, Mheshimiwa Waziri tuletee nguzo za zege, maeneo yote yenye majaruba weka nguzo za zege ili wananchi wawe na uhakika wa kupata umeme kiangazi pamoja na masika. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Gulamali kengele ilishapigwa.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Charles Poul Mwijage, Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mheshimiwa Vita Kawawa wajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuhutubia bajeti ya kimataifa, unajua kuna bajeti ile ya wananchi, ilipita ile bajeti ya kitaifa, sasa hii ni ya kimataifa kwa sababu mambo yake ni dola, ni *geopolitical,* sijui ni migogoro ni Ukraine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilihudhuria maonesho ya nishati, lakini nimesikiliza vizuri hotuba ya Mheshimiwa Waziri na nimeisoma na viambatisho hivi, napenda nikiri kwamba kuna majibu mengi hapa kuliko maswali niliyonayo kutoka kwenye maonesho na kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, lakini kabla sijaanza kuhutubia

nizungumze jambo moja; mwezi Januari, 2018 nilipata bahati ya kuhutubia Kabare, Uganda; Mheshimiwa Rais Jenerali Kaguta Museveni aliniomba nihutubie tena nihutubie kwa Kinyankole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuwepo Mheshimiwa Dkt. Kalemani, nikahutubia lakini Wizara ya Nishati wakanikaribisha Bunazi walikuwepo watu wengi na watu kutoka Nzega walikuwepo na kutoka Tanga walikuwepo na baadhi ya Wabunge, sikuona mahali popote ambako watu wa Uganda na Tanzania wanalalamika kwamba bomba la mafuta la kutoka Hoima kwenda Chongoleani lina matatizo, wala mimi katika Jimbo langu sijawahi kuona mahali watu wanalalamika kwamba watafukuzwa. Sasa hao wanaokwenda kutusemea huko Ulaya wametumwa na nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafuta ni ya Uganda, bomba ni la Tanzania; sisi na Uganda ni ndugu, mimi Rais wa Uganda Msita Waitabara ni mjomba wangu na alikuwa anaishi Jimboni kwangu kabla hajaenda kuwa Rais wa Uganda ni ndugu, kwa hiyo, watuache watuache. Lakini wale watu wanaosema bomba lisijengwe nimewapenda kitu kimoja, wanasema tupande miti bilioni tano, mimi ninakubali waje tutawapa eneo watupandie michikichi, watupandie mibuni, watupandie majani ya chai; miti bilioni moja sisi tutakwenda kuvuna wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye nishati; kwenye maonesho nashukuru kwa umeme visiwani *off grid* watu wa Mazinga, Ikuza, Kerebe, Gumbire, Nyaburo na Goziba suala la umeme nimepata majibu, lakini nimepata majibu kwamba *REA II* iliyokwama vijiji vya Busingo, Ruwanda yote itakuwa haina matatizo na miradi

yote ya *TANESCO* itatengenezwa, nishukuru kwenye hotuba Mheshimiwa Waziri umekumbuka suala la *campsite,* vituo vidogo vinavyoondoa matatizo ya *distribution* ya mafuta, nashukuru Mheshimiwa Waziri ulikuwa Mwenyekiti wangu kwenye Kamati zetu tulilijadili sana sasa upele umepata mkunaji, ulishughulike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe jambo lingine umesema magari ya Wizara ya Nishati yatafungiwa gesi, mimi sikubali, magari yote ya Serikali yaanze kutumia gesi, zipo faida za kutumia gesi, gesi *is economical,* gesi *is available,* waanze kutumia gesi hiyo nimeisoma kwenye hotuba yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumze mambo ya kidunia; suala la mafuta na mwenendo wa mafuta duniani; hili tunaomba uelewa Watanzania wote muelewe suala la mafuta halimhusu Mheshimiwa Rais wala halimhusu Waziri, wala halimhusu Mkurugenzi, ni suala la kidunia, sina muda ningezirudia zile sababu tano zinazosababisha hivyo, zipo nje ya uwezo wetu, na ninapozungumzia hiyo suala la uelewa nipende kuishukuru Serikali na hasa hasa Mheshimiwa Rais, kimsingi hoja sio bei ya mafuta imeshuka, bei ya mafuta haijashuka, bei ya mafuta imeshushwa, ukiangalia kwenye soko la dunia na nilikutana na mtaalam mmoja nilikuwa naangalia bei ya dunia inapanda, ila mamlaka imeshusha bei angalau kwa siku mbili hizi tupate afueni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uelewa wa Watanzania muelewe huko bado vumbi linatimka, bei ya mafuta inaendelea kupanda, ila mamlaka imeamua bei ishuke na hiyo ninaiita zawadi namba tatu, zawadi ya mama na hii ni zawadi ya mama namba tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze suala moja muhimu ambalo watu hawalielewi katika somo la mafuta; *petroleum business management introduction* huwa tunafundishwa *availability, reliability* na *availability of* mafuta ndio tunafundishwa. Sasa katika suala la *availability* kuna kitu Watanzania hatukijui, ni siri iliyo wazi kwamba sisi tunapata umeme asilimia 60 inatokana na gesi ya Songosongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama isingekuwepo kutokana na vyanzo vya maji kutotosha tunge-*import* mafuta, kama ingetokea tatizo la *supply/ disruption of supply* ina maana tungeingia gizani mnasema mafuta yamepanda watu wanapiga kelele nawaambia Mungu apishe mbali ikitokea tatizo la umeme *60 percent* kila mtu atatafutana. Kwa hiyo, tuipongeze Serikali, tuishukuru Serikali kwa kuwezesha hii gesi na tunapoishukuru gesi lazima uwakumbuke waasisi akina Sylvester Barongo na vijana wake wakati ule akina Mzee Ntomola, akina Kilagani, akina Khalifani na hapo ndipo ninapoipongeza Serikali ya Mheshimiwa Samia kwa kuwarudisha wakongwe kwenye sekta yaani uwarudishe wakongwe waje wakuoneshe njia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikuwa rahisi kuchukua gesi ya Songosongo, sasa niwaambie kama sisi leo tungeingiza mafuta kwa bei hii, tungetumia trilioni moja kuagiza mafuta ya miezi minne; trilioni moja kuagiza dizeli ya kuendesha mitambo, sasa hoja sio trilioni moja, hoja ni kwamba *foreign currency* ungeipata wapi. Kwa hiyo wakati tunashukuru punguzo la bei huku kushuka kwa bei tushukuru kwa kuwepo na mfumo wa gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze *bulk procurement; bulk procurement* watu hawaielewi, Tanzania haijawahi kuwa soko la mafuta na nilikuwa nikilisema Tanzania haijawahi kuwa soko la mafuta, huwezi kumwambia *international trader* kwamba unataka tani 10,000; tani 5,000. Sasa hivi kutokana na *bulk procurement consolidation* ya maziwa yote makuu, mahitaji kupitia Dar es salaam sasa dunia inatambua kwamba Tanzania kuna soko la mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tunashika mpini wao wanashika makali, watakuja hapa, watakuja hapa, sasa kwakuwa na wingi wa mafuta kama walivyosema Mbunge wa Manonga ndio maana hata mtikisiko unaompata *South Africa,* unaompata Nigeria, unaompata Kenya hautupati sisi na hiyo ni siri Waziri anajua na nasema Waziri usiisema kwa sababu tupo *live* watu wengine watakuja kuiba *style* yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatuwezi kuadimika mafuta kwa sababu ya mfumo wetu, asije mtu akakwambia rahisi, *what is* rahisi? Hakuna kitu *cheap*, *cheap* lazima kiwe *pegged,* kiwe *pegged* kwenye *international* kuna watu wamekwenda kuagiza mafuta *cheap* fedha zimeliwa, fedha zikiliwa za Serikali utamwambiaje *CAG,* hili Bunge utaliambiaje, lazima tufuate mfumo unaojulikana kama tunapata ya aghali tupate aghali, tuvumilie kesho tutapata nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine nataka kuzungumzia ni *trading hub*, kidogo na hii nazungumza taratibu Mheshimiwa Waziri wasije wakawepo watazamaji kwingine kule, shangazi yangu nikamsalimia akakataa kuniitikia, kuna tofauti kati ya *strategic reserve* na *trading hub*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ningeomba mlete mjadala, mlete semina sijakubaliana nalo. *Strategic reserve* inaweza ikawa ni *trading hub* na ninakupongeza umekubali kwamba tuweke *bonded warehouse,* sasa zitumie zile *bonded warehouse* ku-*re-export* kwenye *enabling countries,* nchi za Kongo kwenye madini kuna watu wanaweza kununua lita 500,000 kwa mpigo, waambie waje Tanga wanunue, waambie waende Dar es Salaam wanunue, nilikuwa nikifanya kazi hiyo unajua, tuna *push volume*. Kwa hiyo tuigeuze Tanzania soko, wanapokuja vijana wetu watapata kazi, lakini ile amari iliyopo kwenye ghala letu ndiyo hiyo *strategic reserve*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwambia Mheshimiwa Waziri akatikisha kichwa, tunahitaji mjadala tukae Wabunge tujadiliane na utaratibu utazingatiwa kusudi tunyukane hapa, kwa sababu hatuwezi kukubali hili suala lipite lina uzuri na ukali wake. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya juzi wamefanya mjadala juu ya hili walitoka bila kuelewana, *OTS* walikuwa na mjadala juzi walitoka bila kuelewana. Mambo ya *aging,* mambo ya kukamatwa na mafuta ya bei kubwa yakashuka, kwa jirani yameshuka wewe una mafuta ya bei kubwa utafanya nini, tunapaswa tuelezane kwa nia nzuri inayofanywa tutoke tumeelewana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine Tanzania tunayo *storage capacity* ya 1.4 *billion liters* kwa mwaka tunayotumia tuna *storage capacity* hiyo, *89 percent* ni *private sector,* ninaiomba Serikali msiiache *private sector,* ndio iliyotufikisha hapa, hamasisha *private sector*

wawekeze, Serikali weka uratibu, weka wadhibiti waweze kuelekeza. *(Makofi)*

Suala jingine naomba la utafutaji na uchimbaji wa mafuta, nishukuru unao wataalam Mzee Khalifani bosi wangu amerudi, tutafute mafuta mambo ya kuogopa *ASPA* sijui nini hakuna, usiogope lazima utapoteza na katika kupoteza utapata, hii ni biashara ya stara kubwa, ni biashara ya gharama kubwa, kwa hiyo, tuhamasishe kutafuta mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sasa siyo siri kwa sababu ya kupanda kwa mafuta nchi za Ulaya wanakimbilia Afrika tumesikia hapa Afrika Magharibi, tungependa kusikia wanakuja Tanzania na wakija wape masharti, tunao vijana wamesoma hapa wamekwenda China wakasoma *petroleum,* mradi wa gesi haukufanya kazi waajiri watoto wale, waingize kwenye sekta ndio masharti kwamba njoo uwekeze, wekeza vijana wa Kitanzania waweze kufanyakazi, tafuteni mafuta, wakati wanatafuta *green energy* ni hadi 2050 sasa 2050 na sisi tutumie ndiyo maana na ninamuambia mjomba asikie huko aliko Kampala na Entebe tunataka mafuta ya Uganda yapite Tanga kusudi Tanga wafaidi na njia yote tufaidi, tufaidi na sisi tuchome gesi kama wazungu walivyochoma wakati sisi tumelala. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Venant Daudi Protas, atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Festo Sanga na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika wajiandae.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nichangie Wizara hii muhimu kwa uchumi wa Taifa letu, Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuipongeza Serikali angalau ilitoa ahadi ya tarehe mosi leo mwezi wa Sita wananchi wetu watapata ahueni ya kupungua kwa bei ya mafuta, sasa Serikali imechukua *gape* lile, wananchi wameona kidogo imepungua ingawa haijapungua sana, lakini angalau Serikali imeonesha njia na nina imani tunapoenda tutaendelea kupunguza zaidi kupitia Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa nitachangia mambo machache sana kwa upole sana ili Mheshimiwa Waziri kwa sababu ni bajeti yake ya kwanza na ametuandikia hapa jarida limetupa vipaumbele na hivi vipaumbele nina imani kavitoa katika Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi, naamini kama akivisimamia kama alivyoandika mwaka kesho hapa bajeti yake haitokuwa na maswali mengi lakini kama havitakwenda kama alivyoandika basi na yeye kidogo awe amejipanga mwakani atumie nguvu kuipitisha bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumpongeza wiki iliyopita alituletea watalaam wetu hapa wa wilaya na mikoa na wakandarasi wote. Tulipita kwenye mabanda kama mlivyokuwa mmeelekeza tuliwakuta mameneja wetu wa wilaya na mikoa na wakandarasi na nikushukuru kwa sababu kwa sisi wengine jimbo letu ni mbali sana na kufika Makao Makuu ya Wilaya, Meneja wangu Grace nilimkuta hapa na nikaongea nae na wakandarasi nikaongea nao, wakanipa ushikiriano mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo siku ile mlivyotuletea hapa nilijikuta tuna maswali mengi. Wakati tupo *site* hawajaja hapa tulikuwa tunajua kuna changamoto ya upandaji wa bei ya vifaa vya ujenzi, lakini hapa tena tukaja kukuta mkandarasi mwenyewe na aliyempa ajira yule yaani *REA* hawaelewani, lakini niliweza kusaidiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri ndugu yangu Mheshimiwa Byabato, alimwita mkandarasi na *REA* wenyewe wakaitwa kuzibaini zile changamoto baina yao za kimkataba, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri alitoa maelekezo pale wakakae kikao, alisema jioni wakae kikao, lakini mpaka leo kikao hakijafanyika na mgomo upo palepale, mkandarasi ameshindwa kuelewa kwa sababu *REA* anampa maelekezo ambayo yapo nje ya mkataba wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe hata ile niliyokuwa nawaambia wananchi tusubiri wanasema wana- *bargain* bei za vifaa kumbe nilikuwa nawadanganya kumbe ni tatizo la mkandarasi na *REA* hawajaelewana ndiyo maana kazi imesimama jimboni kwangu. Hata hivyo, nikumbushe mwaka jana 2021 Mheshimiwa Naibu Waziri alifika jimboni kwangu waliahidi Kijiji cha Izumba watawasha umeme baada ya mwezi mmoja, lakini sasa hivi mwaka mmoja na miezi miwili hawajawasha umeme. Nilivyokuja kufuatilia kwa mkandarasi, kuja kumhoji hicho, akaniahidi mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Julai, maeneo ya Songambele, Izumba yatakuwa yamewaka umeme, lakini kwa mgogoro huu kama tusipoutatua mapema mpaka muda huo umeme utakuwa haujawaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa kuwa alituletea wataalam wenyewe, yale maswali yote yaliyoibuka, akae na wataalam wake,

wakusanye maoni yote ya Wabunge ambayo tuliyaongea pale wakayafanyie kazi kuliko sasa, walituambia saa kumi watakaa kikao, leo tunaenda siku ya tano au ya sita hawajakaa kikao. Sasa ndiyo Waziri ajue ana watu gani ambao anafanya nao kazi kwa sababu yeye ameingia mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kampuni inaitwa *JV POMY* walimpa kazi ya kuunganisha umeme, amechukua hela za wananchi wangu, ameondoka LUKU hataki kuwaletea, wakimpigia simu sababu ni nyingi. Niombe kwa sababu zipo LUKU zaidi ya 120, tutoe kauli nini kilicho nyuma ya pazia juu ya mkandarasi huyu je, ni uzembe wake au kuna tatizo gani ambalo limemkumba? Kama kuna tatizo, basi wananchi wapewe taarifa kuliko sasa hela zao zimekaa kule halafu hawajui lini wataunganishiwa umeme. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atusaidie hili hii Kampuni ya *JV POMY* ndio ilitusababishia hata hasara kwa ndugu yangu jirani yangu Mheshimiwa Kakunda, eneo la Makibo umeme umechelewa sana kwa sababu ya uzembe tu na ucheleweshaji mdogomdogo ulionao hii kampuni. Nimwombe Waziri aipitie vizuri, ikiwezekana wampunguzie kazi sehemu nyingine kwanza kumwezesha kumaliza kazi za mwanzo ili kuondoa kelele na lawama kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nichangie, nilishamlilia Mheshimiwa Waziri na nikamwambia hatujapinga maelekezo ya Serikali kupandisha gharama za umeme, tumemuunga mkono, lakini tunacholia maelekezo ambayo aliyoyaleta walisema vijiji vitaendelea kuwa Sh.27,000 lakini maeneo ya miji itakuwa Sh.320,000 na kwingineko, lakini kwangu kuna vijiji vimeingizwa kwenye Sh.320,000 havina sifa ya

kuingizwa huko kikiwemo Kijiji cha Goweko, Kijiji cha Igalula, Kijiji cha Kigwa na Nsololo Tambukareli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atoe kauli moja, wananchi wana hamu ya kuunganishiwa umeme na wao kama wangewaletea wakati ule wangeunganisha mapema, tatizo Serikali yetu ilikuwa inaleta kidogo kidogo, sasa wakati Serikali imefungua kupeleka umeme kwenye vitongoji, leo wanawapandishia bei wanaenda kumuunganishia nani, lakini tunakumbuka bei haikuwa hiyo ilikuwa Sh.170,000 basi wangerudisha hata ile Sh.170,000 kuliko sasa hivi imepanda, ukinunua nguzo moja unalipa mpaka zaidi ya 1,700,000 mpaka 2,000,000, kwa Mtanzania gani na uchumi gani? Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri aweze kutusaidia jambo hilo ili tuweze kulitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Igalula lina vijiji 46 havina umeme, lakini juzi Mheshimiwa Waziri alitoa takwimu tatizo ambalo saa hivi wanaenda kulitatua kusafirisha umeme kwa umbali mrefu, ninavyoona kuna umeme nautoa Igunga unakuja jimboni kwangu kwenye Kata ya Loya, umeme ule umekuwa na changamoto sana, unakuja mdogo, wananchi hawafanyi kazi, mashine moja ikiwaka mashine zingine zote haziwaki na wananchi hawapati huduma nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe katika utekelezaji wa miradi, tulikuwa tunaomba muweze kujenga Kituo cha Kupozea Umeme hasa katika Kata ya Kigwa, itatusaidia sana kwa sababu vile vijiji 46 kama umeme kweli tukiuchukulia katika Kata ya Kigwa kama walivyo-*plan* sasa hivi, basi katika vile vijiji vyote kutakuwa kuna tatizo kubwa la umeme kwa sababu umeme unasafiri zaidi ya kilometa 200, kilometa 300 na huko

ulipotoka zaidi ya kilometa 800 au 900 sasa unauongozea 200, huku kwenyewe bado unatusumbua unakatikakatika, unapoenda kuuongezea tena 200 zaidi, utaendelea kuwa na matatizo badala ya kwenda kutatua tatizo ndiyo tunaenda kuongeza kelele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wafanye tathimini waweze kuongeza Vituo vya Kupozea Umeme, pale Kigwa tutampa eneo nadhani tuna maeneo makubwa ili waweze kujenga kituo chao cha kupozea umeme na baadaye twende tukausambaze katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linaloendelea sasa hivi, tumekuwa na *plan* za muda mfupi, sasa hivi wakandarasi wapo *site,* tunapitisha nguzo za miti kwenye majaluba, anajua kabisa hili ni jaluba, lakini saa hizi watalaam wa *REA* wapo, *TANESCO* wapo, mkandarasi yupo, umeme unapitishwa kwenye jaluba, baadaye masika inakuja nguzo zinakuwa kwenye maji zinaanguka, halafu baadaye wanasema tunaomba fedha za *maintenance,* kwa nini wasitengeneze mapema nguzo za zege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri waangalie maeneo yote ambayo yana matatizo ya kujaa maji, basi tuanze kugundua mapema wakandarasi wapo kule kama hawayajui hayo maeneo, Viongozi wa Vijiji wapo, Viongozi wa Dini wapo, wawashirikishe watawaambia hapa maji yanajaa wakati gani, hapa maji hayajai. Kama ile *route* imelazimika ipite palepale, waweke nguzo za zege ili kuweza kusaidia wananchi wetu. Kwa hiyo, kwa mwaka huu yangu ni hayo machache kwa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kama ushauri, niipongeze Serikali wanaendelea na harakati nzuri za ujenzi wa bomba la mafuta, lakini tulishauri bei ya mafuta inaongezeka hasa Mikoa ya Kagera, Kigoma kule kwa sababu bei ya Dare es Salaam unakuta shilingi 3,100 lakini Kigoma ukienda shilingi 3,600 au shilingi 3,700, lakini wakija kuuliza kwa nini tunatofautiana na Dar es Salaam kitu ambacho kinachosababisha ni kwa sababu kule ni mbali *depot* zipo Dar es Salaam, tunaongeza *cost* za *transport*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri tulishauri kwenye Kamati, lakini tuendelee kushauri kama sisi wawakilishi wa wananchi, katika Mradi wa Bomba la Mafuta kwa kuwa tumeliunganisha kutoka Uganda mpaka Tanga, palepale tujenge bomba letu lingine tena ambalo litarudisha mafuta mengine ambayo yatasaidia Mikoa hiyo ya Kanda ya Ziwa. Leo meli ikipaki Tanga tuweze kufungua mafuta Tanga tukaweka *depot* pale Nzega au Bukene, yakaweza kuja magari ya Mwanza yakawa yanachukua pale, magari ya Kigoma yakawa yanachukua pale tutasaidia sana kupunguza bei, lakini vile vile tutasaidia kupunguza mlundikano wa magari kwenda Dar es Salaam. Kwa hiyo, tukiweka vituo vyetu vya Serikali na bomba likawa la Serikali, gharama itakuwa ni *cheap* ingawa tutaweka tozo kidogo. Kwa sasa hivi kwenda Mwanza ni zaidi ya Sh.150 hadi Sh.170, lakini ukiweka pale kutoka Mwanza kuja Bukene wakachukua mafuta pale watachukua kwa Sh.50 ile nyingine itakuwa *cost* ambayo tumemsaidia mwananchi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kauli kwa kusema naunga mkono hoja kwa sababu mabanda yalikuja, majibu mengi niliyapata. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Venant Daud Protas. Nilimwita Mheshimiwa Vita Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Sanga, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere wajiandae.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa. Kwanza naungana mkono na wenzangu kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara na Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO*, *EWURA* na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri mnayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Wizara kwa maana ya Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Waziri kwa dhamira ya dhati ya kuongeza nguvu ya umeme na usambazaji wa umeme na utayarishaji, kuanzisha umeme katika maeneo mbalimbali ambayo kwa ujumla wake watakaoweza kuzalisha katika mwaka huu bajeti 2022/2023 *megawatts* 1,466 lakini zilizopo mbioni kwenye kukamilika ni *megawatts* karibu 2,380 ambayo ni Nyerere *Hydro power*, Rusumo *megawatts* 80 na Kinyerezi 185. Jumla yake zikikamilika na kwa sasa tuna *megawatts* 1,694 tunazozalisha kwa maji na gesi na *biomass megawatts* 1,694, jumla yake tutakuwa na *megawatts* 4,075.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tulivyo *megawatts* 1,694 na matumizi ya juu kabisa ya umeme nchini ni *megawatts* 1,335. Kwa hiyo, hapa tukijumlisha na miradi hii iliyopo na ukaenda kukamilika nadhani mwishoni mwa mwaka huu na mwakani tutakuwa na *megawatts* 4,075, lakini tutakuwa na *surplus* ya umeme ya *megawatts* 2,740. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu, sasa hivi tukishakamilisha hii miradi tu-*concentrate* katika kazi ya kusambaza kwa maana ya kusafirisha na kusambaza umeme na ile kufanya ile kazi ya *National Grid* Stabilization *Project*. Tukishamaliza miradi hii ya kuzalisha umeme, tutakuwa na *megawatts* 4,755, fedha nyingi tuzielekeze huko kwenye kusafirisha, kusambaza na *stabilization* za *grid* kwa sababu tutakuwa na *surplus* ya 2,740. Kwa hiyo, nadhani sasa hivi tukiendelea na *concentration* ya eneo hili itatusaidia sana kuwafikia wananchi vijijini ili waweze kufikia vitongoji vile tu-*concentrate* kwenye kukopa kwenye umeme wa kusambaza kwa wananchi vijijini badala ya kuendelea ku-*invest* kwenye uzalishaji wa umeme kwa sababu tutakuwa na *surplus* kubwa ya umeme katika kipindi hiki mpaka hapo tukiona hitaji linazidi kuongezeka basi tuendelee pamoja na kwamba *policy or electric supply industry reform* ile *strategic road map* inatutaka mpaka 2025 tuwe tunazalisha *megawatts* 10,000, lakini kwa sasa hivi mimi nadhani tukishafika hapo tu-*concentrate* na usambazaji na *stabilization* ya umeme vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, namshukuru Waziri walivyoleta timu yao hapa na nikaenda kuzungumza nao na wakanielewa, tuna *proposal* ya *additional villages* ambavyo vilirukwa katika vijiji vyetu na maeneo, tuna maeneo ambayo niliyasema ya maji. Serikali ina-*invest*

fedha nyingi sana kwenye vituo vya maji, kwa maana visima kwenye vyanzo vya maji, lakini hakuna umeme katika vile vyanzo vya maji, tunatumia nishati ya mafuta ambayo ni *very expensive*. Kwa sasa hivi katika vijiji vya kwangu kule kwa mfano Ligunga, Lusewa wanalalamika na wanagoma kulipia kwa sababu wanashindwa kumudu gharama ya mafuta ili kusukuma maji yaweze kusambazwa. Kwa hiyo, ni vyema Serikali waka-*concentrate* sasa hivi kupeleka umeme katika maeneo ya vyanzo vya maji, kwenye vitongoji vyenye shule, zahanati na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana kwangu na vijiji na maeneo ya Ligunga pale nilishaeleza nilikubaliwa kwamba utashushwa umeme, kuna Sasawala Sekondari ambako kuna *water pump* pia, kuna eneo la Kijiji Zanzibar, Mchanjira, Likuwi *Water pump, Selous Camp*, *Selous* Sekondari, Vitongoji vya Mfuate, Rukimwa na Semu Zahanati, *Magazine* Sekondari lakini pia tuna Kituo cha Jeshi pale hakina umeme na kuna sehemu wana *pump* nazo hakuna umeme. Kwa hiyo, tutashukuru sana maombi yangu yale yakienda kutekelezwa ili tuweze kufanya kazi yetu ikiwa njema ya kusambaza maji na wapate huduma iliyo bora ya umeme. Nina imani sana na Waziri na Naibu Waziri kwa ubunifu wao, usimamizi wa kazi zao, tunaamini tutafika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, sisi katika *East* Afrika hapa kwenye suala la mafuta, Uganda mafuta wao kwa bei ya Tanzania ni Sh.3,468, Kenya baada ya ku-*subsidize* ikashuka mpaka Sh.3,001, sisi Tanzania Sh.3,148 na leo hii bei imeshuka naamini itakuwa imefika 3,000 kwa bei. Kwa hiyo, tupo vizuri na hii *crisis* iko dunia nzima, tuendelee kuwa wavumilivu, naamini kabisa Waziri na timu yake na *EWURA* wataendelea kuratibu vizuri suala hili la mafuta

kwa nchi yetu. Hata hivyo, lazima tumshukuru Rais wetu kukubali kutoa bilioni 100 ambayo leo hii hapa kwetu bei imeshuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Watanzania tuendelee kuwa wavumilivu na tukiamini kwamba Serikali yetu imara ipo na inawajali wananchi na tutaendelea kuhakikisha kwamba tunasimamia vizuri bei hizi za mafuta. Kwa kushuka kwa bei ya leo naamini katika nchi za Afrika Mashariki tutakuwa chini zaidi. Kwa hiyo, nawaomba sana Wizara, Mheshimiwa Waziri waendelee kusimamia hivyo hivyo, waendelee kusimamia ule mfumo wa *bulk procurement* ambao unatuhakikishia kuwa na mafuta ya kutosha katika mwezi mzima na kidogo na tunaweza tukawauzia na wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ulikuwa huo, nakushukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vita Kawawa. Tunaendelea na Mheshimiwa Festo Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere na Mheshimiwa Tumaini Magessa wajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Nishati. Kwanza nipende kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Mama yetu mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo ameifanya hadi leo mafuta yamepungua bei. Watanzania wafahamu mafuta si kama yamepungua bei, yameshushwa bei na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. Pia niwapongeze wataalam wa Wizara na nampongeza Mheshimiwa

Waziri, kwa kuwa *smart* kwa sababu hata kutuletea *REA* na *TANESCO* ndani ya Bunge ni kuonyesha jinsi gani ambavyo anatamani matatizo ya Wabunge yaweze kutatuliwa papo kwa papo, tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo ya kuchangia kwenye vipaumbele vyako 12 ambavyo tunavyo hapa, ninaweza nikaanza na kipaumbele Namba Moja, Namba Mbili na Namba 12 ndivyo nitakavyovizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele Namba Mbili, Mheshimiwa Waziri umezungumzia kuhusu kutekeleza miradi ya nishati vijijini pamoja na kuanza utaratibu wa kupeleka umeme katika vitongoji vyote nchini. Mheshimiwa Waziri nizungumze wazi, utekelezaji wa *REA* kwenye sehemu kubwa ya Majimbo kipindi cha nyuma haukuwa mzuri sana. *At least* Makandarasi wa sasa japokuwa nao wapo wanaosuasua ila kwa Jimbo la Makete Mkandarasi wa sasa anaunafuu, lakini wale waliopita wana changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunalitekeleza hili, kabla hatujaenda kwenye kuangalia vitongoji, tufanye sensa ni Watanzania wangapi wamesuka nyumba kwenye Taifa hili na hawajaingiziwa umeme hadi sasa. Kwa sababu gani, umeme huu umeishia sehemu kubwa kwenye vituo vya afya na maeneo mengine. Watanzania wengi wamejitoa kwa moyo kusuka umeme toka mwaka 2019, 2018, 2020 lakini hadi sasa hawajaingiziwa umeme. Hao wangepewa *special task* kuangalia jinsi gani tunaweza tukawasaidia, wakaweza kupata umeme kwenye Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni maswali tukienda Wabunge kwenye mikutano wanauliza, mimi nimesuka Mheshimiwa Mbunge umeme utafika lini? Mimi nimesuka umeme utafika lini? Tunaomba sana mfanye sensa kwa Mameneja wetu wa Mikoa watuambie. Kwa mimi Makete tu nina kijiji cha Mago, na kijiji kama cha kule Matamba na vijiji kama vya Lupalilo, hivi vyote vinawakazi takribani zaidi ya 2,000 hadi 3,000 wamesuka umeme lakini hawajaingiziwa. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri kwenye jambo kama hilo uweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Makete tunalo Bwawa la Umeme la Mto Lumakalya. Ninyi mnaita Lumakalya lakini sisi ni Mto Luvanyila. Hili Bwawa la Mto Lumakalya ni bwawa ambalo linaenda kuzalisha zaidi ya megawati 222. Lakini pili tuna bwawa la Mto Luhuji, zaidi ya megawati 300, kwa maana kwamba megawati karibu nusu zinazotumika kwenye Taifa hili zinaweza zikaenda kuzalishwa ndani ya Mkoa wa Njombe. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri, nimeona kwenye bajeti umenitengea Bilioni Nane, imani yangu ni kwamba hii Bilioni Nane ni kishika uchumba tu kwa sababu mradi una zaidi ya Bilioni 787 thamani yake. Kwa hiyo, ninaamini hii Bilioni Nane ni ya kuanzia tu. Nikuombe, wananchi wetu wamekuwa *stranded* kwa muda mrefu hawajui mradi unaanza lini. Pili tathmini ya gharama ambazo wananchi wanazunguka bwawa lile la Mto Lumakalya inafanyika lini ili wananchi wetu waweze kupewa fidia na waweze kupata fedha ambazo zitatokana na fidia za maeneo yale. Ninaomba sana huu mradi uweze kuanza, utakuwa umeandika Mheshimiwa January Makamba. Ninakuomba sana sana sana. Hii miradi miwili ikisimama inaweza kutusaidia sana katika kuondoa *gap* la umeme kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ninalotaka kulizungumzia Mheshimiwa Waziri ni kwenye Mikoa na maeneo kadhaa ambayo Serikali inatumia fedha nyingi kununua umeme na kuwapa umeme na wengine hawatumii umeme. Tunatumia fedha nyingi za Serikali kuhakikisha kwamba wanapata umeme. Kwa mfano, nizungumzie, tuna Mkoa kama wa Kigoma Mheshimiwa Waziri. Mkoa wa Kigoma wanatumia kwa mwezi 1.4 Bilioni kununua mafuta kwa ajili ya kuendeshea Mkoa ule umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba gridi ya Taifa iweze kwenda Kigoma. Wakati Serikali inatumia Bilioni 1.4 kununua mafuta, *return* yake ni chini ya Milioni 800. Kwa hiyo, tunatengeneza hasara zaidi ya Milioni 700 kila mwezi kwenye Taifa hili kwa ajili ya Mkoa wa Kigoma. Ni lazima uangaliwe kwa jicho la karibu Mkoa wa Kigoma ili tuondokane na hii *debt* ambayo tunaitengeneza kila siku ya kupoteza Milioni 800. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda Mkoa wa Kagera mimi nilikuwa Kagera juzi. Mkoa wa Kagera tunanunua umeme kutoka Uganda, megawati 10 tunanunua kutoka Uganda. Lakini megawati tano zinatumika na kiwanda cha Kagera *Sugar.* Megawati tano ndiyo zinatumika na Mkoa wa Kagera. Tunatumia zaidi ya Bilioni Moja na Milioni Mia Mbili kwa mwezi kununua umeme kutoka Uganda. Miundombinu ile siyo ya kwetu, ni miundombinu ya kutoka Uganda. Wakati huo huo pale tuna uwezo wa kutoa umeme Nyakanazi na tukapeleka Kagera na watu wa Kagera wakawa wameondokana na tatizo la umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, Kiwanda cha Kagera *Sugar* wanao uwezo wa kuzalisha zaidi ya megawati 25 na waka-*supply* kwenye Mkoa wa Kagera. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri zungumza na watu wa *Kagera Sugar* waweze kukusaidia jinsi gani ya kutatua na uzuri mitambo wanayo, wanachokwama ni sheria za nchi zinawazuia kuwauzia umeme watu wa gridi ya Taifa, lakini hapo anao uwezo wa kukupa megawati 20 na ukatatua tatizo la kununua umeme Uganda ambapo tunapoteza *over 1.4 billion, 1.2 billion* kununua umeme. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Mkoa wa Katavi tunanunua umeme kutoka Zambia. Tunatumia *over 1.5 billion* kununua umeme kutoka Zambia, lakini watu wa Katavi na Sumbawanga wanao uwezo wa kupata gridi ya Taifa ili tukaondokana na fedha hizi nyingi ambazo tunatumia kununua umeme kutoka nje. Ninakuomba Mheshimiwa January Makamba, imekuwa ni muda mrefu Mikoa hii wanahangaika na umeme, tunaomba utusaidie, Watanzania hawa wapate umeme wa ndani na hizi fedha ambazo tunapeleka kwenye Mataifa mengine tuweze kutatua changamoto za Watanzania ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha Mheshimiwa Waziri, nenda pale kwenye mgodi wa Geita *Gold Mining*. *Geita Gold Mining* wanatumia mafuta, hawatumii gridi ya Taifa na sijajua ni mchezo gani unaendelea. Kwa sababu wanapata *exemption* kwenye mafuta, wanaingiza mafuta hawataki kuingiza gridi ya Taifa kwenye mgodi wao. Ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri…. *(Makofi)*

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aah ananikata upepo huyo…

**T A A R I F A**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natambua mchango mzuri wa Mheshimiwa Sanga, lakini Geita tayari kuna *substation* ambayo imekamilika ina megawati 98 ina mwaka mzima na laini ya umeme ilishaingia mpaka mgodini lakini hawajaanza kutumia umeme kwa kisingizio kwamba umeme ule hauko *stable*. Kwa hiyo, ni muda muafaka Mheshimiwa Waziri kuwasimamia wa-*stabilize* umeme kuokoa gharama ambazo wanazitumia kwenye mafuta ya *diesel*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga unapokea hiyo taarifa?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napokea taarifa yake na ndiko nilikokuwa naelekea, kwamba Mheshimiwa Waziri watu wa Geita *Gold Mining* ule mgodi unatumia mafuta. Mafuta ambayo wanayatumia ndani ya mwezi wanatumia mafuta ya Bilioni 3.3 ambayo yana *exemption* ambayo kodi hiyo ingeweza kuingia Tanzania na ingetusaidia Serikali yetu, kwa siku wanatumia zaidi ya megawati tano hadi 10 kwenye mgodi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale tumetengeneza *substation*. *Substation* tuliyoitengeneza ipo kwenye Kijiji cha Mpumbwi kama sikosei, Kijiji cha Mpumbwi ni kilomita sita tu kuelekea mgodini, umeme uingie ili hawa Geita *Gold* walipe fedha hizi. Megawati tano kwa siku ni fedha nyingi, lakini inaonekana kuna mchezo hapo unaendelea wa uchelewashi wa wale kuingiziwa umeme, na Shirika letu la *TANESCO* linazidi kukosa mapato kutoka kwenye mgodi wa Geita *Gold* kwa sababu hawataki kutumia, wameona mlango na dirisha kwenye mafuta, kwenye *exemption* hawataki kuja kuingia kwenye gridi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ninakuomba Kaka yangu January Makamba, tuna imani na wewe vijana, wana CCM tuna imani na wewe, Bunge lina imani na wewe, unaenda kuwa ni *game changer, issue* ni moja kwamba una *long strategic plan* ambazo wengi hawawezi kukuelewa, lakini ninakusihi kwenye haya maeneo ambayo nimeyazungumza, nenda katatue matatizo ya Watanzania. Suala la umeme kwenye Geita *Gold* lianze kufanya kazi. Hii *exemption* ya mafuta tupate fedha hii, hii ni fedha *Gold Mining* hapa kuna kitu wanakicheza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nishukuru na niunge mkono hoja na nikutakie kila la kheri, ninaamini hii ni moja kati ya bajeti *super* na Kaka yangu nakutakia kila la kheri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Festo Sanga. Tunaendelea na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika,

Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere na Mheshimiwa Tumaini Magessa ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu ambayo ni hotuba ya Waziri wa Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema naunga mkono hoja hii iliyopo mbele yetu. Ninapenda vilevile nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yake nzima, tunaanza kuona sekta inavyozidi kujipambanua, tunaanza kuona *transparency* kwenye hii sekta, uwazi, Waziri ametuonesha na ametuunganisha na wataalam wa kila aina katika maonesho ambayo tuliyaona hapa karibuni, kwa hiyo ninampongeza sana, ni jambo ambalo linaonekana ni dogo lakini ni kubwa sana, hiyo ndiyo inaitwa *leadership. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kwa kuanza, kuongelea jambo ambalo nimelisikia leo hapa kwamba tayari tumefikia mahali ambapo *LNG* tutakuwa kwenye hatua ya kwanza ya kusaini. Hii hatua ni kubwa sana na sijui kama Wabunge wanaweza kuelewa vizuri kwa nini nasema ni kubwa sana. Jambo hili ni zito, uchumi sasa tunajua kuliko tulivyojua huko nyuma. Kwamba uchumi wa gesi ni uchumi ambao tutautegemea sana tunakokwenda lakini uchumi wa gesi siyo uchumi tu, gesi ni silaha, gesi ni usalama wa Taifa na Mheshimiwa Mwijage ameweza kuielezea vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema na kusisitiza, tunaomba sana kwamba haya majadiliano ambayo yamefikia mahali ambapo sasa wanakwenda

kusaini wayakamilishe kwa haraka, hizo *signing* zifanyike na tuende kwenye hatua nyingine. Tumepoteza muda mwingi sana kwenye suala la gesi, tumepoteza muda mwingi sana, leo hii tusingekuwa hata na kilio cha haya mafuta ambayo tunayasema kwa sababu gesi hii tumekuwa nayo kwa miongo zaidi ya 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo nipende kusema kama alivyosema mdogo wangu Mheshimiwa Sanga, Njombe tunayo *potential* kubwa sana ya ku-*generate power,* peke yetu tunaweza tukafika megawati karibu 1,200 hata bila Nyerere *Dam*, Njombe tunao huo uwezo. Kwa sababu ukiangalia tuna megawati 600 pale Liganga na Mchuchuma, ukienda Ruhuji tunakaribu *megawatt* 360, ukija Lukamali hapa amepazungumzia kuna *megawatt* 200, ukienda Makambako tunazo megawati karibu 150 za upepo. Lakini tuna mito mingi midogo midogo na maporomoko ambayo yanaweza kuzalisha umeme kwa wingi. Kwa kiasi kikubwa tumekuwa mbali na tumetoa mchango mkubwa sana katika *energy sector. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuongelea tu uzalishaji kutoka katika maporomoko madogo madogo. Nchi nyingine pamoja na yote wakiwa na uwezo wa kujaliwa na Mwenyezi Mungu kupata maporomoko ambayo Njombe tunayo, leo hii tungekuwa tunaongelea uzalishaji mkubwa sana wa umeme kutoka katika maporomoko mbalimbali ya mito midogo midogo katika Mkoa wa Njombe, kwa bahati mbaya sisi katika Jimbo langu bado tuna matatizo makubwa ya umeme. Nimepata faraja leo kusikia kwamba na umekuwa muwazi Mheshimiwa Waziri kusema kwamba kilichokwamisha ni nini na Serikali inakwenda kufanya nini. Nipende kumpongeza sana sana Waziri, lakini nipende

kumpongeza Mheshimiwa Rais sana kwa haya makubwa mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hilo la *LNG* ni jambo kubwa anastahili kupongezwa na kwa kweli, kwa *LNG* nchi hii inaenda kuwa nchi ya uchumi wa gesi. Tunajua itachukua muda kwa vile tumechelewa, lakini tulipeleke kwa nguvu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maporomoko madogo madogo ambayo napenda kuyazungumzia. Pamoja na matatizo niliyonayo katika Jimbo langu ya kutokuwa na umeme kwenye vijiji zaidi ya takribani 20 mpaka leo hii na mitaa kadhaa kama 15, tumeweza kuzalisha umeme kutoka kwenye maporomoko haya madogo madogo. Ninapenda kusema tukienda kwenye kijiji kimoja kule kinaitwa Boimanda na Matola, pale tuna umeme ambao unazalishwa na Masista. Kuna mradi wa Masista ambao wameshaunza ni wa maporomoko. Mradi ule umekwama, na nipende kuishukuru Wizara kupitia *REA* wameweza kuwasaidia kwa kuwapa baadhi ya fedha. Mradi ule unahitaji 2.6 *billion dollars* wameweza ku-*invest* wao wenyewe kwa nguvu zao 1.6 *billion dollars.* Walikuwa na *gap* ya karibu *one million dollars* naongelea *million dollars* siyo *billion.* Serikali imewasaidia lakini Mheshimiwa Waziri nipende kusema, ukiangalia Masista wale ni Masista wa Benedict Getrude. Masista wale tayari wameshapeleka *transmission line* mpaka kwenye maeneo ya vijiji wakitegemea kwamba wangeweza kukamilisha *generation.* Kwa bahati mbaya hawakuweza kwa ukosefu wa fedha, Serikali imeamua kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* kwa makubaliano na *REA* walikubaliana waende kwenye maeneo yale, watumie *transmission line* ambazo zimeingia kwenye

maeneo ya vijijini ili waweze kuchukua umeme ambao unatoka kwenye gridi ambao unapita yale maeneo kwenda maeneo mengine ya Ludewa, wautelemshe kwa transfoma uingie kwenye maeneo ya vijiji vile vya Matola na Boimanda na waweze kuwasha umeme mapema. Tunavyoongea wako gizani lakini wana nyaya za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ninapenda kukuomba wakati umewaleta wataalam hapa niliweza kuongea nao kidogo lakini naomba utie mkazo ili *transformer* ile ambayo tayari imeshawekwa kwa gharama za *TANESCO* lakini haifanyi kazi iko *idle,* ifanye kazi ili wananchi wale waweze kupata umeme kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye jambo la pili la umeme wa maporomoko vilevile. Ninapenda hapa kuzungumzia mradi mdogo wa umeme unaitwa Mapembasi. Mradi huu ni wa siku nyingi, na ninapenda kusema toka mwanzo ni-*declare interest* kwamba ni mmoja katika waanzilishi wa mradi ule na mradi ule ni mradi ambao una Watanzania *professionals* katika Serikali, katika Mashirika ya Umma, vijijini wameungana, wamekusanya fedha zao, wengine wazee wamekusanya fedha ya *pension* kwa ajili ya kuendeleza mradi wa Mapembasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha ni kwamba mradi huu mpaka leo haujaweza kuendelea na kinachokwamisha ni urasimu ambao umejitokeza kwa muda mrefu ndani ya *TANESCO* na hasa kabla ya *TANESCO* haijapata uongozi mpya. Nina matumaini makubwa sana mradi huu utakwenda kufanyika sasa. Pia mradi huu unapata tatizo ambalo tunasema ni la kiufundi, kwa sababu ndani ya vifungu vya sheria

ambavyo Mheshimiwa Sanga hakuviongelea kwa undani, nipende kufafanua kidogo na hii ni miradi mingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ambayo ni ya mwaka 2000 ni *regulation* inasema kwamba, hakuna mtu ataruhusiwa kuingia kwenye miradi midogo midogo ya *SPPA* kama uzalishaji wake unazidi *demand* katika maeneo yale ambayo yeye anazalisha umeme. Kwa hiyo, Njombe tunazalisha, tuna-*consume megawatt* Tano lakini Mapembasi wanaweza kuzalisha megawati 10. Kwa utaratibu wa *regulation* hii *TANESCO* hawawezi kuwapa mkataba Mapembasi kwa sababu wao wanazalisha umeme zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nadhani hata *logic* inakuwa *defeated* hapa, kwa sababu hawa wanazalisha umeme siyo kwa ajili yao, hawazalishi umeme kwa ajili ya Njombe, wanazalisha umeme kwa ajili yaku-*feed* kwenye gridi, uende kwenye maeneo mengine na ikiwezekana uuzwe mpaka nje ya nchi. Kwa hiyo, ni wazi kwamba sheria hii inawezekana iliwekwa kwa maksudi Fulani lakini nadhani imepitwa na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewasikia hapa Wajumbe wa kamati ya Nishati wakisema ikiwezekana ni vema tutumie kila nafasi yakuweza ku-*generate* umeme katika nchi yetu kwa kutumia rasilimali tulizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna rasilimali zinachukua megawati 10. Tunawezaje kwa miaka karibu Saba bado tunasema kwamba majadiliano yanaendelea? Nimeona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameongelea hapa, na nimshukuru Waziri toka ameingia amelisukuma hili jambo lakini bado linakwamba

huko *TANESCO*. *TANESCO* wanataka umeme huu uuzwe siyo zaidi ya senti Saba *American Dollars.* Lakini sheria ya *EWURA* ya *SPPA* imeshaweka vigezo kwamba ukizalisha umeme kutoka katika maporomoko madogo madogo yasiyozidi megawati 10 unaweza ukauza umeme huo kwa senti 7.8. Lakini wao hawataki, sifahamu wana-*interest* gani na ndiyo maana watu wengine huwa wanakuja na mawazo kwamba labda kuna kitu ambacho wanakitaka. Kwa sababu sheria iko wazi, vitu viko wazi, lakini hatufanyi *progress* kwenye mradi huu mdogo wa Mapembasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Mheshimiwa Waziri uendelee na nguvu ile ile ambayo ulishaonesha kwamba utasukuma miradi midogo midogo na hasa ile ambayo iko ndani ya uwezo wa sheria. Hakuna mtu anavunja sheria hapa, sheria inaruhusu, ukiweza ku-*develop* na mradi huu siyo mradi mdogo ni mradi utakaotumia karibu *Dollar* Milioni 30 na watu wame-*invest.* Katika hao ma-*shareholder* tunao wazee wengi, Mzee Luhanjo alikuwa *Secretary* ni moja ya wanahisa kwenye mradi ule. Mzee Profesa Mbilinyi mpaka amekufa hajaona hata megawati moja ikizalishwa na ameweka hela zake pale, na kuna *professionals* wengi, Madaktari na Maprofesa kutoka Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni moja ya mradi ambao ni mfano wa mkusanyiko wa Watanzania waliojitolea ili kuweza kutengeneza *power* iingie kwenye gridi. Unawezaje kuanza kusita, unawezaje kuanza kuwa na wasiwasi na mradi ambao Watanzania wameamua ku-*invest* na wanataka kuuza umeme kwa bei ile ambayo inakubalika kwa minajiri ya sheria ya Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deodatus.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere. Mheshimiwa Tumaini Magessa, Mheshimiwa Joseph Kamonga ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia Wizara hii ya Nishati. Namshukuru Waziri na Naibu Waziri na viongozi wote, Katibu Mkuu wa Wizara na wote wanafanya kazi nzuri, wengi tumewapongeza wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa najiuliza mambo mengi, nikichangia hapa huwa mnaniona. Najiuliza kuhusu Waziri Makamba, wakati Mheshimiwa Makamba anawania Urais mwaka 2015 nilisoma sana hotuba yake. Moja ya hotuba yake aliyokuwa anaisema ni kwamba akiwa Rais atashughulikia mafisadi na wala rushwa katika nchi hii, akasema nchi yetu inaweza kwenda mbele au ikarudi nyuma kutokana na matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikuombe kwa hilo ambalo ulilokuwa unalisema kipindi hicho, kwenye Wizara yako tunataka kukuona kwa miaka hii ambayo mama amekupa, tuone unatekeleza yale ambayo ulitaka kuwa Rais, leo nilikuwa nataka nikupe ushauri. *(Makofi)*

Lingine ambalo nikuseme Mheshimiwa Makamba ni kwamba ni moja ya vijana bora wa Afrika waliosoma chuo kikubwa duniani *Harvard University* ni vijana bora waliosoma na Watanzania na wale ambao walipelekwa

na CCM. Umekaa Harvard miaka mingi, nategemea sasa ukija hapa uta-*apply* mambo makubwa ingawa Watanzania hawayaoni, lakini wanayaona hiki ulichotutengenezea hapa leo ni jambo kubwa sana na mabanda uliyoleta juzi hapa ni jambo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndugu yangu Makamba umesoma Harvard, Harvard ambayo ina vitabu ma-*cover* yake yamefunikwa na ngozi ya binadamu unaogopa nini? Harvard ambayo ina watu ambao wanafanya sayansi jumla ya miili iliyoko pale ni 23,000 unaogopa nini Harvard ambayo maraisi saba wa Amerika wamesoma pale, unaogopa nini kutekeleza mambo haya? Nina imani na wewe kwamba sasa tumepata mtu wa kutupeleka kwenye mwanga ni wewe, ukishindwa ni uzembe wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nishauri tu sasa wasomi hawa wakisoma sana wanataka kila kitu wafanye sayansi ndio shida sasa, kwa mfano hivi karibuni wakati unatoa hotuba yako umetuambia mambo mazuri sana, lakini moja umesema utaunda tume ya kwenda kuchunguza maeneo ya mjini yanayofanana na vijijini uyape umeme. Uunde tume miezi sita, hayo ndio matatizo ya wasomi. Kumbe sisi Wabunge tunaweza kuwa tume, ukasema baada ya hapa kila Mbunge alete maeneo ambayo yanafanana na vijijini yanayohitaji umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wenyewe ni tume hapa, hizo hela za tume tupe sisi tuweke mafuta mzee, halafu baadaye wewe tuma watu wako wilayani na mkoani wakachunguze haya maeneo. Nakujua msomi kazi yake ni kuhakikisha kwamba hawezi kufanya jambo lazima

alifanye kwa utafiti, sasa u-*apply geopolitics* ya Marekani na Tanzania ni vitu viwili tofauti, sisi hapa hatuna hela, wenye hela ambazo ungezitumia kuunda tume ungetupa sisi tuunde pale kwenye Jimbo langu nina vitongoji zaidi ya 37 havina umeme, hizo hela zingekuja upande wa pili.

Kwa hiyo, mimi nakushauri uangalie upya kwamba tume ya nini, sisi wenyewe Wabunge ni tume, leta makaratasi hapo leta fomu hapo tujaze halafu fuatilia uone kama ni ukweli ama sio ukweli, kwa hiyo jambo litakuwa liko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri nimeangalia hivi vipaumbele vyako kweli nimesikitika sana yaani kabla sijafanya utafiti nimesikitika mno, hivi najiuliza vipaumbele viko 12 Bwawa la Nyerere liko wapi ambalo lina shilini trilioni 6.55 liko wapi kwenye vipaumbele hivi ambavyo umevitoa? Lakini nikajua kwamba pengine umejumlisha kwenye kipaumbele Na. 1 haiwezekana, kwa sababu *political is all about perception* unaweza ukasema mtu akaangalia akasema Bwala la Nyerere limeachwa haliko kwenye vipaumbele tutasemaje sisi watu wa CCM tutasemaje, lakini kumbe umeliweka humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipofunua ukurasa wa pili nikakuta unasema miradi ya kusafirisha umeme, ukasema miradi ya uzalishaji wa umeme iliyopo katika hatua za utekelezaji; Bwawa la Nyerere ambalo umelitaja hapa shilingi trilioni 6.55 umelitengea shilingi trilioni 1.44 maana yake hili bwawa fedha yake imechukuliwa ni karibu ya nusu ya bajeti yako yote ambayo ina shilingi trilioni 2.9. Kwa hiyo hapa umelifanya vizuri, lakini nikuombe kipaumbele cha kwanza ni Bwawa la Nyerere, hili bwawa likiwepo maana yake matatizo ya umeme yanaisha,

nikuomba hii karatasi ibadilishwe iwekwe upya Bwawa la Nyerere liwekwe la kwanza, lifanane na hiyo tunayokuwa tunazungumza hapa, lakini kwenye bwawa hili mimi najiuliza mambo mengi sana, nimesikia kuna changamoto ya Bwawa la Nyerere, najiuliza ni changamoto gani hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kama kuna changamoto tuletee, sisi tunaamini wataalam na wanasheria nguli wa Tanzania waliokwenda kufanya mikataba ya ujenzi wa Bwawa la Nyerere wamejiridhisha na kila kitu. Kwa hiyo mkandarasi anapaswa kufuata ile mikataba waliyoweka, sasa kama kuna changamoto zinatoka wapi?

Mimi nikuombe kama inawezekana waite wote waliofanya mikataba, wanasheria wote nguli, kaa nao na mkandarasi pengine mkandarasi ameona sasa wewe umeenda anakupa mambo mapya, mikataba iliyoko pale walioifanya wamefanya kwa uhakika zaidi, ifuate na mkandarasi afuate mikataba atekeleze mradi. Akikuzingua na wewe mzingue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa nirudi kwenye jimbo langu, mimi nakushukuru sana tena sana na Watanzania na Wabunge niwaambie huyu Makamba ni moja ya vijana ambao tunatakiwa kumtumia sana, tatizo tu kwamba ana-*apply geopolitics* ya Marekani, sasa arudi kwenye polepole ya Tanzania, asiwe na magharama makubwa ya kutekeleza miradi lakini ana uwezo wa kutengeneza vitu vyovyote vile, ana uwezo wa kufanya jambo hilo, nikushukuru kwa sababu ya mabanda yako uliyoleta hapa tumetembelea mabanda yote, nimekutana na *TANESCO* mkoa nilikuwa na

Wajumbe wa Serikali za Vijiji nilikuwa na Wenyeviti wa Vijiji karibu 30 wamejiridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo maeneo yote ya Kurusanga, Kata ya Salama Kurusanga na maeneo yote ya Mgeta, Gogea, Bukoba na maeneo yote ya Machimolo pale Janungu na maeneo yote ya Nyamswa yote kwenye vijiji vyote ambayo tumeleta utaenda kuyatekeleza na bahati nzuri wamenipa uhakika huo. Kwa hiyo wananchi wa Jimbo la Bunda, wananchi wa Tarafa ya Chamliho wajiandae kupokea umeme wa Makamba ambao sasa utatuweka kwenye mambo mazuri katika mwanga utakaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho ambalo naliona hapa ni suala la kuweka umeme vijijini, hivi tuna kitu kinaitwa *REA,* kuna ka mradi kanaitwa *densification,* kamradi kale kalikuwa kanafadhiliwa na watu wa nje hivi kamekufa au kapo? Maana yake siku hizi sikaoni sana kanaendelea labda ukija hapa utanipa majibu kale kamradi ka-*densification* kamefia wapi? Kalikuwa kanaenda kama kamradi kanatelekeza umeme kwa msaada wa hela za nje, sasa tujue kamradi kanaenda wapi, kanakuja au kanaenda sehemu nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine ambacho nakiona hivi tunapeleka umeme vijijini, unaenda unaweka transfoma ya volti 50 halafu inabeba watu 20, sasa watu wanafika mpaka 50, mpaka 70 transfoma ni hiyo hiyo haibadilishwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, transfoma ya kilovolti 100 inabeba watu mpaka 300 haibadilishwi, sasa kwa nini umeme usikatike? Lazima ukatike tu, haiwezekani kuweka

transfoma ya kubeba watu 20 halafu watu wakatumia 60, wakatumia 100 haiwezekani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama ni tume ya kuunda ni hiyo sasa kaunde tume ya kutazama maeneo gani ya transfoma zina matatizo ambazo zinafanya umeme unakatikakatika. Sasa umeme unapokatika unatuletea shida sana na mimi Mheshimiwa Makamba nikuambie sasa watu wa *REA* na watu *TANESCO* uwaambie siku Yanga na Simba zinacheza umeme usikatike na siku tukienda kule Arusha umeme usikatike, siku tunaenda kucheza na Coastal umeme usikatike, sasa hilo liwe agizo kwamba sasa siku tunafanya mambo yetu umeme usikatike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namkushukuru sana Mheshimiwa Waziri Makamba kwa kweli uwezo unao, sasa ukishindwa kutekeleza hii Wizara wakati mama amekupa amekuamini na sisi tumejilizisha na kisomo chako....

**MHE. JACKSON G. KISWAGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mnenaji hapa anazungumza kwamba January Makamba ana uwezo mkubwa, lakini ningependa nimuongezee taarifa kwamba hata Mkurugenzi wa *TANESCO* Maharage Chande ni mmoja ya vichwa vigumu tulivyokuwa navyo hapa Tanzania, kijana mbunifu, lakini pia yupo Mwenyekiti wa Omary Issa mwanzilishi wa *Celtel Tanzania* namfahamu vizuri, ni

mmoja ya vichwa vigumu sana tulivyonavyo hapa nchini ahsante sana, nataka nimuongezee tu kwamba hilo *TANESCO* ipo salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere unapokea hiyo taarifa?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea lakini nilitaka kujua labda analeta Simba ambaye imemfukuza kocha kumbe ameleta mambo mazuri, naipokea. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwneyekiti, nashukuru kwa yote hayo na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, tunaendelea na Mheshimiwa Tumaini Magessa, Mheshimiwa Joseph Kamonga na Mheshimiwa Mohamed Said Issa wajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii, lakini namshukuru sana Mwenyezi Mungu vilevile kutupa nafasi ya kuweza kujadili hotuba hii ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii nilikuwa napitia randama, nikaona wazi kwamba katika malengo makubwa ya Wizara ya Nishati moja ni kuongeza uzalishaji, kuboresha mfumo wa usafirishaji na usambazaji wa umeme. Sasa nikawa najaribu kuangalia Waziri anapozungumza ni mahali gani anagusa kuongeza uzalishaji na ni wapi ripoti hii inaongeza kama anaongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu nifanye marekebisho kwamba katika kuongeza uzalishaji inawezekana hii *leaflet* haikuonesha Bwawa la Nyerere, lakini kwenye vipaumbele vya Wizara hii kwenye randama kipengele "A" kinaonesha Bwawa la Julius Nyerere kwa hiyo inawezekana katika usomaji kuna mahali watu wamesoma tu haraka haraka lakini imeonyeshwa ndio namba moja kwenye vile vipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yako nzima ambayo wachangiaji wameonesha namna ulivyo na wataalam wazuri, lakini Mheshimiwa Waziri niseme tu wazi mimi ningeulizwa leo mahali gani kuna shida kule kwa wananchi wetu pamoja na uzalishaji huu unaosemwa, ningezungumza shida tunayoipata kubwa ni kutokana na wananchi wetu kuwa na ahadi ya vijiji kadhaa kumaliziwa kupewa umeme na havijapewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa na jirani yako anakula, halafu wewe unalala njaa pembeni, unaweza ukajua malalamiko uliyonayo ndani ya moyo na hata ndani ya kusema, kwa hiyo kuna watu wengi ambao tunao kule kwenye vijiji vyetu wanalalamika kwa sababu umeme haujafika kwao. Lakini nikupongeze kwa sababu kama nilivyosema malengo haya ambayo nimesema umeonesha wazi kwamba kuna uzalishaji unakwenda kufanyika sasa shida ambayo naiona katika vile vipaumbele kuna vipaumbele kutoka "A" mpaka "U"; sasa "A" mpaka "U" vinanionesha kama ni vingi sana na hii pesa ambayo niseme tu kwenye randama inasomeka bado ni shilingi trilioni 2.7 lakini hapa imesemwa shilingi trilioni 2.9 maana yake kuna mahali fulani hapajarekebishwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nisema pesa hii nina mashaka sana kwenye utekelezaji kama inaweza kufanya haya mambo ambayo yameandikwa huku, kwa hiyo inawezekana mipango ikawa mizuri sana, lakini mwisho wa siku tutakapoanza kuteleza tukaingia kwenye mahali fulani ambako tunashindwa kuitekeleza. Kwa hiyo, niombe sana nikiona hapa kama nilivyosema "A" mpaka "U" inaonesha tuna sehemu tunakwenda kuongeza umeme uzalishaji JK Nyerere megawati 2115.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna Ruhuji megawati 358; Lumakari megawati 222; Kinyerezi megawati 185; Lusumo megawati 80; Malagalasi megawati 47.5; ukiangalia Somanga kuna megawati 330 na sehemu zingine nyingi ambazo zinaonekana kwamba lengo letu inaonekana ni kubwa na mpango wetu mkubwa kwenye hotuba hii ni kufikia megawati 5,000 ifikapo mwaka 2025/2026. Sasa nikawa na mashaka hapo kwamba je, hii *allocation* ya fedha ambayo tunaisema hapa, itatupeleka kutengeneza na tufikishe megawati 5000 kama tulivyoandika hapa maana tusife mahali tukawa na mipango mizuri kubwa *resources* zetu hazitoshi.

Kwa hiyo, niombe sana kwenye hoja hii tuhakikishe *resource* tunazozizungumzia tuna mahali tunaweza kwenda kuzipata ili tuzipate megawati 5000 kwa sababu wananchi wanahitaji umeme sasa, mwanzo umeme ulikuwa ni hanasa lakini sasa hivi kila mmoja ana uhitaji kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna usafirishaji nimeona hapa kuna Rufiji Chalinze - Dodoma Kv 400; kuna Chalinze - Kinyerezi Kv 400; Singida – Arusha - Namanga Kv 220; kuna Rusumo - Nyakanazi Kv 220; kuna Geita -

Nyakanazi Kv 220. Sasa nisimame hapa kwenye Geita - Nyakanazi hapa, ndipo Jimbo la Busanda vijiji kadhaa vinategemea vipate umeme kwenye mradi huu wa Geita - Nyakanazi. Hapa vimeandikwa kwamba kuna *allocation* ya shilingi bilioni 6.53; mradi huu umekuwepo muda mrefu, unajengwa na hauishi, kwa hiyo mahali fulani kwenye vijiji ambayo tunategemea vipate umeme kutoka kwenye mradi huu imeendelea kuwa ni mazungumzo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzo nilisema ni nguzo za umeme, lakini baadaye imezungumzwa kwamba sasa kama hapa inatakiwa kwenda kumaliziwa, sina uhakika kama mradi huu utamaliziwa kwa wakati ili wananchi waweze kupata umeme kutoka mradi huu wa Geita – Nyakanazi; kuna Bulyanhulu - Geita Kv 220; kuna *North-West Grid Extension* ambayo inaenda Mbeya, Sumbawanga, Mpanda, Kigoma na Nyakanazi iko mingi ambayo imeandikwa hapa, lakini *more interesting* ni mradi ule ambao mnakwenda kuhakikisha kwamba sasa mnaenda ku-*rectify SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme kwenda kwenye *SGR* ambayo sasa hivi ipo kwenye *construction,* tunategemea kabisa hapa pawe muhimu sana kwa sababu bila umeme maana yake hatutaweza ku-*oparate*. Sasa inaonekana katika miradi hii ambayo imeandikwa hapa, hiyo *SGR rectification* ni sehemu yake. Kwa hiyo, niwaombe sana tuhakikishe kwamba tunakwenda kufanya hivi vitu ili wananchi wetu waweze kuona maendeleo ambayo tumekwisha waambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna kipengele “C” ambacho ni cha kuendeleza miradi ya nishati vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini, hapa kuna changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni Busanda mwaka jana kwenye hotuba hii kwenye bajeti hii tulionesha kuna vijiji 57 havina umeme, *REA* wakaonekana tumepata mkandarasi, mkandarasi yule akaonekana baadaye alikuwa anaonekana *performance bond* hana, tumepata mwingine, lakini mpaka leo ninavyozungumza mwaka jana vilikuwa 57 na mwaka huu ni 57. Sasa kama tunapima *KPI* tunataka kuona utekelezaji umefanyikaje mwaka jana vilikuwa 57 na mwaka huu bado viko 57, niwaombe sana unaweza ukajua ilivyo vigumu kusimama kwenye mkutano wa wananchi ukawaeleza mwaka jana vijiji 57 vilikuwa havina umeme, halafu wanakuambia vingapi umeshaweka umeme mwaka huu unasema bado viko 57, kwa hiyo wewe una nafanya *zero performance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikuombe sitaki kusema Waziri una *zero performance* kwenye hili, lakini Mbunge ndiye ana *zero performance* kwa sababu wananchi wanajua hajafanya kitu chochote. Sasa niwaombe sana kwenye *REA* hapa kwamba kama tumewaambiwa wananchi kuna vijiji 3,617 basi kazi ianze kuonekana, tuanze kuonekana kama vijiji vinapungua ili kufika mwaka 2025 kuwe na mahali fulani wananchi ambao walikuwa hawana umeme wameshapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi juzi nimepewa *t-shirt* kwenye semina ya hapa *t-shirt* imeandikwa nyuma sasa tunaingia vitongoji vyote, huku nyuma ya *t-shirt* yangu nimeogopa kuivaa kwa sababu wananchi wanaweza wakanipiga mawe, kwamba mimi jimbo langu lina vijiji 84, halafu nina vijiji 26 tu vyenye umeme na vijiji 58 havina umeme, halafu nitembee na tisheti nyuma imeandikikwa kwa sababu tunaingia kwenye vitongoji

wataniuliza, *are you mad*? Umekuwaje tena? Yaani mmeingia kwenye vitongoji wakati vijiji havina umeme, mbona mmeruka? *(KIcheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana nataka hii *t-shirt* niivae, lakini naomba sasa nihakikishiwe kwamba nikiivaa tunapata kweli umeme kwenye vijiji na baadaye twende kwenye vitongoji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu "D" kwenye randama kuanzisha maandalizi ya kupeleka umeme katika vitongoji vyote ambayo iko ukurasa wa saba kwenye randama yetu, niwapongeze sana kwa hili kama kuna mahali wananchi wanapata shida ni ile kilometa moja tulio-*supply* umeme yaani mtu umemuonjesha biriani, lakini biriani yenyewe ilikuwa ni punje 10 sasa anatamani aanze kula biriani imekwisha, hebu tuwapelekee nimefurahi sana kusikia sasa unatuongezea kilometa mbili, sijui zinaanza lini hizi, ili walau hizi kilometa mbili hizo zionyeshe kwamba kuna mahali sasa wananchi wameongezewa hii *peripheral* ya kilometa moja ilikuwa inatuletea ukipiga zile nguzo *span* ya mita 50 ni nguzo 20; lakini ukipiga *span* ya mita 100 maana yake ni habari ya nguzo kumi na ngapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana ili wananchi wetu waweze kuona maandalizi haya tunayafanya kwenye vitongoji na nyongeza tulioifanya, lakini wako wananchi wengi wameamasika kuweka umeme kwenye nyumba zao na bahati mbaya hapa katikati tumeambiwa mita hakuna, kwa hiyo wananchi wengi wamekwisha fanya *wiring,* wamekwisha fanyiwa *survey,* lakini umeme hauendi kwao kwa sababu mita hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa niliyokuwa nayo mchana wa leo ni kwamba mita kadhaa zimeenda, lakini kuanzia wale waliofanya *wiring* na kuwa *surveyed* kuanzia mwezi wa pili kuja mwezi wa tano hapa bado mita zile hazitoshi. Niombe sana wananchi wale wapate umeme, maeneo mengi sitaki kuyataja hapa wako wananchi kila anayekupigia simu anaonesha amemaliza hii kazi *wiring,* amekuwa *surveyed* lakini hawezi kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niwaombe sana wataalam Mheshimiwa Waziri kwa sababu *scope* ya kazi wanaijua, kama *scope* ya kazi wanaijua maana yake wanajua ni mita ngapi zinahitajika, ni nguzo ngapi za *LV* zinahitajika, ni *wire* kiasi gani za *copper* au *aluminum* zinahitajika, *insulator* kiasi gani zinahitajika kuunganisha huu umeme. *(Makofi)*

Sasa ni mahali gani ambako tunafika mahali tanafanya mradi utekelezeke, lakini tunavyoenda kutekeleza mita 800 hamna, mita 10000 hakuna, hii inakujaje? Kwa hiyo niombe sana tunapokwenda kwenye mradi ambao tayari tutakaa mezani kuandika kwenye makaratasi, *scope* ya kazi inajulikana, tutatengeneza *chart activities* zetu tufike mahali kwamba tuna vijua vile vitu tuviagize vije ili wananchi wetu wasifike mahali ameshalipa amefanya *wiring* lakini anaonekana umeme anasubiri mita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kuna watu toka mwaka jana mwezi wa 10 walikuwa hawajafungiwa umeme, leo ni mwezi wa tano miezi saba na ameshalipa pesa yake hii pesa angelipia mwanafunzi ada, sasa kwa nini aliingiza huku lazima naye ana vipaumbele vya alifikiri angepata umeme azalishe, halafu alipie mwanafunzi

ada, sasa imekaa miezi saba, mtoto hajaenda shule, kwa hiyo, niwaombe sana kwa sababu *scope* tunayo tuwe tunafanya makadirio ambayo yanaweza yakafanya wananchi wetu waweze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Jimboni Busanda kila siku nimekuwa ninasema sisi ni wachimbaji wa dhahabu, sisi ni wakulima, nilitegemea sana umeme uje kule ili hizo *maximum demand* hizo *KVA* tuweze kuwalipa, sasa nashangaa inaonekana umeme unaenda mahali kwenda tu kwenye matumizi ambayo ni *domestic* wakati matumizi ya viwanda yalitakiwa yazalishiwe kule Busanda umeme haufiki. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri inawezekana jicho lako lilikuwa halijachungulia Busanda kwa ukubwa wake nikuombe sana ulete tuchimbe dhahabu kwa kutumia umeme huu ambao tunausema leo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tumaini Magessa. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Kamonga, Mheshimiwa Mohamed Saidi Issa na Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo, ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie bajeti hii na niungane na Waheshimiwa Wabunge wote walioendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri pamoja na Mheshimiwa Waziri January

Makamba na Naibu wake Mheshimiwa Stephen Byabato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba nimekutana na Mheshimiwa Waziri na changamoto zangu ameweza kunisikiliza vizuri, lakini bahati mbaya wakati nazungumza na Mheshimiwa Waziri, wananchi wa Ludewa walionituma hawakuwepo, kwa hiyo, hawakusikia. Kwa hiyo, naomba nirudie niliyoyaongea kwa Mheshimiwa Waziri. Nikiri pia kwamba nimezungumza na Mkurugenzi wa *REA* changamoto zangu ameweza kuzisikiliza vizuri na nipongeze sana Wizara hii kwa kuandaa wataalam wote kuja hapa viwanja vya Bunge kuweza kutusikiliza. Kwa hiyo changamoto zetu tumeziwasilisha tunaamini zitafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa maana ya wananchi walionituma wasikie nikiwasemea, naomba nianze kwa kumuomba sana Mheshimiwa January Makamba kule Jimboni kwangu Ludewa hasa Tarafa ya Masasi, Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kusambaza umeme isipokuwa ni ngazi ile ya vijiji kwenye vitongoji mbalimbali bado kuna malalamiko sana na nilifanya ziara kwenye vijiji vyangu vyote 77 vikiwemo hivi vya Tarafa ya Masasi.  Nilikwenda Kitongoji cha Chingole pale Manda kuna wananchi walikuwa hawajaunganishiwa umeme. Kwa hiyo, naomba sana na vitongoji vingine vya Manda viweze kuunganishiwa umeme pamoja na Tarafa yote ya Masasi.  Huu mradi wa vitongoji naomba Ludewa nao iweze kupewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna mradi wa *REA* ambao uko kwenye tarafa ya Mwambao, kuna mkandarasi mmoja alipewa kazi kwenye Kijiji cha Mkwimbili, Kata ya Makonde, Kata ya Lifuma, mkandarasi

huyo anashindwa kuwasha umeme tokea mwezi Aprili kwa sababu niliomba Serikalini wapewe umeme mkubwa wa *KV* 33, lakini sasa umeme uliotoka Makao Makuu ya Wilaya ya Ludewa kwenda Lupingu ni *KV* 11. Kwa hiyo sasa waliomba na nashukuru niliongea na *engineer* wa *TANESCO* Ludewa amekiri kwamba Mheshimiwa Waziri ameshatoa maelekezo, kwa hiyo naomba amsisitize ili aweze kubadilisha hiyo KV 11 Kuwa 33 ili wananchi wa Mkwimbili, wananchi wa Makonde na wananchi wa Lifuma waweze kuwashiwa umeme mapema iwezekanavyo, kwa sababu zile nguzo tokea ziwekwe wamekuwa wakipiga nazo picha mwaka sasa umeisha, wanatamani sana umeme uweze kuwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa Tarafa ya Mwambao, kuna vitongoji ambavyo vina idadi kubwa ya watu, kuna Kitongoji cha Ndamba na Kitongoji cha Kilindi, Kitongoji cha Ndamba kipo pale Kata ya Makonde na Kitongoji cha Kilindi kipo Lifuma, ni vitongoji ambavyo vina idadi kubwa ya wananchi ambao wapo *willing* na wameupokea mradi vizuri, lakini hawa wameachwa, naomba nao wafikiriwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Tarafa hii ya Mwambao kuna mkandarasi mwingine ambaye amepewa Mradi wa Kusambaza Umeme Kata ya Lumbila, Kijiji cha Ndoa, Kitongoji cha Kimata, Kitongoji cha Kitewele na Liunji, Mkandarasi huyu bado hajapeleka nguzo kwa muda mrefu sana tokea asaini mkataba. Nilivyozungumza naye alikuwa amezungumza kwamba ameshawasiliana na watu wa meli ya mizigo pale Itungu kwa sababu ipo vizuri inafanya kazi, watapeleka. Naomba ahimizwe ili aweze kufanyakazi ili kule mwambao kwote waweze kupata umeme kama maeneo mengine ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kijiji cha Kitewele ambacho kipo Kata ya Mawengi, eneo hili lipo jirani na mzalishaji binafsi umeme wa JUHUMA. Kwa hiyo nilishauri ili waweze kufikisha umeme huu ni vizuri wakaingiza kile Kijiji cha Mawengi kwenye Mradi wa *REA* ili waweze kupata uelekeo mzuri wa kupeleka umeme katika Kitongoji cha Liunji na Kitongoji cha Kitewele. Kwa hiyo kwa Tarafa ya Mwambao tutakuwa tumemaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika niliweza kuzungumza na Mheshimiwa Waziri na Mkurugenzi wa *REA* kwamba wananchi kwenye vijiji 20 vya Jimbo langu la Ludewa ambao wanategemea umeme wa mzalishaji binafsi Kampuni ya Madope, kwa kweli tunaomba sana Serikali isaidie Kampuni hii ya Madope, kwa sababu jukumu la msingi la Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na namwona Mwanasheria Mkuu wa Serikali pale, najua atatusomea kama si Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, kama ilivyofanyiwa marekebisho yake mara kadhaa, inasema jukumu kubwa la Serikali ni ustawi wa wananchi. Kwa hiyo umeme ni ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa jukumu hili ni la Serikali, naomba sana Serikali iweze kumsaidia huyu mzalishaji binafsi Kampuni ya Madope kwa sababu vijiji 20 ni vingi sana kupata mgao wa umeme wa masaa zaidi ya 12. Naamini kabisa wakipewa nyaya kwa sababu ule mradi wa mwanzo zile nyaya zilizowekwa zilikuwa ni *aluminum millimeter* 50. Wamejitahidi wao kwa nafasi wameweza kuhakikisha Mkiu ile Kata ya Lubonde wanapata umeme masaa yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili waweze kutatua tatizo hilo Kata ya Madilu na Kata ya Mlangali, wanahitaji kupata nyaya ili waweze kubadilisha ile miundombinu, waweze kufikia na Kata ya Madope na Lupanga. Kwa hiyo naomba sana Wizara hii, nikiri kwamba baada ya kuwasiliana na Mkurugenzi wa *REA*, Bodi ya *REA* imefika pale wameona hizi changamoto, hilo lazima niwe muungwana, Mkurugenzi mwenyewe amekwenda ameona changamoto na yeye atakubaliana na mimi kwamba kuna haja *REA* na mimi Mbunge na wale wazalishaji wa Kampuni ya Madope tuna kila sababu ya kupita kwa pamoja na watalaam wa *REA* kwenda kuzungumza na wananchi, kuwapa uhakika kwamba wale ambao wateja wapya hawajaunganishiwa umeme kule Lupanga wawe na uhakika kwamba hadi lini matatizo haya yatakuwa yametatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niendelee kuishukuru Serikali, tulikaa kikao na Mkurugenzi wa *REA* kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri waliweza kutoa Shilingi Milioni 307, Milioni 150 zilitolewa lakini hizo zilizobakia wamewadhamini Kampuni ya Madope kuweza kuchukua nyaya kwa mzalishaji. Naomba Mkurugenzi wa *REA* atusaidie kuongea na yule mzalishaji ili nyaya hizi ziweze kutolewa haraka ziwawezesha Kampuni ya Madope kuunganisha umeme kwenye gridi ya Taifa, ule mkataba ambao wanauzia Serikali, itawasaidia kupata mapato yatakoyoweza kutatua changamoto ndogondogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukitatua tatizo la mgao wa umeme kwenye hivi vijiji 20 na tukaenda kusaidia yule mzalishaji binafsi wa JUHUMA ambaye anazalisha umeme pale Mawengi, unakwenda Milo itasaidia sana kuweza kumaliza kero za umeme kwenye Jimbo la Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya ninayoyasema ni maeneo ya uzalishaji mkubwa sana. Pale Mlangali idadi ya watu ni kubwa, pamekaa kibiashara, kwa hiyo, kukosa umeme pale kwakweli ni kuwaadhibu sana wale wananchi. Nimepita juzi wakanisimamisha, nilikuwa natoka kwenye ziara jimboni, kilio chao kikubwa wananchi wa Mlangali, Madilu, Madope, Lupanga na pale Lugarawa ni umeme na katika maeneo haya kuna vituo vya afya, kuna taasisi, kuna chuo cha afya, kuna chuo cha *VETA* pale Shaurimoyo kinajengwa na Serikali imetoa bilioni tano na milioni mia nne, kipo kwenye Kata hii ya Lugarawa. Kwa hiyo, kuna taasisi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili niendelee kuomba sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Nape ametuwekea *booster* pale Milo ya *TBC* lakini pale hakuna umeme. Nimshukuru Meneja wa *TANESCO,* Mkoa wa Njombe ameshawasilisha kwenye bajeti hii na ndiyo maana naunga mkono hoja kwa sababu kuna fedha nimeona zinakuja jimboni kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja, naomba tu changamoto zote za Jimbo la Ludewa ziweze kutatuliwa na kukatika kwa umeme kuweze kuisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kamonga. Tunaendelea na Mheshimiwa Mohamed Saidi Issa, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo ajiandae.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika Wizara hii ya Nishati. Awali ya yote, niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati Mheshimiwa January Makamba pamoja na Naibu wake, lakini pamoja pia na watendaji wake katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli dira ambayo wameionesha ya kutuhakikishia Watanzania kupata umeme wa uhakika ni nzuri sana, mipango yao kwa kweli mimi binafsi naipongeza. Pia hii imeonesha, pale ambapo katika michango yetu ya leo Wabunge, baada ya kupata semina ambazo zimetupa uelewa mkubwa, nimeona pia Wabunge wengi sana wameelewa mipango ya Wizara. Kwa hiyo, hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitaanza kwa sehemu ya Umeme wa Joto Ardhi yaani *geotherm*. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake hapa ameonesha kwamba tutapata umeme wa *megawatt* 195 ya Umeme wa joto ardhi, lakini mimi kama Mjumbe wa Kamati tulivyofuatilia tumeona kwamba bado Sheria ya JotoArdhi haijawa sawasawa, haijatekelezwa. Sasa najiuliza maswali, ni wapi hasa Waziri anaweza kuja kutekeleza kuzalisha umeme wa jotoardhi wakati bado haijatambulika kwamba bado ni sehemu ya madini ama ni sehemu ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Waziri anapokuja ku-*windup* atueleze tayari amefikia wapi kwanza sheria haijaletwa, lakini la pili hakuna miundombinu na la tatu pia bado fidia kwa wanaomiliki maeneo haya yenye jotoardhi haijafanyika. Kwa hiyo,

tunakujaje kuzalisha umeme huu wakati haya mambo ya msingi bado. Tunaomba anapokuja ku-*windup* atufahamishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *REA,* tunawapongeza sana mpango wao ni mzuri kwa kuhakikisha kila kijiji, kila kitongoji kinapata umeme unaostahiki, lakini kuna tatizo kidogo ambalo limejitokeza. Tulivyofanya ziara Kamati tuliona kwamba *REA* imepeleka umeme kijijini lakini nyumba zilizounganishwa ni mbili. Ina maana hapa hakuna maandalizi mazuri, watu hawakuandaliwa na pale tayari kuna mkandarasi tayari ameshalipwa, waliopata umeme ni watu wawili ama watatu, lakini zipo nyumba za jirani hazipata kwa sababu hawakuandaliwa. Nashauri kabla ya kufika pale wananchi waandaliwe, wafanye *fitting* ili wote wa-*enjoy* ule umeme wa *REA* unaokwenda pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine pia ni hili suala la ujazilizi; naona *REA* kwanza tulianza mita moja, halafu tukaenda mita mbili, halafu tunaenda ujazili, yaani tunakwenda mwisho tutafika hata majina mengine hatuyafahamu. Kwa hiyo, nashauri kwamba sisi lengo letu si mita moja, si ujazili lengo letu ni kuwapa umeme wa uhakika wananchi. Kwa maana hiyo tuhakikishe ile sehemu ambayo tuna *deal* nayo, basi wapate umeme wote sio tunarudia, hili jambo linatutia hasara kama Taifa, kesho tunarudia, kesho mkandarasi huyu, kesho mkandarasi huyu, linatutia hasara. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri alichukue hili pamoja na timu yake waliangalie ili kuondoa hasara kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niende kwenye suala la bei za umeme; hili suala la bei za umeme, nazungumzia umeme wa mijini, sizungumzii umeme wa

vijijini ambao huo tumeshaujua ni Sh.27,000. Mheshimiwa Waziri watu wa mijini ambao tayari wana umeme, wale wenye uwezo tayari wameshaweka umeme kwa maana hiyo watu ambao hawajaweka umeme, hawana uwezo kwa nini sasa tumekwenda kuweka bei ya shilingi 320,000; shilingi 500,000 au shilingi 600,000 bila kuangalia hawa maskini ya Mungu, watu wanaishi mjini wanasaidiwa na watu wa vijijini. Kwa maana hiyo lazima hizi bei za umeme kwa sehemu za mijini bado tuziangalie, hii shilingi 320,000 ni kubwa mno, maskini ni wengi pale, tuna umaskini mkubwa katika nchi hii hata kama watu wanaishi mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba bei hii ya shilingi 320,000 ni kubwa sana, hata kama hawatalipa shilingi 27,000 lakini iangaliwe ilipwe ya nafuu ameshauri hapa Mbunge wa Manonga kwamba wao walikuwa wanalipa shilingi 170,000, hiyo kidogo ni *affordable,* lakini huwezi ukalipa 320,000 hata kazi huna na wewe unataka umeme, unataka kuuza *ice-cream,* unataka kuuza biashara ndogondogo, lakini hamna. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba aliangalie hili ili tupate bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pale ambapo mwananchi ameshalipa kuunganishia umeme, kunakuwa na muda mrefu anafuatilia muda mrefu, tunaomba Waziri aje na *commitment* hapa baada ya kulipa atachukua muda gani kuunganishiwa umeme kwa sababu watu wanachukua mpaka miezi miwili, mitatu, tayari wameshalipa lakini hawapati umeme. Kwa hiyo, Waziri atuambie muda halisi hasa baada ya kulipa ni shilingi ngapi na baada ya hapo nini kitafuata kama mwananchi hakupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa sikuona sehemu ambayo kutakuwa na ukarabati wa mabwawa kama vile Hale, Kidatu, Nyumba ya Mungu, Rusumo ambayo haya ni mabwawa yetu ambayo sasa hivi yanatuzalishia umeme, hakuna ukarabati, kwa maana hiyo anapokuja ku-*windup* atueleze kwamba haya mabwawa ambayo sasa hivi ndiyo tunafaidi keki yake, kuna mpango gani wa kuyaendeleza kwa sababu sasa hivi unapokwenda pale ukiangalia ile mitambo imechakaa. Kwa nini tusiipangie mipango ili ikawa nayo ni mazuri iendelee kutupa umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la mafuta; kwa kweli suala la mafuta napongeza bei ambazo zimetangazwa kwa sababu zimekuja kuleta unafuu mkubwa kwa Mtanzania. Kwa mfano, Dar es Salaam imepata ruzuku ya kila lita ya *petrol* Sh.306 lakini *diesel* Sh.320. Hii ni nafuu kubwa Mheshimiwa Rais anapaswa kupongezwa, lakini pia Wizara imefanya kazi nzuri, tunategemea kwamba huu mpango utakuwa ni endelevu na wananchi wapate nafuu waweze kufaidika na hii hali nzuri ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nataka kuzungumzia hii *TPDC*. Hii *TPDC* ina mchango mkubwa kwa Taifa, tuliiunda wenyewe na kwa ajili ya kufanya biashara ya mafuta, lakini cha kushangaza mtaji wake wote umemegwa na *TANESCO* na sababu ni nini? *TANESCO* wanauziwa umeme kwa kutumia gesi, lakini hawalipi, sasa leo unakuja kutuambia unaanzisha vituo vya TANOIL, yaani unaandaa nguo za mtoto lakini mama unampiga viboko atazaaje huyu mama… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mohamed Said Issa. Tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, ajiandae.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wabunge tupitishe hii bajeti kwa sababu mimi vitongoji vyangu 374 tayari nimeshavipeleka *REA* na Januari nazunguka navyo kama unavyo nitakutumia tu sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya kusema hayo naomba mchango wangu uwe wa picha kidogo usiwe wa jimbo tu. Ni kwamba wakati tulitengeneza *plan* yetu ya miaka mitano tukawa tunasema tutaishia 2025 ilikuwa hivi; *GDP per capita* yetu lengo letu lilikuwa kufikia dola 3,000 na kufikia hapo tulikuwa na mipango au tunayo mipango ya umeme jumla *installed capacity* kuwa *megawatt* 10,000 mpaka *megawatt* 15,000 na ndugu zangu Wabunge nawaomba niwaeleze ukitaka uchumi ukue kwa zaidi ya asilimia nane kwenda asilimia kumi, unahitaji umeme mwingi na wa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya sasa ya senti 11 kwa *unit* bado ni umeme wa bei ghali. Sasa tulivyosema kama tukishindwa kufikia *megawatt* 10,000 mpaka 15,000, wakati tukiwa *GDP per capital* ya Dola 1,500 yaani nusu yake, tunapaswa kuwa na umeme *installed capacity* ya

*megawatt* 5,000. Ndiyo maana ukiangalia kwenye *document* za Serikali zimewekwa kwamba kufikia mwaka 2025 tunapaswa kuwa na *megawatt* 5,000. Kwa hiyo, niwakumbushe tu kuwa na *megawatt* hizo ni lazima tuwe na vyanzo vingi, tujadili kila vyanzo lakini tusing'ang'anie kimoja, viwili bado hatutafikisha *megawatt* 5,000. Lengo letu ni *megawatt* 5,000 ifikapo 2025. Kwa hiyo, bado ndiyo maana nasema tupitishe hii bajeti ili kusudi tufike huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa upande wa umeme na maendeleo lazima ujilinganishe na ushauri wangu kwa Wizara nimeshawapatia Vitongoji 374, lakini mimi kuangalia maendeleo ya upatikanaji wa umeme nchini sitahesabu Vitongoji wala Vijiji, nitachukua hesabu ambazo zinatumika Kimataifa. Sasa Kimataifa unachukua *unit* ambayo Wizara inapaswa kutuambia ni *energy per capital,* yaani tukitupia vyanzo vyetu vyote tukagawa na *population* ya Milioni 62, je kila mtu ana *unit* ngapi, hizo ndizo zinahitajika. Lakini nzuri zaidi Vitongoji nimewapa nitakachoenda kuangalia mimi je, watu wa Kitongoji 'X' ni wangapi wanatumia umeme, ndiyo kipimo muhimu sana. Kwa hiyo, kwenye ripoti ya Wizara ninaomba mtoe ripoti ya *energy per capital* halafu mtoe *electricity energy consumption per capital*. Ukichukua hivyo vipimo unakuta kwamba Kenya, *IMF* inasema mwaka 2002 *GDP per capital* ya Kenya itakuwa Dola 2,252 na ya kwetu ni Dola 1,260.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wenye *GDP per capital* ya dola 1,260 Tanzania, *installed capacity* yetu ambayo imeandikwa Kimataifa na hiyo huwezi ukaidanganya kwa sababu unavyonunua *turbines* duniani wanaweka kwenye *database,* kwa hiyo wanajua nchi fulani wana uwezo wa kuzalisha umeme kiasi fulani. Kwa hiyo, *installed*

*capacity* yetu ambayo iko *reported Internationally* ni *megawatt* 1,605.86. *GDP per capital* ya Kenya ambayo ni 2,252 wanazo *megawatt* 2,840, kwa hiyo lazima tushindane na Kenya kwa sababu alivyokuwa anaeleza Waziri *transmission lines* tulizozijenga za *400KV* kupita Namanga na *400KV* kwenda Zambia nia kubwa ni kununua umeme na kuuza umeme ndiyo uchumi wa kisasa duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ili tuweze kuwa na umeme mwingi tuendelee na hii miradi, *energy mix* yetu Tanzania ambayo ipo kwenye vitabu vyetu tumesema tutazalisha umeme kutokana na *natural gas* ya kwanza, pili itakuwa *hydro*, tatu itakuwa ni *coal* na nne itakuwa ni *renewable energies*. Sasa *renewable energies* zipo zaidi ya 11 lakini wengi wanajua *solar* na *wind*, lakini zipo 11 hiyo nayo kuna siku nyingine tutajaribu kuijadili. Lakini ukilinganisha na Kenya sasa, maana yake Kenya waliwahi kutuomba tuwauzie *megawatt* 1,000 ya umeme walivyokuwa wanaona miradi yetu inaenda kasi lakini sasa unaona wanatuzidi. Kwa hiyo sidhani kwamba wanategemea sisi tuwauzie umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia Kenya wanavyofanya vizuri, kwenye *geothermal* wanazo *megawatt* 863, ndiyo wanaongoza Afrika kwa kuwa na *megawatt* 863, halafu Waheshimiwa Wabunge mmesikiliza michango humu matatizo ya ku-*develop geothermal* siyo kwamba yako Wizara ya Nishati havihusiani kabisa, *completely outside the scope of the problems of geothermal energy development in the country, completely out*. Kenye *wind* wanazo *megawatt* 437 linganisha na Tanzania, *solar* wana *megawatt* 173 sasa hizi nazitaja kwa sababu Tanzania tupo kwenye *East African Power Pool*, lazima tuuziane umeme. Halafu tuko

kwenye *SADC Power Pool* kwa hiyo nadhani Mheshimiwa Waziri Wizara yako inavyotoa ripoti nzuri za Kitaifa lazima zionyeshe hali ya umeme ndani ya *East Africa* na ndani ya *SADC* kwa sababu sisi tunanunua umeme Uganda, sisi tunanunua umeme Zambia, sisi tunanunua umeme Kenya ndiyo maana tumejenga *transmission lines* tuzalishe umeme mwingi na sisi tuanze kuuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikiacha suala la umeme kwa ajili ya muda ninakuja kugusa kidogo kwenye mambo ya *oil and gas*. Muda usiponiruhusu nadhani nitaongea kwenye bajeti ile ya fedha kuhusu uchumi na *gas*. Kwenye *oil and gas* upande wa *TPDC* ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge ushauri wangu ni *TPDC* ambayo ilianzishwa mwaka 1969 iachwe na majukumu yake. Haya ya biashara ya mafuta kwa sababu waliopo pale *TPDC* ni Ma-*geologist*, Ma-*geophysics, Seismologists, Geochemists* wewe unawapeleka kwenye biashara ya mafuta haviendani na siyo eneo lao hilo! Kwa sababu *TPDC* bado kazi wanayoifanya hawajaifanya hata kwa asilimia 20. Wewe muulize *TPDC* inapaswa kutueleza Je, Tanzania kuna mafuta? ndiyo maswali tunauliza *TPDC*! Siyo kuuliza *TPDC* mafuta kwenye *petrol stations* za *MOIL* hapana! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapaswa kuiuliza *TPDC* Je, Tanzania tunayo *gas* kiasi gani? Kwa mfano, sasa hivi Tanzania ni nchi ya 10, unajua wengi wanaongea tunayo *gas* nyingi, sisi ni wa 10 kwenye *reserves* kwa Afrika kwa dunia itakuwa kwenye mamia naongelea Afrika. Kwa hiyo ukiangalia Afrika ya kwanza Nigeria ina *TCF* 209, Algeria 159, Senegal 120, jirani yetu Msumbiji ana ripoti 100, lakini ambayo wanayo hawajaripoti wako kwenye 200. Ndiyo maana *TPDC* mimi sitaki iingie kwenye mambo ya kununua na kuuza mafuta kwa sababu hii *gas* 200 *TCF*

za Msumbiji wamezipata *Province ya Capo Delgado*, ni kwenye Ruvuma *basin*. Sisi Ruvuma *basin* hatujaanza kufanya *exploration*, utaitoaje *TPDC* kwenye *exploration* na huko Kusini ndiyo tunayo *gas* nyingi kuacha hii tuliyonayo. Kwa hiyo, pendekezo langu mimi ni kwamba *TPDC* iwezeshwe na lakini siyo kununua na kuuza mafuta, iwezeshwe kufanya *exploration*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna hii nafasi iliyopatikana vita ikipiganwa duniani, *European Union* asilimia 40 ya *gas* yake inanunua kutoka Russia, hizo ni 155 *billion Cubic metric tons*, 40 *percent*. *European Union* imezunguka nchi za Kiafrika kujaribu kununua *gas* lakini haijaja Tanzania kwa sababu sisi bado! Ndiyo maana *TPDC* waachwe kwenye *core mission* yao ya *oil and gas exploration and development*. Hata lile jina lenyewe jamani *TPDC*, *Tanzania Petroleum Development Cooperation*, haliitwi *Tanzania Development Trade,* unaona ile 'T', unaona tofauti hapo? Kwa hiyo tuwaache *TPDC* huko. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Mengine nitaongea siku nyingine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Profesa. Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea na wachiangiaji niliowataja kuna matangazo mawili madogo hapa.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la kwanza ni kutoka Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye amemtaka Mheshimiwa *Captain* Mstaafu George Huruma Mkuchika

akaimu nafasi ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo. Kwa hiyo, naona Mheshimiwa *Captain* Mstaafu yuko tayari hapo kwa hiyo atakuwepo mpaka wakati ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu atarudi. *(Makofi)*

Pia, kuna tangazo la wageni ambao wametembelea Bungeni jioni hii na ambao ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni pia wa Mheshimiwa Ali Juma na Mheshimiwa Maulid kutoka Zanzibar pamoja na wageni wengine wote, naomba msimame kwa ujumla wenu. Karibuni sana wageni wetu kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo na Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, ajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia na mimi fursa angalau nitoe mchango wangu kwenye Wizara hii muhimu ya nishati katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, yale maonesho ya nishati waliyotuletea pale kwa kweli yametujibia maswali mengi mbayo pengine tungeyaleta hapa na ingetuchukua muda mrefu kuzungumza, lakini tuliutumia ule muda vizuri kwenye mabanda yale kwa hiyo tumepata majibu sahihi. Ni ombi langu sasa yale ambayo tuliambiwa yakafanyiwe kazi siyo kwamba baada ya bajeti kupita sasa waka-*relax* waje watuletee mabanda tena mwakani. Tunataka kazi kule *field,* mambo yaonekane tuwashe umeme vijijini mwetu kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika moja ya mambo ambayo mimi ningeenda kuuliza isingekuwa yale maonesho ilikuwa ni vile vijiji ambavyo vilisahaulika kwenye ile *survey* ya mwanzo ama *list* ya mwanzo ambayo iliorodheshwa ya vijiji ambavyo vinaenda kupatiwa umeme. Kwangu nilikuwa na vijiji Tisa ambavyo ni Mdilu, Mwasauya, Mwakincheche, Itamka, Mwigh'anji, Endeshi na Sefonga lakini vijiji hivi tayari vimeingizwa. Ninachoomba sasa na wenyewe *survey* ikafanyike ili nao wapate matumaini na wao sasa kupata umeme, maana yake mpaka sasa hakuna kilichofanyika pamoja na kwamba tayari vimeshaonekana kwenye orodha kwamba watapatiwa huduma hii ya umeme. Kwa hiyo, ile kufanya *survey* itaonyesha kwamba kweli sasa kazi inaenda kufanyika na wao wanaenda kuwasha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo ni la muhimu sana tunalolipata kule kwa wananchi ni ile kilomita moja. Kwamba umeme unakwenda kilomita moja tu kwenye Kijiji sasa ile haikidhi haja, ni eneo dogo sana. Ninashukuru sana Mheshimiwa Waziri katika *presentation* yake amesema kwamba kuna timu ambayo inaenda kukaa na kufanya utafiti zaidi, kufanya tathmini ili kuongeza angalau iongezeke iende hata kwenye kilomita tatu mimi naona hiyo ni sawa, angalau kilomita tatu itafikia kukidhi vigezo au kukidhi kuwapatia wananchi wengi huduma hii. Ukizingatia vijiji vyetu ni vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwangu nina vijiji vikubwa unakuta Kijiji kimoja kina vitongoji mpaka vinafika zaidi ya kumi. Mathalani Kitongoji cha Sokoine kikubwa kina hadhi ya Kijiji, Songa kina hadhi ya Kijiji, Kwaye na Mapinduzi na vina huduma za Taasisi za Umma, vina shule, vinavyo hospitali wakati mwingine na

vina shughuli za kijamii zinazoendelea zinazohitaji umeme. Lakini kwa sababu tumesema ni Kijiji basi umeme unapelekwa pale Kijijini tu kwenye *center* jamii iliyo kubwa inaachwa haijapata huduma. Kwa hiyo, ninashauri na ninapendekeza maeneo haya kiwango kile cha kilomita moja kiongezeke ili wananchi wetu waneemeke na hii huduma. Na ni-*appreciate* kwamba nchi yetu ni miongoni mwa nchi nadhani ipo kwenye *top three* za *rural electrification* kwa hiyo ni hatua muhimu na sisi tunaiunga mkono lakini ifanyike iendane na wakati ili sasa tuonde na hili tuende kwenye programu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine la muhimu ambalo hili nadhani *TANESCO* walichukue. Kuna wananchi ambao wamepeleka maombi, wameshajaza fomu, wamefanya *wiring* muda mrefu wengine zaidi ya miezi sita lakini mpaka kesho hawajawahi kuunganishiwa umeme. Wakienda wanaambiwa mara *generator* sijui limefanyaje, mara waya sijui nguzo zimefanyaje, mwananchi hataki kujua habari za nguzo yeye anataka umeme uwake. Kwa hiyo, niwaombe sana ndugu zetu wa *TANESCO* kwa kuwa tuliowana hata siku ile tuliwaeleza haya, mlitusikia basi naomba haya malalamiko yaondoke, wananchi waliyofanya *wiring* waunganishiwe umeme ili waache sasa na wao kulalamika, waneemeke na hii huduma. Mathalani pale Kijiji cha Mughamu na Kinyasatu ni zaidi ya nyumba 40 wamefanya *wiring* lakini hawajapata huduma, pale Miangae, Kinyeto wamefanya *wiring* muda mrefu lakini hawajapa huduma. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri ulichukue hili angalau tuwapatie watu hawa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru tena pia katika hii programu inayoendelea kwangu nilikuwa na vijiji 31 ambavyo vilihitaji umeme lakini kwa habari njema ni kwamba katika programu inayoendelea sasa hivi kuna vijiji nane ambavyo vinaenda kuwasha umeme kabla ya Tarehe 15 ya mwezi huu. Mimi nalipongeza sana Shirika letu la *TANESCO*, naipongeza sana Wizara, hata Mkandarasi wa ile *Central Electrical* ambae anasimamia mradi huu kule Jimboni kwangu, mpaka Tarehe 15 amenihakikishia kwamba vijiji nane vinakwenda kuwashwa umeme. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri siku hiyo uje tuambatane na wewe tukawashe umeme tukaone taa pale zikiwaka, vijana wakifurahi, wakipokea fursa hii kwa mikono miwili na kwenda kuchangamkia sasa fursa za viwanda na mambo mengine yanayohitaji umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji ambavyo vinaenda kuwashwa umeme nawaomba wananchi wangu wajiandae ni Kijiji cha Muhango, Kijiji cha Mvae, Kijiji cha Kinyagigi, Kijiji cha Munkhola, Soghana, Mwanyonye na Kiyunadi hawa ninaomba sana Mheshimiwa Waziri ujiandae ili siku hiyo ikifika tuondoke mimi na wewe mguu kwa mguu tuhakikishe umeme unawaka kama ambavyo nimeahidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine na la mwisho kabisa ni umeme wa upepo pale Singida. Walizungumza nadhani wasemaji wawili waliotangulia hapa kuhusu huu umeme wa upepo. Nchi yetu ina uhitaji mkubwa sana wa umeme na tunafahamu gharama kubwa tunayotumia kupata umeme. Sasa kuna huu umeme wa upepo ambao unapatikana Singida, *investment* yake wala siyo kubwa, lakini kuna Kampuni ambayo imejitokeza muda mrefu zaidi ya miaka tisa sasa ya Upepo *Energy* mpaka

leo tunaambiwa majadiliano yanaendelea, mazungumzo yanaendelea ile michakato tunayolalamika kila siku, mara mchakato na maneno matamu matamu kwa nini hili jambo halifiki mwisho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana hili jambo sasa lifike mwisho umeme huu wa upepo utakwenda kutupatia megawati 100; lakini huyu mzabuni yeye anasema ana uwezo wa kuzalisha hata megawati 300, kwanini apewe megawati 100 tu apewe *tender* hii ya kutosha ya megawati azalishe umeme wa kutosha ili nchi yetu inufaike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, megawati 300 itapunguza tatizo kwa kiwango kikubwa sana, lakini pia kuna ule umeme wa *solar* pale Kititimo wa megawati 45 kwa nini hizi *project* hazikamiliki *tender* zake? Niombe sana Waziri atakaposimama aniambie tatizo hapa ni nini mpaka mchakato wa kazi/*project* hii isikamilike na mradi huu wa upepo kwa upande wangu kwenye Jimbo langu unakwenda kunufaisha vijiji nane ambavyo ni Msikii, Kinyamwenda, Itaja, Kinyamwambo, Miipilo, Kinyagigi na Mwanyonye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme huu ukikamilika haya maeneo yatapata umeme hata hatutahangaika na *REA* ambayo tunasema inakwenda kilometa moja, huu utapanua wigo utakwenda hata maeneo mengine.

Kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwa na yeye ni kijana mwenzangu atanisikia na yeye kwanza ni msikivu, ni mtu ambaye ni mzalendo. Kwa hiyo, niombe sana alichukue hili atakaposimama hapa aniambie nini sasa kinakwenda kufanyika kuhusu *project*

hizi mbili; huu *upepo energy* pamoja na ule wa *solar*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya niunge mkono hoja na niwasilishe ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, tunaendelea na Mheshimiwa Ahmed Shabiby na baadaye Mheshimiwa Nusrat Hanje ajiandae.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuwa mmoja wa wachangiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitaanza kwa upande wa *TANESCO* na ninataka niseme kwamba Mheshimiwa Waziri kwa upande huu pamoja na Naibu wako Bunge lililopita mliongea vitu vizuri sana kuhusu mipango yenu ya kusambaza umeme kwenye nchi hii na sehemu mojawapo uliyoigusa ilikuwa ni katika eneo la Jimbo la Gairo na maeneo ya Mpwapwa, Kongwa na sehemu nyingine ambayo tunatumia *line* moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Waziri anakumbuka nilishakwenda kumlalamikia mara nyingi maeneo ya Gairo umeme unakuwa unakatikakatika sana na mojawapo ya sababu ni nguzo kuanguka hizi za miti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa bahati nzuri sasa hivi tunaona mnabadilisha mnaweka nguzo za zege, lakini hizi nguzo nazo naomba kwa ushauri wangu mjaribu kuziangalia. Hizi nguzo za zege ni fupi kuliko nguzo za umeme zile za miti hata mkiziangalia barabarani unaona ni vifupi vifupi na katika maeneo haya ya kuja Dodoma

maeneo haya mpaka kule Gairo watu wengi wanajenga. Kwa hiyo, sasa mtawapa watu usumbufu wenye vile viwanja, *otherwise* mtaanza tena kuwaambia nunua nguzo ndefu ili labda kama kuna magari yanapita au nini kwa ajili yasiguse. Kwa hiyo, tunaomba muwe makini kwenye nguzo mzidishe kidogo urefu wa nguzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba uharakishaji wa kile kituo cha kupooza umeme, kwa ajili ya kupata umeme wa kuanzisha viwanda katika maeneo hayo niliyoyataja kwa sababu sasa hivi huwezi ukaanzisha pale kiwanda cha mafuta wala kiwanda cha sembe kwa ajili umeme ni mdogo na bahati nzuri Gairo tuna bahati moja, katika Wilaya ya Gairo tunatumia umeme wa aina mbili; tunatumia umeme wa Bwawa la Kidatu na tunatumia umeme wa Bwawa la Mtera. Kwa hiyo, tunatumia umeme pote, pale pana *switch* kwa hiyo umeme wa Dodoma ukikatika tunawasha wa Morogoro lakini uwezo nao wa umeme ni shida.

Kwa hiyo, tunaomba na kile kituo cha Morogoro-Msamvu toka ile transfoma kubwa iungue hamjaweza kuweka tena transfoma kubwa. Tunajua mna mipango, lakini tunaomba ile mipango mharakishe kwa sababu mipango ya transfoma ile ndio itaweza kuweka umeme mkubwa Morogoro Mjini, Mvomero, Kilosa, Morogoro Vijijini pamoja na Gairo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo yanajitokeza bahati nzuri nawashukuru *REA* pamoja na *TANESCO* kwamba vijiji vyote vya Gairo vimo kwenye programu ya umeme na vimeshapata umeme, kasoro vijiji vya Tarafa ya Nungwe ambayo kuna milima mikubwa sana kama ya Lushoto. Sasa pale wakandarasi wa *REA* wameweka umeme karibu vijiji vyote, lakini kuna kisehemu ambako

wako *TFS,* kuna misitu kama mita 400 au mita 300. Sasa wale hawataki kuachia ule msitu ili zile nyaya zipite wanadai shilingi milioni 400. Sasa mimi nashangaa Serikali kwa Serikali mnadaiana fedha ili wananchi wapate huduma, wakati wananchi wangu wamekubali kutoa mashamba yao na maeneo yao bure kupeleka huo umeme na hata hao wenyewe watu wa *TFS* watafaidika na huo umeme kwa sababu mashamba yao ya miti yale yatapata mashine sasa za kutumia umeme badala ya majenereta na dizeli kwa hiyo tunaomba hilo ulishughulikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ahadi ya Waziri aliyepita Mheshimiwa Kalemani ya gari pale Gairo baada ya kuona yale maeneo ya mlimani na alisema pale pale na aliongea na Mkurugenzi aliyepita kwamba iende pale gari, zilikuwa gari mbili *TANESCO* moja iende Gairo lakini sasa sijajua je, haya matamshi ya Mawaziri akiondoka linakuwa la kwake binafsi au linakuwa la Kiserikali na Wizara? Naomba ile gari ya Gairo ya *TANESCO* ifike, tuliongea na wewe, tulimtafuta Mkurugenzi wa *TANESCO* lakini hatukumpata, naomba ile gari iliyoahidiwa kwa sababu ilikuwepo, tunaiomba ile gari yetu iwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni masuala ya bili za umeme. Bili za umeme ni shida sana, yaani kwa mfano nianze na watumiaji wadogo, yaani mtumiaji mdogo akiwa anaweka umeme wa shilingi 20,000 siku akijiroga tu labda awe na LUKU tu lakini kwa mfano kama ana mita siku akirogwa akiweka umeme wa shilingi 50,000 hata akifunga nyumba wale watakuja na umeme wa shilingi 50,000. Kwa hiyo, nikuambie Mheshimiwa Waziri *TANESCO* na Wizara yako usione watu wengi sana wamechomoka chomoka humu kwenye Uwaziri hata Mheshimiwa

Muhongo, akina Mheshimiwa Kalemani, akina nani na nani sio kwamba walikuwa hawafai, walikuwa wanafaa, lakini watendaji wengi kwenye *TANESCO* ni matatizo. Kwa hiyo, unaliendesha halmashauri maana yake *TANESCO* na Wizara yako ni kama halmashauri fulani ya Wilaya hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mazingira mabovu mabovu ni mengi sana humo ndani, kwa hiyo wanafanya *timing*/kupanga na mimi nimekurushia bili mbili, wewe pamoja na Naibu wako. Kuna sehemu unatumia umeme kuna kitu kinaitwa *KVA* ile *KVA* ni nini? Mbona haieleweki maana yake unakuja mtu unaambiwa hapa umeme *per unit,* labda kwenye wale wanaotumia umeme mkubwa sasa wa viwanda na nini kama alivyosema Mheshimiwa Muhongo kwamba hamuwezi kuendelea bila kuwa na umeme mkubwa na wa bei rahisi. Lakini unapewa *unit* unaambiwa *unit* zako ulizotumia ni hizi bei yake ni shilingi milioni sita, halafu unaambiwa kuwa *KVA* shilingi milioni tatu halafu *plus VAT*. Sasa ukiangalia hii *KVA* hujui unaipata wapi, wala haisomeki mahali popote *KVA* ni kitu gani haijulikani ukiwauliza unaambiwa, unajua umeme ukizima ukiwaka unavyokuja kuwasha mitambo yako pale ndio hii *KVA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huo unawaka kila siku unawaka tu, kwa hiyo kila mwezi na nilikurushia kwa mfano moja kwa jengo moja la Morogoro na lingine la Dodoma; la Dodoma matumizi makubwa KVA shilingi milioni mbili katika shilingi milioni 10 *KVA* shilingi milioni mbili, jengo lingine la Morogoro matumizi shilingi milioni sita *KVA* shilingi milioni tatu. Sasa hii yaani tunaonekana kama ni aina fulani ya ujanja ujanja ambao hauna sababu yoyote ya msingi.

Kwa hiyo, hili neno *KVA* kama mnataka *KVA* iwepo basi bora muongeze tu bei kwenye *unit* na mtu anasoma, halafu hamumletei mtu zile mita zenu mnayofunga kubwa mtu hana *access* ya kusoma. Kwa hiyo, mpaka wewe umletee bili unavyotaka wewe, kwa hiyo unaweka unavyoandika wewe, sasa mteja anapata wapi mahali pa kuangalia pale? Kwa hiyo, hapo tunaomba sana mshughulike na hili suala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nimeshazungumza sana masuala ya mafuta kuna sehemu umeyatekeleza tunakuunga mkono kwa hilo na tunajua wewe hujui chochote kwenye hii Wizara mgeni, lakini nataka nikuambie wewe ni mgeni, Katibu Mkuu ni mgeni Naibu Katibu Mkuu ni mgeni na Naibu wako Waziri ni mgeni. Nilishawahi kujaribu kuongea na wewe siku moja na ulishuhudia kitu nilichokuambia ukakishuhudia mwenyewe na ukakiamini.

Sasa nataka nikuambie haya mambo ya mafuta tunavyochangia najua mnahangaika sana watu wako kutujibu jibu hata kwenye ma-*tv* na nini, kama yule mmoja Kamishna wa Mafuta anahangaika anasema waliongea Wabunge na sisi mkitujibu na sisi tunajibia hapa, umeona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema hawa Wabunge mafuta yakija na mmehangaika sana, wameita hata semina juzi za Kamati tatu tu kuja kuwaweka sawa pale Hazina, lakini nataka nikuambieni sisi hatuchangii wala hatuchukii mtu, sisi tunachangia kwa sababu tunapenda nchi yetu na tunavyovichangia tunajua, unaweza ukawa profesa wa biashara lakini hujawahi kufanya biashara, unaongea kwa maneno. Unaweza ukawa profesa wa kilimo, lakini huna hata heka moja, kwa hiyo hujui hiyo

biashara. Mtu anakuambia nikiagiza mafuta kwa kila mtu nchi italeta mafuta machafu, nchi itapata sijui upungufu wa mafuta toka enzi ya Nyerere, kaja Mwinyi, kaja Mkapa, kaja Kikwete mpaka mwishoni, tuonesheni nchi hii ilipata upungufu lini na ilikuwa inatumia *system* hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa inatumia *system* hiyo lini ilipata upungufu? Hakuna kitu kama hicho na mimi najua kabisa Mheshimiwa Waziri, wewe hujui lolote na ndio maana nilikuambia ukitaka ufanye vizuri hata hawa *EWURA* safisha kitengo cha…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Shabiby.

**MHE: TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa msemaji Mheshimiwa Shabiby kwamba *TPDC* toka mwaka 1970 inafanya biashara ya mafuta mpaka mwaka 2002, nchi hii ilikuwa haijapata kukosekana kwa mafuta na ilifanya kazi ya kutafuta petroli na *TPDC* ikafanya kazi ya kuuza mafuta na bei zikawa nzuri katika nchi hii ahsante endelea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shabiby unaipokea taarifa?

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yoyote inayokuja mimi napokea. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wangu na Katibu, hebu jaribuni kuangalia juzi nilikuonesha kitu kimoja tu na nikakuambia twende tukapige simu huko uangalie bei za mafuta ni hizi? Kwa hiyo, sisi hatujasema hatutaki *bulk*

*procurement,* tumesema iwepo lakini ipate ushindani na wawepo na watu binafsi, hakuna mtu amekataa *bulk procurement* isiwepo iwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hebu ingieni basi hata angalau angalieni kwenye gesi mlitaka muweke *bulk procurement* wale watu wa gesi wamekataa, leo gesi katika Afrika, Tanzania ni nchi ya kwanza yenye bei rahisi kuliko nchi yoyote ya Afrika, hamjiulizi swali na iko chini ya Nishati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao wataalam wanaokupakupa utaalam wewe ni utaalam wa maneno na wa masilahi, mimi narudia kusema hayo maneno. Kuwa mwenyewe na msiweke mtu wa kati. Mnaposema kwamba haya makampuni 28 yameomba kuomba kuleta mafuta, lakini tumechagua sita sasa sisi tunakuwa na uhakika gani si sita yale yale mnayoyapenda? Ninyi mruhusuni kila mtu alete na ile *bulk procurement* iwepo hiyo ndio ukweli, halafu nilitaka ujiulize swali moja tu na Wabunge wote mjiulize, angalieni toka wakati wa *bulk procurement* ilipoanza *petrol station* sasa hivi zinaota kuliko shule za kata. Sasa hapo mjiulize na kuna vitu vingine mimi nataka nikuambie ukweli mimi nitakupa kwa maandishi, sitaki nikupe ushahidi wa maneno maneno ninayoongea hapa, nitakupa kwa maandishi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua wako wengine wamepata shilingi 2,000/shilingi 3,000 hapa hao tuachane nao, kuna watu duniani hawapo na mbinguni hawajafika wanaelea katikati tu umeona bwana. *(Kicheko)*

Mimi nataka nikupe kwa *document,* sitaki kuongea kwa mdomo nitakupa kwa *document* na ninashukuru

kwamba umekubali ukaniambia kwamba nikuletee utafanyia kazi. Mimi naomba uliangalie, je, kweli kuna ukweli na hata Mbunge anayetaka naye aje nimueleweshe halafu aone tunavyotandikwa, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ahmed Shabiby, tunaendelea na Mheshimiwa Nusrat Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitanukuu maneno ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwaka 1962 alipata kusema; "hatuwezi kutatua matatizo yetu kwa kujidanganya kwamba hayapo." Wizara hii ni Wizara ambayo mimi naweza nikaichukulia kama Wizara ya mfukoni kwenye pochi la mama, kwa sababu mama ameweza kutoa shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kusaidia kushusha bei ya mafuta ambayo imeonekana inaathiri wananchi wengi sana wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa masikitiko makubwa sana leo mpaka tunafunga Bunge saa 7.00 mchana bado Wabunge walikuwa hawajapata taarifa ya Kamati kuona mapendekezo ya Kamati kwa sababu ya unyeti wa *information* ambazo Wabunge wangeweza kusaidia/kumsaidia mama ili fedha aliyoitoa asione kama imepotea kupeleka kwenye sehemu ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo niwapongeze sana Wabunge wenzangu kwa sababu wamejitahidi kutafuta taarifa nyingine sehemu nyingine na wameendelea kusaidia kuchangia kwenye kuona

namna gani tunaweza tukasaidia Taifa letu na isionekane kama Serikali imepoteza fedha, kwa sababu tunahitaji fedha mno kuna miradi ya barabara, kuna miradi ya hospitali, kuna miradi ya shule, lakini mama ameona apeleke upande wa mafuta kwa ajili ya kupunguzia Watanzania gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tarehe 25 Mei Mkoa wa Singida mzima ulikatika umeme na kwenye mitandao ukaonekana kibonzo kinasambaa kwamba mtu anasema Singida nzima umeme umezima halafu mwenzie anamjibu kwamba unaishi Singida kwani wewe ni alizeti? *(Kicheko)*

Mimi kama Mbunge wa kutoka Mkoa wa Singida kwa mpango huu ambao nimeona na namna ambavyo Mkoa wangu umetajwa kwenye bajeti ya Nishati, ninasikitika kwamba inawezekana Serikali inafikiri wanaoishi Singida wote ni alizeti. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mingi tumekuwa tunajadili kuhusiana na umeme wa upepo Mkoa wa Singida na kila Mbunge wa Mkoa wa Singida anayesimama anaongea kwa sababu kuna uwezekano mkubwa sana wa umeme wa upepo Mkoa wa Singida ukasaidia wananchi wa Mkoa wa Singida, lakini pia ukasaidia watanzania wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka tunapozungumza Singida ni miongoni mwa Mikoa ya Tanzania ambayo miundombinu yake na upatikanaji wake wa umeme bado unasuasua. Ukisoma bajeti ya Wizara ya Nishati inaonesha kwamba wana-*respond* (wanaitikia) ile mipango ya maendeleo endelevu *SDGs* namba saba ambayo inalenga kutoa upatikanaji wa nishati safi ya

uhakika na gharama nafuu. Lakini nasikitika sana mimi nimezaliwa kijijini kwenye giza, kwa taarifa za waliokuwepo wakati nazaliwa wanasema nilizaliwa kijijini kabisa kwenye giza, kwa hiyo, ninasikitika sana kwamba mimi nakaribia kuzeeka bado Watanzania wamama wa Singida wanajifungulia kwenye vibatari na giza kwa sababu bado Singida hospitali hazijaunganishwa kwenye umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana na jambo hili sio geni, Wabunge wengi sana wanaotoka vijijini wanajua kama Watanzania bado wanajifungua kwenye vibatari, bahati mbaya hata bei za mafuta zinazotegemewa kushuka bei ya mafuta ya taa bado haijaguswa kabisa. Mimi natoka mkoa ambao sehemu kubwa ni vijijini, kwa hiyo, watumiaji wa vibatari na taa za chemli bado wapo ni masikitiko yangu makubwa sana. Kwa sababu mimi ni mama wa Mkoa wa Singida, naomba nitaje katika Wilaya ya Ikungi zipo zahanati ambazo hazijaunganishwa na umeme. Bahati mbaya sana katika Wilaya ya Ikungi zahanati 33 hazijaunganishwa na umeme lakini pia bahati mbaya zaidi Jimbo la Singida Magharibi zahanati 20 hazijaunganishwa na umeme mpaka tunapozungumza na umeme umepita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wananchi wanakwenda hospitali, wanatumia tochi, mama anajifungua kwa kutumia tochi anatoka nje anaangalia umeme umepita juu. Zahanati ya Kintandaa, zahanati ya Mtunduru, zahanati ya Ihombwe, zahanati ya Msosa, zahanati ya Mgungira, zahanati ya Yumbu, zahanati ya Mwaru, Ntuntu, Minyuhe, Iglansoni, Muhintiri, Nduru, Mpugizi, Mnang'ana, Kipunda, Songandogo *and the list goes on*. Inasikitisha mno Ubunge wangu mimi

mwanamke kutoka Singida hautakuwa na maana kama tutaendelea kuacha akina mama wajifungue kwa kutumia tochi za simu, haiwezekani. Bajeti ya Wizara ya Nishati imeongezeka asilimia 13; kuongezeka kwa bajeti hii kukatoe tafsiri kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania hawajui miradi mikubwa na tunaipongeza, lakini niseme tu matumaini ambayo ninayo kama mimi kwa sababu mimi pia Mjumbe wa Kamati miongoni mwa miradi ambayo imepewa fedha kubwa sana katika ongezeko la bajeti ambayo imeongezeka ni pamoja na umeme wa *REA* Vijijini.

Kwa hiyo, Watanzania waelewe na tunategemea huwa nashangaa kwa nini Serikali wakati inaweka mikakati haiangalii maeneo muhimu? Hatuwezi kujadili kupeleka umeme shule, kupeleka umeme kwenye mahakama bila kujadili hospitali? Mimi naweza nikalala nyumbani kwangu na kibatari, lakini nakwenda kujifungua hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za afya zinategemea umeme, kuna vipimo vingine lazima utumie umeme. Kwa hiyo, wakati unapanga na tunategemea *REA* kwa ongezeko hili na wao ni sehemu ya kipaumbele watumie ubunifu wao wote kuhakikisha kwamba kipaumbele cha kwanza kinakuwa kuunganisha vituo vya afya na zahanati zetu ili akina mama ule mzigo ambao Mheshimiwa Rais alisema kwamba mzigo wa usawa wa kijinsia kwenye mabega yake ni mzito zaidi, kwa sababu ni aibu tuna Rais mwanamke, halafu kuna watu ambao wanatakiwa wamsaidie ili wanawake wenzake wasijifungulie kwenye giza, lakini wasaidizi wake inaonekana wanashindwa kumsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana kwa niaba ya akina mama wa Tanzania tunaomba muwasaidie wanawake kuunganisha hospitali umeme ili waweze kupata huduma za afya kwa mazingira ambayo ni rafiki ili waweze kufanya kazi ambazo zitasaidia wao kuchangia Pato la Taifa, tumsaidie Mheshimiwa Rais kufanya kazi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nusrat Hanje.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa siku ya leo umefikia mwisho, niwashukuru na kuwapongeza sana kwa kazi nzuri ambayo tumefanya toka asubuhi, michango ni mizuri, naamini kabisa Mheshimiwa January, Waziri wa Nishati pamoja na Naibu wake wamewasikiliza vizuri sana na yale yenye maslahi kwa Taifa letu na ambayo yanawezekana kwa sasa hivi watayafanya na ya baadaye watayafanya, basi tuwe na matumaini na tuwaombee kila la kheri waweze kufanya yale ambayo tunayatamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kuna tangazo dogo sana kutoka kwa Mheshimiwa Seif Gulamali, Meneja wa Timu ya Bunge anawatangazia Wabunge wote kwamba kutakuwa na mazoezi kwa Wabunge viwanja vya Jamhuri na Chinangali kuanzia saa 12.00 asubuhi. Kwa hiyo Wabunge wote mnakaribishwa mazoezi ni muhimu tangazo hilo linatoka kwa Mheshimiwa Gulamali.

Baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.40 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 2 Juni, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*